

TANGAZO LA SERIKALI Na. .... La tarehe .....

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(Sura ya 290)

**SHERIA NDOGO**

*Zimetugwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16 (1)*

**SHERIA NDOGO ZA (KODI YA HUDUMA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KALIUA ZA MWAKA 2014.**

- |                            |    |  |
|----------------------------|----|--|
| Jina na mwanzo wa kutumika | 1. | Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Kodi ya Huduma) za Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua za Mwaka, 2014 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali  |
| Eneo la matumizi           | 2. | Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.  |
| Tafsiri                    | 3. | Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo;-<br><br>“ <i>Afisa mwidhiniwa</i> ” maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri au mtu yeyote aliyeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi hii ni pamoja na Afisa Mtendaji wa kata au Kijiji;<br>“ <i>Halmashauri</i> ” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.<br><br>“ <i>Hesabu</i> ” maana yake ni jumla ya mauzo au manunuzi ikiwa ni pamoja na kodi na ada katika mwaka wa mapato.<br><br>“ <i>Hesabu za mwisho</i> ” maana yake ni hesabu za mwisho zinazowasilishwa na taasisi yoyote ya kibiashara baada ya kipindi cha hesabu kwa mjibu wa kifungu cha 9 cha Sheria Ndogo hizi pamoja na nyaraka au maelezo yatakayotakiwa kutolewa kwa mjibu wa Sheria Ndogo hizi;- |

“*Jumuisho*” maana yake ni taarifa, nyaraka, au hesabu au maelezo yoyote yahusuyo kiasi na thamani ya kifedha ya bidhaa au huduma zilizoanzishwa, zilizosambazwa zilizotolewa na, au kuuzwa kibiashara na ikiwa ni pamoja na jumuisho la awali au la mwisho;

“*Kipindi cha hesabu*” maana yake ni muda ambao mfanyabiashara anatakiwa kuwasilisha hesabu za biashara zake;

“*Mkurugenzi*” maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Kaliua;

“*Mwaka wa mapato*” maana yake ni kipindi cha miezi 12 ya kalenda ya mwaka;

“*Mkusanya kodi*” maana yake ni mtumishi au wakala aliyeteuliwa na Halmashauri kukusanya kodi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

“*Sheria*” maana yake ni Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura 290

“*Taasisi ya kibiashara*” maana yake ni taasisi iliyosajiliwa kwa mjibu wa sheria ya kampuni au sheria ya majina ya kibiashara inayojihusisha na shughuli za kiuchumi za uzalishaji wa bidhaa za mazao ya Kilimo, usambazaji wa bidhaa au utoaji wa huduma na, au biashara ikiwemo uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi au kikundi au mtu yeyote anayeendesha shughuli za biashara na ana leseni ya biashara.

“*Wakala*” maana yake ni mtu yeyote, kikundi cha watu, kampuni au taasisi, yoyote iliyoteuliwa na Halmashauri kukusanya ushuru kwa niaba yake:

“*Waziri*” maana yake ni waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa.

- Utozaji kodi      4.      (1) Halmashauri itatoza kodi ya huduma kwa mjibu wa Sheria Ndogo hizi kutoka kwa kila taasisi ya kibiashara au kikundi au mtu ambaye ana leseni ya biashara katika kila mwaka wa mapato ambayo ni sawa na asilimia sifuri nukta tatu (0.3%) ya hesabu ya shughuli zote zikiwemo za uzalishaji wa bidhaa au huduma kutoka nje ya nchi zinazofanyika katika eneo la Halmashauri

ukiondoa kodi ya ongezeko la thamani ya mlaji (VAT).

- (2) Kodi hiyo italipwa kwa Afisa Mwidhiniwa au wakala aliyeteuliwa kukusanya Ushuru kwa niaba ya Halmashauri
- Uwasilishaji taarifa kuhusu shughuli za kibiashara 5. (1) Mkurugenzi kwa taarifa ya maandishi anaweza kumtaka mlipa kodi au mkusanya kodi yeyote kuwasilisha hesabu zenye taarifa kamili za shughuli za kibiashara zikionyesha thamani ya kiasi na thamani ya kifedha ya bidhaa au huduma zilizozalishwa, kutolewa, kusambazwa au kuuzwa, kibiashara na taarifa ya fedha katika kipindi maalum kisichozidi siku thelasini (30) tangu tarehe ya taarifa hiyo.
- (2) Mkurugenzi anaweza kwa taarifa ya maandishi kumtaka mtu yeyote mwenye taarifa au maelezo kuhusu taasisi yoyote ya kibiashara inayopaswa kulipa kodi kwa mjibu wa Sheria Ndogo hizi, kuwasilisha kwake taarifa au maelezo hayo katika kipindi kisichopungua siku thelathini tangu tarehe ya agizo hilo.
- Uwezo wa kuingia kwenye jengo 6. Mkurugenzi anaweza kumwagiza kwa maandishi Afisa Mwidhiniwa kuingia kwenye jengo au eneo la taasisi ya kibiashara au la mlipa kodi au mkusanya kodi yeyote kwa nia ya kufanya uchunguzi na tathmini ya kumbukumbu za kibiashara, vitabu vya hesabu, na taarifa nyinginezo kama atakavyoona inafaa kufanyiwa uchunguzi kwa ajili ya kupata na kujua kiwango sahihi cha kodi anachotakiwa kulipa mlipa kodi au mkusanya kodi hiyo.
- Wajibu wa mlipa kodi 7. Kila mlipa au mkusanya kodi ya huduma atatakiwa kutoa na au kuwasilisha hesabu za awali na kulipa kodi anayotakiwa katika muda kama ifuatavyo;
- (a) Kwa waagizaji bidhaa kutoka nje ya nchi watalipa kodi katika muda kama itakavyokuwa imeelekezwa na kamishina wa kodi ya forodha na kodi ya mlaji (VAT)
- (b) Wazalishaji wa bidhaa za viwandani watalipa

kodi kama itakavyokuwa imeelekezwa na kamishina wa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) isipokuwa haitakuwa zaidi ya muda wa kulipa kodi ya mlaji (VAT)

- (c) Watu wengine watalipa katika awamu nne (4) awamu ya kwanza ikianza katika kipindi cha miezi mitatu baada ya kuanza kwa kipindi cha mahesabu.

- |                        |    |  |
|------------------------|----|--|
| Kumbukumbu za biashara | 8. | Mkurugenzi anaweza kwa taarifa ya maandishi kumtaka mlipa kodi au mkusanya kodi yeyote kuwasilisha kwake kumbukumbu za biashara na vitabu vya hesabu kwa niaba ya kupata taarifa kwa ajili ya kufanyiwa tathmini au kukusanya kodi ya huduma.  |
| Kamishina              | 9. | Mkurugenzi anaweza kumteua kamishina wa kodi ya forodha au kodi ya mapato kutathmini na kukusanya kodi ya huduma na kuwasilisha kwa Halmashauri kwa wakati kama ilivyoelekezwa kwenye Sheria Ndogo hizi chini ya kifungu cha 9 kwa lengo la kufanya tathmini, kukusanya na kupata kodi pamoja na madeni yake.  |
| Kiwango cha kodi       | 10 | <p>(1) Kiwango cha kodi kitakuwa ni asilimia 0.3% ya hesabu ya shughuli zote baada ya kuondoa kodi ya ongezeko la thamani na kodi ya mlaji.</p> <p>(2) Mkusanyaji kodi au mlipa kodi yeyote akishindwa kuwasilisha kodi yake au ya mlipa kodi, atachukuliwa kama hajalipa kodi na anastahili au kuwajibika kulipa kodi hiyo kama vile ndiye mlipa kodi ya Halmashauri na njia zote za kukusanya madeni zitatumika dhidi yake kama vile ndiye mlipa kodi husika.</p> <p>(3) Bila kuathiri masharti ya Sheria Ndogo hizi Mkurugenzi anaweza kuteua wakala kukusanya kodi kwa niaba yake.</p> |

- |   |     |  |
|---|-----|--|
| Jinsi ya kuwasilisha hesabu                   | 11. | <p>(1) kila mlipa kodi au mkusanya kodi atatakiwa kuwasilisha kwa Halmashauri hesabu za mwisho katika kipindi cha miezi minne tangu kumalizika kwa kipindi cha hesabu ya kodi anayostahili katika mkupuo mmoja.</p> <p>(2) Iwapo mlipa kodi hajawasilisha majumuisho ya hesabu zake kwa Mwaka wote wa pato aidha ametakiwa kufanya hivyo na Mkurugenzi au Afisa mwidhiniwa anafikiri kwamba mlipa kodi huyo ana wajibu wa kulipa kodi kwa mwaka huo anaweza kwa kadri atakavyoona, kuamua kiwango cha hesabu za mlipa kodi huyo isipokuwa tathimini hiyo haitaathiri wajibu wowote wa mlipa kodi anayostahili kwa mjibu wa Sheria Ndogo hizi, kwa kushindwa kwake kuwasilisha hesabu hizo.</p> <p>(3) Kodi iliyothaminiwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi italipwa katika siku thelathini (30) tangu tarehe ya kufanya tathmini.</p> |
|   | 12. | <p>(1) Mtu yeyote anayetakiwa kulipa kodi akishindwa kuwasilisha hesabu zake kama inavyotakiwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi katika kipindi kilichoongezwa atatozwa riba ya asilimia 1.5 kwa Mwezi au shilingi Elfu Hamsini (50,000/=) kutegemea kiwango kipi kitakuwa kikubwa.</p> <p>(2) Iwapo mtu yeyote atasema uongo au ataficha baadhi ya hesabu zake kwa nia ya kupunguza kiwango cha kodi anachotakiwa kulipa, na inapobainika kuwa ufichaji au upunguzaji huo aliufanya kwa makusudi mtu huyo atatozwa ushuru pamoja na nyongeza ya kodi ya asilimia hamsini (50%) ya tofauti kati ya kodi anayotakiwa kulipa na hesabu alizowasilisha pamoja na kiwango cha kodi halisi.</p>   |
| Jumla ya riba kutozwa kwenye ushuru usiolipwa | 13. | <p>(1) Kodi ambayo haijalipwa kwa wakati kama ilivyoelezwa kwenye Sheria Ndogo hizi, itatozwa riba ya jumla ya asilimia 15% kwa Mwezi na itatakiwa kulipwa pamoja na kodi anayodaiwa.</p> <p>(2) Riba itozwayo katika Sheria Ndogo hizi itachukuliwa kama kodi inayostahili kulipwa na njia zote za kukusanya kodi na riba hiyo italipwa na mlipa kodi hiyo.</p>   |
| Makosa  | 14. | Bila kuathiri masharti ya kifungu cha 12 cha sheria hii;   |

Mtu yeyote ambaye bila ya sababu za msingi:-  
Atashindwa kuwasilisha hesabu sahihi na za kweli;

(a) Atashindwa kuwasilisha nyaraka, maelezo au taarifa inayotakiwa kuwasilisha kwa Halmashauri katika muda uliowekwa

(b) Atashindwa kutunza kumbukumbu, kitabu au hesabu

(c) Atashindwa kuonyesha kumbukumbu yoyote au nyaraka kwa ajili ya uchunguzi  
Atakuwa ametenda kosa chini ya Sheria hizi Ndogo.

Utoaji wa taarifa ya uongo

15. (1) Mtu yeyote ambaye bila ya sababu za msingi:-

(a) Akifanya hesabu za uongo kwa kupunguza au kutoa hesabu zisizokuwa sahihi

(b) Atatoa taarifa isiyokuwa sahihi kuhusu jambo lolote linaloweza kuathiri jukumu lake au la mtu mwingine la kulipa kodi.

(c) Ataandaa au kutengeneza au kusababisha kuandaliwa au kutengenezwa kwa vitabu vya uongo vya mahesabu au kumbukumbu.

(d) Atamzuia au atajaribu kumzuia Afisa mwidhiniwa kutekeleza majukumu yake aliyopewa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa.

(2) Mtu yeyote atakayekiuka Sheria Ndogo hizi atalazikima kukiri kosa hilo kwa kujaza fomu maalumu mbele ya mkurugezi kama ilivyo katika Sheria Ndogo hizi.

Adhabu

16 (1) Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa la jinai na akipatikana na hatia atalazimika kulipa faini isiyozidi Efu hamsini (50,000/=) au kifungo cha miezi sita jela

au adhabi zote mbili kwa pamoja faini na kifungo.

- (2) Pamoja na adhabu katika kifungu cha 17 (1) cha Sheria Ndogo hizi; mkosaji atawajibika kuilipa Halmashauri gharama iliyoingia kutokana na kuvunja masharti ya Sheria Ndogo hizi.

Kufifilisha kosa 17

Endapo mtu ametenda kosa na kukiri kwa maandishi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, Mkurugenzi anaweza kushughulikia kosa hilo na kuagiza kuwa mtu huyo alipe deni analodaiwa; kwa kujaza hati ya kukiri kosa, kama ilivyo katika jedwali la Sheria Ndogo hizi.

### **JEDWALI HATI YA KUKIRI KOSA**

Tarehe.....

Hati Na..... ya mwaka 20.....

Mimi.....  
.... nakiri Chini ya kifungu cha 8 cha Sheria Ndogo hizi za (Kodi ya Huduma) za Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua za Mwaka ,2014 kutenda makosa yafuatayo:-

- 1.....
- 2.....
- 3.....
- 4.....
- 5.....

Kwa hiari yangu ninakubali kuadhibiwa kwa kulipa faini ya Shilingi.....(kwa maneno:.....)  
badala ya kushitakiwa mahakamani kwa makosa haya.

Saini ya Mkosaji..... Tarehe.....

**ADHABU/FAINI HII IMETOLEWA NA:-**

Jina.....  
Cheo.....

Saini..... Tarehe.....

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua ilibandikwa katika Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe.....mwezi.....mwaka 2014 na nembo hiyo ilibandikwa mbele ya;-

.....  
**ABDALLAH S.NGODU**  
Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.

.....  
**JOHN KADUTU**  
Mwenyekiti,  
Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.

NIMEKUBALI.

.....  
**MHE.MIZENGO P.PINDA(MB)**  
WAZIRI MKUU.

Dodoma  
Tarehe.....2014.



**TANGAZO LA SERIKALI Na.....La tarehe.....**

**SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)**

**(SURA YA 287)**

**SHERIA NDOGO**

*Zimetungwa chini ya Kifungu cha 153*

**SHERIA NDOGO ZA (KILIMO KWANZA NA USALAMA WA CHAKULA)  
ZA HALMASHURI YA WILAYA YA KALIUA ZA MWAKA, 2014**

**SEHEMU YA KWANZA**

**UTANGULIZI**

Jina la sheria na Mwanzo wa kutumika	1	Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Kilimo Kwanza na Usalama wa Chakula) za Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua za Mwaka 2014, na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.
Eneo la matumizi	2	Sheria Ndogo hizi zitatumika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.
Tafsiri	3	<p>Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo:-</p> <p>“<i>Halmashauri</i>” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua</p> <p>“<i>Mkurugenzi</i>” maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua;</p> <p>“<i>Afisa mwidhiniwa</i>” maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi ni pamoja na Afisa Mtendaji wa Kata au Kijiji;</p> <p>“<i>Afisa Ugani</i>” maana yake ni mtaalam wa Kilimo, Mifugo, uvuvi, au nyuki katika ngazi za vijiji, mitaa na kata;</p> <p>“<i>Kilimo</i>” maana yake ni shughuli yoyote ya uzalishaji mali inayofanywa na binadamu na itajumuisha Kilimo cha mazao, ufugaji wa wanyama, samaki, nyuki, na uvuvi;</p> <p>“<i>Maji ya asili</i>” maana yake ni bahari, maziwa, mabwawa ya asili, mito, pamoja na mabwawa yasiyo ya asili ambayo uvuvi wa umma unafanyika;</p> <p>“<i>Mazao</i>” maana yake ni mazao yote ya chakula, biashara, maua, matunda, na mbogamboga yanayolimwa ndani ya Halmashauri;</p> <p>“<i>Mifugo</i>” maana yake ni wanyama wote wafugwao na binadamu na itajumuisha nyuki, samaki, bata, na kuku;</p> <p>“<i>Mfugaji</i>” maana yake ni mtu yeyote anayejishughulisha na ufugaji wa Mifugo katika eneo la Halmashauri;</p>

“*Mkazi*” maana yake ni raia wa Tanzania ambaye kwa kawaida anaishi kwenye mtaa au Halmashauri na ambaye ana kaya au anaishi katika kaya au taasisi iliyopo katika eneo la Halmashauri isipokuwa mtu;-

- (a) mwenye umri chini ya miaka 18
- (b) asiyejiweza kutokana na ulemavu, kuugua au uzee wa zaidi ya miaka sitini (60)
- (c) Mwanafunzi aliyeko masomoni.

“*Mkulima*” maana yake ni mtu yeyote anajishughulisha na Kilimo; “*Uvuvi haramu*” maana yake ni uvuvi unaotumia zana zisizokubalika katika uvuvi kama mabomba, baruti, sumu, makokoro, mikuki, vyandarua, na nyavu zenye matundu madogo;

“*Vyazo vya maji*” maana yake ni mito, vijito, visima, mabwawa, mifereji, maziwa, chemichemi, ardhi oevu au ardhi chechepepe;

“*Wizara*” maana yake ni wizara yenye dhamana ya masuala ya kilimo, mifugo na uvuvi na umwagiliaji.

“*Wagani kazi*” maana yake ni wakazi ambao wamepata mafunzo ya ugani nje ya vyuo ili kufanya kazi za maafisa ugani pale ambapo hawapo;

“*Zana haramu*” maana yake ni zana zisizokubalika kitaalamu kama vyandarua, baruti, mabomu, sumu, makokoro, nyavu, zenye matundu madogo, pamoja na mikuki.

#### SEHEMU YA PILI KILIMO CHA MAZAO

Wajibu wa 4  
Halmashauri  
kutekeleza  
majukumu  
ya  
usimamizi

Katika kuhamasisha na kutekeleza adhima ya Kilimo bora Halmashauri itakuwa na wajibu wa;-

- (a) Kuhakikisha viongozi wa Serikali, Vyama vya Siasa na wadau wengine wanashiriki ipasavyo katika kuendeleza sekta ya Kilimo katika Halmashauri
- (b) Kuhakikisha kuwa wakulima wanasajiliwa pamoja na mazao wanayolima na kiasi cha hekari ya mazao wanayolima;
- (c) Kuhakikisha upatikanaji rahisi na kwa wakati wa pembejeo za Kilimo;
- (d) Kuakikisha upatikanaji wa maafisa ugani katika kila Kata
- (e) Kuanzisha mfuko wa stakabadhi ghalani
- (f) Kuainisha matumizi bora ya ardhi ili kuhakikisha na kutofautisha ardhi ya Mifugo, Kilimo na hifadhi;
- (g) Kusimamia upatikanaji wa mbolea na pembejeo za Kilimo, na kufanya ukaguzi wa mbegu zinazoingizwa ndani ya Halmashauri.
- (h) Kuakikisha visumbufu na magojwa ya mazao yanadhibitiwa;
- (i) Kuakikisha kuwa wanunuzi wa mazao wanakuwa na vibali vya kununua mazao;

- (j) Kuhakikisha kunakuwa na masoko rasmi yanayotambulika.
  - (k) Kuweka mabango kwenye kila Kijiji yanayoeleza kanuni bora za Kilimo yanayopaswa kuzingatiwa na mkulima kwa mazaoyayolimwa kwenye eneo hilo;
  - (l) Kuanzisha mashamba darasa ya mfano katika kili Kijiji;
  - (m) Kuhamasisha uanzishwaji wa vyama vya wakulima vya kuweka na kukopa kwa lengo la kujipatia mikopo ya benki;
  - (n) Kuhakikisha kila mkulima wanalima angalau kuanzia ekari sita (6), ekari 1 mazao ya mizizi, ekari 2 mazao ya biashara, ekari 3 mazao ya chakula.
  - (o) Kuhakikisha mkulima anazingatia vipimo katika uuzaji wa mazao
  - (p) Kuhakikisha matumizi sahihi ya viatilifu ili kulinda mazingira
  - (q) Kuhakikisha wakulima wanaotumia maji kwa ajili ya kilimo, wanazingatia sheria za raslimali maji kupunguza migogoro.
- Wajibu wa 5 Serikali ya Kijiji itakuwa na wajibu ufuatao;-
- (a) Kusajili wakulima na mazao wanayolima
  - (b) Kuakikisha kuwa sheria za mazao na kanuni zake zinatekelezwa;
  - (c) Kuhakikisha mkulima anamuuzia mazao mnunuzi mwenye kibali cha Halmashauri na leseni ya kununua mazao na kwa kuzingatia vipimo stahili
  - (d) Kuhakikisha kuwa kila mkazi katika eneo la Kijiji anayemiliki ardhi ya Kilimo chini ya sheria yoyote ile, analima mazao ya chakula na biashara.
- Wajibu wa 6 (1) Afisa mwidhiniwa atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kwamba kila mkulima;-
- (a) Anaandaa shamba kwa wakati;
  - (b) Anapanda mbegu bora kwa nafasi zinazoshauriwa
  - (c) Anaweka mbolea kwa viwango na kwa wakati;
  - (d) Anapalilia kwa wakati palizi mbili au zaidi.
  - (e) Anathibiti wadudu na magonjwa
- (2) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuingia na kukagua shamba lolote wakati wa saa za kazi ili kujionea kama mkulima amezingatia maelezo ya kitaalam kama yalivyotolewa na wataalam wa Kilimo.
- Jukumu la 7 (1) Itakuwa ni jukumu la kila mkazi hususani Mkuu wa kaya kuhakikisha kuwa anahifadhi chakula cha kutosha yeye na familia yake kwa angalau mwaka mmoja au zaidi;

- (2) Litakuwa ni jukumu la kila kaya kuwa na ghala la kuhifadhia chakula ambalo litapaswa kuwa katika hali ya usalama na lisilo ruhusu wadudu kama vile dumuzi, panya, au wadudu wengine kusababisha uharibifu wa chakula hicho.
- Wajibu wa Afisa Ugani 8 Kila Afisa Ugani atakuwa na wajibu wa kutoa program ya Kilimo ya mwaka kulingana na hali ya hewa;-
- (a) Programu hiyo itazingatia aina ya mazao kwa msimu;
  - (b) Aina ya mbegu kwa msimu husika;
  - (c) Namna na wakati wa kupanda;
  - (d) Namna na wakati gani wa kuvuna;
  - (e) Namna ya kuhifadhi mazo baada ya kuvuna.
  - (f) Kutoa mafunzo kwa wakulima juu ya teknolojia mpya
- Uwezo wa Maafisa 9 Afisa Mwidhiniwa akishirikiana na Afisa Ugani:-
- (a) Ataweza kuingia katika kaya yoyote wakati wa kazi ili kukagua ghala la chakula kuona kama taratibu za kuhifadhi chakula zinazingatiwa;
  - (b) Ataweza wakati wa saa za kazi kuingia kwenye eneo la Kilimo kwa madhumuni ya kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;
  - (c) Kumchukulia hatua za kisheria mtu yeyote atakayevunja Sheria Ndogo hizi;
  - (d) Atatakiwa kuwa na daftari linaloonyesha idadi kamili ya wakazi na idadi ya ekari za mazao ya Kilimo
  - (e) Atapanga ratiba ya kutembelea mashamba ya wakazi ili kujionea kama wanatekeleza wajibu wa kulima na kutunza mashamba kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.
- Utunzaji wa mashamba 10 Kila Afisa Mtendaji wa Kijiji au kata atawajibika kutunza kumbukumbu za mashamba yote ya mazao yaliyomo katika Kijiji au kata yake na atasimamia moja kwa moja utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi katika Kijiji au kata yake.

## SEHEMU YA TATU

### UFUGAJI WA KISASA

- Wajibu wa Halmashauri 11 Ili kuendeleza ufugaji bora na wa kisasa Halmashauri zitakuwa na wajibu ufuatao;-
- (a) Kuundaa mpango wa matumizi bora ya ardhi ili kutenga maeneo ya wakulima, wafugaji na maeneo ya hifadhi;
  - (b) Kuhakikisha upatikanaji wa maafisa ugani
  - (c) Kuhakikisha upatikanaji wa madawa ya Mifugo na chanjo za Mifugo;
  - (d) Kuhakikisha uwepo wa majosho katika kila Kijiji kwa

kushirikisha nguvu za wananchi; kuhakikisha upatikanaji wa masoko ya Mifugo hai na nyama;

- (e) Kuhamasisha wananchi kuanzisha vyama vya ushirika wa wafugaji na vyama vya kuweka na kukopa;
- (f) Kuundaa vigezo vya kuwapata maafisa ugani bora wa Mifugo katika vijiji, mtaa, na kata;
- (g) Kutoa zawadi za Kijiji, mtaa, na kata bora katika ufugaji kwa mwaka;
- (h) Kutoa zawadi kwa shamba darasa la Mifugo kwa mwaka;
- (i) Kuakikisha upatikanaji wa mabwawa/malambo ya maji ya kunyweshea Mifugo;
- (j) Kuhakikisha uhibitaji wa ufugaji wa kuhamahama ili kuhifadhi mazingira
- (k) Kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi ili kudumisha amani, utulivu na maelewano katika jamii za wakulima na wafugaji.

Wajibu wa 12  
Serikali ya  
Kijiji

Uongozi wa Serikali ya Kijiji utahakikisha;-

- (a) Unaandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi;
- (b) Unasimamia na kulinda mipaka ya ardhi ya Kilimo na Mifugo iliyobainishwa na mpango wa matumizi bora ya ardhi;
- (c) Unatoa au kutaja idadi ya Mifugo ambayo kila mfugaji ataruhusiwa kuwa nayo kwa mjibu wa sheria;
- (d) Unasimamia uanzishwaji wa majosho ya Mifugo kwa kushirikiana na wafugaji
- (e) Unahamasisha wafugaji kuvuna Mifugo yao mara kwa mara ili kubakisha idadi ya Mifugo yenye kuleta tija;
- (f) Kuhakikisha wataalamu wa ugani waliopo katika Kijiji wanatoa elimu ya ufugaji wa kisasa ili kupata Mifugo bora na mazao bora ya Mifugo;
- (g) Kuandaa njia maalum za kupitisha Mifugo (stock routes)

Wajibu wa 13  
Afisa  
Mwidhiniwa

Afisa Mwidhiniwa akishirikiana na Afisa Ugani:-

- (a) Kuwa na daftari linaloonyesha idadi kamili ya Mifugo kwa kila mfugaji;
- (b) Kuingia katika kaya yoyote ili kukagua idadi ya Mifugo
- (c) Kuhakikisha kuwa mfugaji anachanja na kuogesha Mifugo yake mara kwa mara ili kuthibiti magojwa ya Mifugo;
- (d) Kuhakikisha kuwa mfugaji mwenye Mifugo iliyozidi idadi ya kibali chake kwa mujibu wa sheria anavuna Mifugo yake kwa njia endelevu;
- (e) Kutoa taarifa kwa Halmashauri mara anapogundua kuna mlipuko wa magojwa ambayo yatahitaji msaada kutoka ngazi za juu;
- (f) Kumchukulia hatua za kisheria mfugaji yeyote

anayekwenda kinyume na masharti ya ufugaji yaliyoainishwa chini ya Sheria Ndogo hizi au sheria yoyote Nchi.

- Wajibu wa mfugaji 14 Kila mfugaji atahakikisha;-
- (a) Anafuga idadi ya wanyama ambayo haitasababisha usumbufu kwa wadau wengine wa Kilimo kama ilivyoainishwa kwenye kibali cha Halmashauri;
  - (b) Kuchanja Mifugo yake mara kwa mara ili kuzuia magonjwa ya Mifugo na magonjwa ya mlipuko;
  - (c) Kuogesha Mifugo yake ili kujihami dhidi ya magonjwa, kupe na mbung'o;
  - (d) Kufuga Mifugo yake katika maeneo yaliyotengwa katika mpango wa matumizi bora ya ardhi;
  - (e) Kuheshimu mipaka iliyotenganisha ardhi ya Kilimo, Mifugo, hifadhi za taifa, makazi, maeneo ya taasisi na maeneo mengine ya wadau wa Kilimo kama mazao ya wakulima, wafugaji wa nyuki, samaki na skimu za umwagiliaji;
  - (f) Atashirikiana na maafisa au maafisa ugani wakati wa tiba au chanjo wakati wa magonjwa ya mlipuko na karantini na kampeni zozote za kitaifa za kudhibiti magonjwa na vifo vya Mifugo;
  - (g) Atashirikiana na maafisa ugani kuanzisha shamba darasa na mashamba ya kulishia Mifugo;
  - (h) Anapitisha Mifugo yake katika njia zilizitengwa na Halmashauri (stock routes)
  - (i) Anaweka alama za utambuzi wa Mifugo yake katika sehemu za wanyama kama itakavyoelekezwa na watalam (branding, earing tag, tattooing) ili kutoharibu ubora na thamani ya ngozi.
- Uvunaji wa mifugo 15 (1) kila mfugaji atawajibika kuvuna Mifugo yake kila atakapobaini kuwa imevuka idadi iliyoko kwenye kibali kilichotolewa na Halmashauri;
- (2) Kabla ya kuvuna mfugaji atashirikiana na Afisa Mwidhiniwa ili kujiridhisha kwamba Mifugo yake haina maradhi au magonjwa ya kuambukiza.
- Makosa 16 Mfugaji yeyote atakuwa ametenda kosa iwapo;-
- (a) Atashindwa kuvuna Mifugo iliyozidi idadi iliyoko kwenye kibali kilichotolewa na Halmashauri;
  - (b) Atashindwa au kukataa kuchanja Mifugo yake ili kuzuia magonjwa;
  - (c) Atalisha mifugo yake kwenye maeneo ambayo

hayakutengwa kwa ajili hiyo

- (d) Ataruhusu Mifugo yake kuzurura ovyo;
- (e) Atazembea au kushindwa kutoa taarifa juu ya ugonjwa wa Mifugo;
- (f) Atamzuia Afisa mwidhiniwa au afisa ugani kutekeleza majukumu yake;
- (g) Atasafirisha Mifugo yake bila kibali cha Halmashauri.

SEHEMU YA NNE  
SKIMU ZA UMWAGILIAJI

- Wajibu wa Halmashauri 17
- (1) Halmashauri kwa kushirikiana na vijiji itaanzisha skimu za umwagiliaji katika maeneo ya vijiji ambavyo upatikanaji wa vyanzo vya maji sio wa shida ili kuchochea Kilimo cha umwagiliaji;-
  - (2) Ili kuendeleza skimu za umwagiliaji Halmashauri itakuwa na wajibu ufuatao:-
    - (a) Kutoa utalam wa ugani na matumizi bora ya skimu ili kuzifanya ziwe endelevu
    - (b) Kushirikiana na vijiji katika kuibua, kuendeleza na Kufanya ukarabati wa miundo mbinu katika skimu isipokuwa kwa uharibifu wa makusudi au uzembe utakaosababishwa na matumizi mabaya ya skimu;
    - (c) Kuanzisha skimu za umma na kuzigawa kwa wananchi watakaomba na kuahidi kutunza skimu hizo ili ziwe endelevu;
    - (d) Kutoa, kufuta, kubatilisha, au kusimamisha kibali cha utumiaji wa skimu afisa mwidhiniwa au Afisa ugani atakuwa na uwezo wa kuingia kwenye skimu wakati wa saa za kazi ili kufanya ukaguzi;
  - (3) Kibali kitolewacho na Halmashauri kwa ajili ya kueleza skimu kitalipiwa ada ya shilingi hamsni elfu kwa mwaka (50,000/=) kabla ya kupewa leseni mwombaji atalazimika kulipa ada ya utunzaji skimu itakayopangwa na Halmashauri au umoja wa wakulima, ada hiyo italipwa kila mwaka na mwombaji ataruhusiwa kulipa kwa awamu mbili kwa mwaka.
- Wajibu wa watumiaji skimu za umwagiliaji 18
- Watumiaji wa skimu za umwagiliaji watakuwa na majukumu yafuatayo:-
    - (a) Kutunza, kulinda, kuhifadhi na kuheshimu miundombinu iliyoko katika skimu za umwagiliaji;
    - (b) Kutoa taarifa za uharibifu wa miundo mbinu ya skimu kila inapotekea;
    - (c) Kulipia leseni na ada za skimu kila mwaka;
    - (d) Kufanya ukarabati wa skimu inapohitajika na kwa uharibifu

ambao umesababishwa na uzembe au matumizi mabaya ya miundombinu ya skimu;

- (e) Kuwapa ushirikiano maafisa wa Halmashauri wakati wowote wanapotaka kuingia au kukagua miundombinu ya skimu;
- (f) Kubuni vyanzo vya mapato na kuweka taratibu za namna ya kukusanya ili kuwa na hazina ambayo itatumika kama italazimika kufanya hivyo ili kuboresha au kuimarisha miundombinu ya skimu za umwagiliaji;
- (g) Kulinda na kuhifadhi vyanzo vya maji ambavyo vinaingiza maji katika skimu za umwagiliaji.

- Makosa na adhabu 19 (1) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa iwapo;-
- (a) Ataharibu miundo mbinu iliyopo kwenye skimu za umwagiliaji;
  - (b) Atashindwa kukarabati miundombinu ya skimu kwa uzembe au matumizi yake mabaya ya miundo mbinu hiyo;
  - (c) Atashindwa au kukataa kulipa leseni na ada ya skimu;
  - (d) Atachepusha maji kutoka vyanzo vya maji bila kibali cha Halmashauri;
- (2) Endapo kosa alilotenda mtu huyo lilisababisha hasara au uharibifu wa mali ya Kijiji au Halmashauri au serikali au skimu ya umwagiliaji au mali ya mtu binafsi, ataamriwa kufanya matengenezo au kulipa fidia ya matengenezo na iwapo atashindwa atashitakiwa na akipatikana na kosa atahukumiwa kwenda kifungo cha miezi kumi na miwili jela.

## SEHEMU YA TANO

### UFUGAJI WA SAMAKI NA UVUVI

#### A: UFUGAJI WA SAMAKI

Ufugaji 20 Halmashauri kulingana na jiografia yake, sayansi yake ya udongo, upatikanaji wa maji, na mvua itakuwa na wajibu wa kuhamasisha serikali za vijiji na wananchi kwa ujumla kuanzisha ufugaji wa samaki wa kisasa katika eneo lake.

Jukumu la Halmashauri 21 Ili kutekeleza mahitaji ya kifungu cha 21 cha Sheria Ndogo hizi itakuwa ni jukumu la Halmashauri kuhakikisha kwamba;-

- (a) Inahamasisha wananchi juu ya uanzishaji wa Kilimo cha ufugaji wa samaki;
- (b) Inaanzisha mabwawa ya mfano ya samaki katika kila kata;
- (c) Inawezesha upatikanaji wa maafisa ugani wa uvuvi kwenye



kata na vijiji

- (d) Vifaranga vya samaki vinapatikana ili kupandikiza katika mabwawa ya wananchi, kata, vijiji na vitongoji;

Jukumu la Afisa uvuvi 22

Kwa mjibu wa Sheria Ndogo hizi kila Afisa Uvuvi wa kata au Kijiji atakuwa najukumu la;-

- (a) Kuanzisha rejesta ya orodha ya wafugaji wote wa samaki katika kata au Kijiji;
- (b) Kupanga ratiba ya kuwatembelea wafugaji wa samaki katika kata au Kijiji;
- (c) Kuanzisha orodha na idadi ya mabwawa ya samaki na aina ya samaki katika kila bwawa katika kata au Kijiji;
- (d) Kuanzisha mashamba darasa au mabwawa ya mfano kwa ajili ya kutolea mafunzo ya nadharia na vitendo;
- (e) Kuhakikisha upatikanaji wa vifaranga na mbegu bora ya samaki
- (f) Kuandaa programu ya uendelezaji na ukuzaji wa Kilimo cha ufugaji wa samaki katika kata au Kijiji;
- (g) Kuakikisha wafugaji wa samaki wanatumia nyavu sahihi wakati wa kuvuna katika mabwawa yao ili kutoharibu mazalia na kutovuna samaki wadogo;
- (h) Kumchukulia hatua za kisheria mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya uvuvi yaliyoainishwa chini ya Sheria Ndogo hizi au sheria yoyote andishi ya uvuvi au hifadhi ya mazingira.

#### B; UVUVI KATIKA MAJI YA ASILI

Uvuvi katika maji ya asili 23

Wananchi watakuwa na ruhusa ya kuvua katika maji ya asili kama, mito, maziwa, mabwawa ya asili yasiyo ya asili kwa vibari maalum vya uvuvi.

Jukumu la halmashauri 24

Halmashauri itakuwa na wajibu wa kuhakikisha kwamba;-

- (a) Wavuvi wote watakuwa na vibali na leseni halali ya uvuvi;
- (b) Wavuvi watatumia nyavu zinazokubaliwa kitaalam
- (c) inapiga marufuku uvuvi haramu wa kutumia makokoro, sumu, mabomu, baruti, mikuki, nyavu zisizokubalika, nyandarua na zana zingine ambazo hazikubaliki kitaalam;
- (d) Inatoa Elimu ya uvuvi wa kisasa na zana za uvuvi zinazokubalika kisheria;
- (e) Inaanzisha vikosi vya ulinzi vya kupambana na wavuvi haramu kupitia ulinzi shilikishi katika mabwawa na maji ya asili;
- (f) Inateketeza zana haramu za uvuvi zinazotengenezwa na wavuvi haramu;
- (g) Vijiji vyote vinvyopakana au kuzungukwa na maji ya asili

vinapatiwa maafisa uvuvi;

- (h) Inatengeneza na kuanzisha makambi ya wavuvi ili kuzuia uvuvi holela na uvuvi haramu;
- (i) Inafanya ukagizi wa leseni za uvuvi mara kwa mara na kuwachukilia hatua za kisheria wavuvi wasio na leseni;
- (j) Itaanzisha na kutengeneza rejesta ya orodha ya wavuvi wote wenye leseni katika Halmashauri;
- (k) Inahamasisha wavuvi kuanzisha vyama vya kuweka na kupopa ili kuweza kujipatia mikopo katika mabanki kwa ajili ya kukuza mitaji na kujipatia zana bora na za kisasa za uvuvi.
- (l) Kusitisha, kufuta au kumnyang'anya mtu yeyote leseni endapo atabainika amekiuka masharti ya leseni ya uvuvi;

Wajibu wa Afisa uvuvi 25

Kila Afisa Uvuvi wa Halmashauri kwa kushirikiana na Afisa Mtendaji wa kata, Kijiji, au mtaa ambazo zinapakana au kuzungukwa na maji watakuwa na wajibu wa:-

- (a) Kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;
- (b) Kuuunda vikosi vya doria dhidi ya wavuvi haramu
- (c) Kufanya ukaguzi wa leseni mara kwa mara katika sehemu za wavuvi;
- (d) Kutoa Elimu juu ya uvuvi salama, uvuvi endelevu na hifadhi ya madhingira katika maeneo ya uvuvi;
- (e) Kuanzisha na kutunza rejesta yenye orodha ya wavuvi katika kata, vijiji na mitaa;
- (f) Kuanzisha rejesta ya majina ya wavuvi.

Makosa 26

Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo:-

- (a) Atavua samaki kwa kutumia zana ambazo hazikubaliki kitaalam;
- (b) Atavua bila kuwa na leseni halali;
- (c) Atakaa au kukwepa kulipa ushuru wa Halmashauri;
- (d) Ataendesha shughuli za uvuvi bila kujiandikisha kwenye rejesta ya wavuvi ya kata, kijiji au mtaa;
- (e) Atavua katika maeneo ya hifadhi au eneo lolote lisiloruhusiwa kisheria;
- (f) Atapatikana akivua au akiuza samaki wadogo wadogo.

#### SEHEMU YA SITA UFUGAJI WA NYUKI

Jukumu la Halmashauri 27

Ili kukuza na kuendeleza ufugaji bora na wa kisasa wa nyuki Halmashauri itakuwa na wajibu ufuatao:-

- (a) Kuhakikisha kunakuwepo mtaalamu wa nyuki katika kila kata au Kijiji;
- (b) Kutoa Elimu ya ufugaji wa nyuki;

- (c) Kuwatafutia wafugaji soko la uhakika la asali;
- (d) Kuhamasisha ufugaji wa nyuki katika kila kata, na vijiji;
- (e) Kutoa Elimu ya utunzaji na uhifadhi wa mazingira;
- (f) Kurahisisha upatikanaji wa mti miche bora ya miti ya asili au ya kisasa itakayotoa maua mengi ambayo nyuki watatumia kutengeneza asali
- (g) Inasambaza bure miche ya miti kwa wafugaji wa nyuki na kwa bei nafuu kwa wakilima wasiofuga nyuki;
- (h) Kuhakikisha upatikanaji wa dawa baridi za kurinia asali ambazo haziui nyuki wala kuharibu mazalia au masenga yake;
- (i) Kutengeneza mizinga bora ya mfano kwa ajili ya ufugaji wa nyuki na kufundishia;
- (j) Kuwasaidia wafugaji walioko katika vikundi kuanzisha vituo vya kukusanyia na kuuzia asali;
- (k) Kuanzisha mashamba darasa ya ufugaji wa nyuki na hifadhi ya mazingira;
- (l) Kufanya tathmini ya kila mwaka ya ukuajiwa sekta ya ufugaji wa nyuki;
- (m) Kutenga maeneo maalum ya ardhi kwa ajili ya wafugaji wa nyuki;
- (n) Kuhakikisha upatikanajiwa pembejeo za ufugaji wa nyuki;

- Maafisa nyuki na wajibu wao 28
- (1) Kila kata na Kijiji kitakuwa na Afisa nyuki;
  - (2) Wajibu wa Afisa Nyuki wa kata au Kijiji atakuwa na wajibu wa;-
    - (a) Atakuwa ndiye Afisa mwidhiniwa wa masuala ya nyuki katika kata au Kijiji husika;
    - (b) Atatunza orodha ya wafugaji wote wa nyuki katika kata au Kijiji husika;
    - (c) Atatunza orodha ya vikundi vyote vya wafugaji wa nyuki katika kata au Kijiji husika;
    - (d) Atatoa mafunzo elekevu ya ufugaji bora wa nyuki katika kata au kijiji;
    - (e) Ataanzisha mashamba darasa ya ufugaji wa nyuki katika kata au Kijiji
    - (f) Ataandaa ratiba za kuwatembelea wafugaji wa nyuki waliomo katika kata au Kijiji husika;
    - (g) Kwa kushirikiana na Afisa Mtendaji wa kata au Kijiji watachukua hatua za kisheria dhidi ya wafugaji wa nyuki au mtu yeyote atayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi au sheria yoyote ya ufugaji wa nyuki au hifadhi ya mazingira.

- Wajibu wa mfugaji 29
- Kila mfugaji wa nyuki atakuwa na wajibu ufuatao;-
    - (a) Atatimiza mazingira ya kisasa ya ufugaji wa nyuki;

- (b) Atarina asali kwa kutumia njia za kisasa badala ya kutumia moshi au moto atahifadhi mazingira kwa kutochoma moto, misitu
- (c) Atatumia dawa isiyoua nyuki wala kuharibu ubora wa asali wakati wa urinaji;
- (d) Atatumia vyombo au vifaa vilivyo safi na salama kwa ajili ya kurinia na kuhifadhi asali;
- (e) Atahudhulia mafunzo yatolewayo katika mashamba darasa ya ufugaji wa nyuki;

30

Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo;-

- (a) Akirina asali kwa kutumia moto au moshi;
- (b) Akiuza asali iliyorinwa kwa kutumia moto au moshi
- (c) Akichanganya au amechanganya asali na vitu vingine ambavyo sio asali
- (d) Akichoma moto msitu au eneo ambalo limetengwa kwa ajili ya wafugaji wa nyuki;
- (e) Akikata mti au miti bila kuwa na kibali kutoka Halmashauri;
- (f) Aking'oa miti iliyopandwa kwa ajili ya kuhifadhi mazingira;
- (g) Akihujumu miundombinu ya ufugaji wa nyuki;
- (h) Akitenda jambo lolote ambalo linadhuru au linahatarisha maendeleo na ukugaji wa Kilimo cha nyuki;

Adhabu

31

Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi laki tatu (300,000/=) au kifungo cha miezi kumi na miwili jela au adhabi zote mbili kwa pamoja faini na kifungo.

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua ilibandikwa katika Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe.....mwezi.....mwaka 2014 na nembo hiyo ilibandikwa mbele ya;-

.....  
**ABDALLAH S.NGODU**  
Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.

.....  
**JOHN KADUTU**  
Mwenyekiti,  
Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.

NIMEKUBALI.

.....  
**MHE.MIZENGO P.PINDA(MB)**  
WAZIRI MKUU.

Dodoma  
Tarehe.....2014.

TANGAZO LA SERIKALI Na..... La tarehe.....

**SHERIA ZA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA YA WILAYA)**

**(SURA 287)**

-----  
**SHERIA NDOGO**  
-----

*Zimetungwa chini ya kifungu cha 153)*

**SHERIA NDOGO ZA (UANZISHAJI WA MFUKO WA AFYA YA JAMII) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KALIUA ZA MWAKA 2014.**

**Jina na mwanzo wa kutumika**

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Uanzishaji wa Mfuko wa afya ya jamii) za Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

**Matumizi**

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya wilaya ya Kaliua

**Tafsiri**

Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapohitajika vinginevyo:-

“*Bodi*” maana yake ni Bodi ya Huduma za Afya ya halmashauri iliyoundwa chini ya ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura ya 287;

“*Halmashauri*” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.

“*Huduma za Afya*” maana yake ni huduma zote za Afya zinazotolewa na Hospitali za Serikali na watu binafsi, na zinajumuisha huduma nyingine za Afya zilizoanzishwa kwa madhumuni ya kutoa huduma za Afya ikiwa ni pamoja na vituo vya Afya na Zahanati.

“*Kadi*” maana yake ni kadi itakayotolewa na Bodi kwa mwanachama wa Mfuko wa Afya ya Jamii.

“*Kaya*” maana yake ni Mama, Baba na Watoto wenye umri chini ya miaka kumi na nane; au zaidi na awe na mtoto au bila mtoto mwenye umri chini ya miaka kumi na nane; au asasi yoyote.

“*Kituo cha huduma kilichoteuliwa*” maana yake ni kituo kinachotoa

huduma za afya na ni pamoja na kituo chochote kilichoanzishwa au kinachoendesha kwa malengo ya kutoa huduma za afya kiwe kinamilikiwa na Halmashauri, Serikali, asasi ya kidini, mtu au watu binafsi ambacho kinahusika na mfuko wa Afya ya Jamii.

“*Mchango*” maana yake ni mchango wa hiari utakaotolewa na Wanachama wa Mfuko wa Afya ya Jamii.

“*Mganga Mkuu wa Wilaya*” maana yake ni daktari ambaye ni Msimamizi mkuu wa shughuli za huduma za Afya katika Halmashauri ya Wilaya Kaliua.

“*Mwanachama*” maana yake ni kaya inayochangia kwenye Mfuko wa Afya ya jamii;

“*Malipo ya huduma*” maana yake ni malipo yanayotozwa na kituo cha tiba, kilichoteuliwa kwa watu ambao sio wanachama, wanapopatiwa huduma za afya katika kituo hicho.

“*Mfuko au mfuko wa Afya ya jamii*” maana yake ni mfuko wa afya ya Jamii ulioanzishwa chini ya Sheria Ndogo hizi.

“*Wizara*” maana yake ni Wizara yenye dhamana au masuala ya afya.

**Mfuko wa Afya ya Jamii**

4. – (1) Kutakuwa na mfuko wa Afya ya jamii ambao ni mpango wa hiari wenye lengo la kutoa huduma za afya, ambapo kaya zitakuwa zikilipia huduma hizo na Serikali itatoa mchango wake wa fedha kama jazilio kwa mchango kutoka kwenye kaya.

(2) Matumizi ya Fedha yatafanywa na kusimamiwa na Bodi kwa mujibu wa sheria Ndogo hizi.

**Madhumuni ya Mfuko**

5. Madhumjuni ya Mfuko yatakuwa ni:

(a) Kutafuta vyanzo vya fedha kutoka katika jamii kwa ajili ya kutoa huduma bora za Afya kwa wanachama.

(b) Kutoa huduma bora za Afya zinazopatikana kwa kutumia mipango endelevu na;

(c) Kuboresha huduma za afya katika jamii kwa kugawanya madaraka na kuzipa nguvu jamii katika kufnya maamuzi na kuchangia katika masuala yanayohusu Afya zao.

**Kazi za Bodi**

6. – (1) Ili kufanikisha malengo yake makuu. Bodi itakuwa na kazi zifuatazo:-

(a) itasimamia masuala na shughuli zote zinazohusu Mfuko wa

Afya ya jamii;

- (b) itafanya kazi kwa kushauriana na timu ya uendeshaji ya huduma za afya ya Halmashauri na kuhakikisha kuwa huduma ya afya inayotolewa ni bora na ya kitaalamu.
  - (c) Kukusanya na kusimamia mapato ya mfuko wa afya ya Jamii;
  - (d) Kupendekeza kwa Halmashauri watu wanaosatahili kusamehewa kutoa mchango kwenye Mfuko;
  - (e) Kuweka malengo ya mfuko;
  - (f) Kupitia ripoti na taarifa kutoka Kamati ya afya ya Kata au chanzo kingine chaochote;
  - (g) Kuratibu makusanyo, matumizi na kudhibiti mapato na;
  - (h) Kupanga mipango ya afya ya mwaka kwa ajili ya kuthibitishwa na Halmashauri;
  - (i) Kupanua na kuongeza utoaji wa huduma za afya kwa wanachama kulingana na mapato ya mfuko.
- (2) Bodi katika kutekeleza majukumu yake, itapokea na kutekeleza maagizo ya halmashaurik kwa mujibu wa Sheria, kanuni na taratibu.

**Vyanzo ya Mapato**

7. Vyanzo vya mapato ya Mfuko vitatokana na:-

- (a) Fedha zote zitakazopokelewa kutokana na michango ya wanachama;
- (b) Ruzuku kutoka kwenye Halmashauri, Serikali kuu, na wahisani mbalimbali toka ndani na nje ya Halmashauri;
- (c) Michango ya watu binafsi wanaoishi ndani na nje ya Halmashauri;
- (d) Malipo ya fedha ya wasiokuwa wanachama wa mfuko kwa kupata huduma ya afya;



- (e) Ushuru utakaotzwa na Halmashauri kutoka vyanzo mbalimbali na kutengwa kwa ajili ya Mfuko; na
- (f) Fedha zozote halali ambazo mfuko unaweza kupata toka mahali pengine popote.

**Akaunti ya mfuko wa Bodi na watiaji saini**

8. – (1) Kutakuwepo na Akaunti maalum inayotumika na Halmashauri ambayo fedha zote zitakazokusanywa kwa ajili ya Mfuko zitahifadhiwa na kutolewa.
- (2) Watia saini wa Akaunti ya Mfuko wanachaguliwa na Bodi na watakuwa ni mmoja kutoka kundi “A” na “B” na kwa namna yoyote hakuna pesa zitakazotolewa kwenye Akaunti ya mfuko bila saini ya mmojawapo kutoka kundi “A” na “B”
- (3) Watia saini kwenye hundi za Mfuko watakuwa kama ifuatavyo:-
- (a) Mwenyekiti wa Bodi na Mjumbe mmoja wa Bodi ambao watakuwa kundi “A”
  - (b) Katibu wa Bodi na Mweka Hazina wa halmashauri watakuwa Kundi “B”
- (4) Kila baada ya miezi mitatu, Bodi itakuwa inatoa taarifa ya akaunti ya Mfuko kwa halmashauri.
- (5) Akaunti ya Mfuko itakaguliwa na wakaguzi waliochaguliwa kwa mujibu wa Kanuni za Fedha za Serikali za Mitaa.

**Taarifa ya fedha**

9. Mwezi mmoja baada ya mwaka wa fedha wa Halmashauri Bodi itatakiwa kuandaa taarifa ya mapato na matumizi ya fedha na kuwasilisha kwa Halmashauri.

**Mipango na Matumizi**

10. – (1) Miezi miwili kabla ya kuanza kwa mwaka wa fedha wa Halmashauri. Bodi itaandaa mipango na bajeti ya mwaka kwa kuonyesha kiwango kinachotarajiwa kupatikana na mgawanyo wa fedha kwa ajili ya utoaji huduma za Afya na maendeleo katika maeneo ya halmashauri.
- (2) Bodi inaweza kuandaa bajeti ya nyongeza kama kutakuwa nahaja ya kufanya hivyo na mazingira yataruhusu.
- (3) Mipango ya bajeti ya mfuko itaandaliwa kulingana na utaratibu kama ilivyoainishwa katika vifungu vidogo vya (1) na (2) hapoo juu, ambayo ni lazima uwasilishwe kwa Halmashauri kwa ajili ya kuidhinishwa.

**Muundo wa  
wajumbe wa  
Bodi**

11. Bodi itakuwa na wajumbe wafuatao:-

- (a) wawakilishi wanne wa watumiaji huduma za afya kati yao wawili ni lazima wawe ni wanawake;
- (b) mwakilishi mmoja kutoka watoa huduma za afya binafsi bila faida na;
- (c) mwakilishi mmoja kutoka watoa huduma za afya kwa faida waliochaguliwa na Halmashauri kutoka vituo vya kutolea huduma za afya binafsi kwa faida waliochaguliwa miongozi mwao;
- (d) mwenyekiti wa Kamati ya Elimu, Afya na Masuala ya Uchumi;
- (e) afisa mipango wa Halmashauri;
- (f) mganga mkuu wa Halmashauri ambaye atakuwa katibu wa bodi;
- (g) mwakilishi mmoja kutoka Hospitali na mwakilishi mmoja kutoka Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Mkoa.

**Sifa za  
wajumbe wa  
Bodi**

12. Mjumbe wa Bodi atakuwa na sifa zifuatazo:-

- (a) awe raia wa Tanzania;
- (b) awe na umri si chini ya miaka ishirini na tano na si zaidi ya miaka sabini;
- (c) awe amehitimu elimu ya Sekondari na kuendelea;
- (d) awe na uzoefu na amewahi kuonyesha uwezo wake wa kuongoza katika shughuli za huduma za jamii;
- (e) awe na sifa za uongozi; na
- (f) asiwe na wadhifa wowote wa kisiasa kupitia chama chochote cha siasa.

**Muda wa  
kukaa  
madarakani**

13. – (1) Mjumbe wa Bodi atakuwa madarakani kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia tarehe aliyochaguliwa na anaweza kuchaguuliwa tena kwa kipindi cha miaka mitatu tu.

- (2) Endapo nafasi yoyote ya mjumbe wa Bodi itaachwa wazi kwa sababu ya kifo, kujiuzulu, kukiuka maadili ya kazi au ulemavu utakaomfanya ashindwe kushiriki kikamilifu kama mjumbe au kwa sababu nyingine yoyote ile, mjumbe mwingine atachaguliwa kujaza nafasi hiyo iliyoachwa wazi.

- (3) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (2) haitaruhusiwa kuchagua mjumbe mwingine iwapo kipindi kilichobaki ni chini ya miezi sita.

**Usimamizi  
wa Mfuko**

14. Usimamizi na uendeshaji wa mfuko utakuwa chini ya:-

- (a) Halmashauri ya Wilaya kupitia Bodi ya huduma za afya ya halmashauri katika ngazi ya Halmashauri;
- (b) Kamati ya maendeleo ya Kata kupitia Kamati ya afya ya Kata, katika ngazi ya Kata; na
- (c) Serikali ya Mtaa kupitia Kamati ya Huduma za jamii katika ngazi ya Mtaa.

**Kamati ya  
Afya ya Kata**

15. Kutakuwa na Kamati ya Afya ya kata.

**Wajumbe wa  
kamati ya  
Afya ya Kata**

16. – (1) Kamati ya Afya ya kata itakuwa na wajumbe wafutao:-

- (a) Diwani anayewakilisha Kata husika;
  - (b) Afisa mtendaji wa kata;
  - (c) Mwalimu Mkuu mmoja kutoka kwenye shule ya msingi ambayo ipo kwenye kata husika.
  - (d) Wajumbe wawili wanawakilisha jamii husika ambapo mmoja wao ni lazima awe mwanamke;
  - (e) Tabibu Mfawidhi au Tabibu Mfawidhi Msaidizi, wa kituo cha afya, ambaye atakuwa Katibu wa kamati;
  - (f) Mjumbe mmoja atakayeteuliwa na Kamati ya Maendeleo ya kata kutokana na watu waliopendekezwa na Serikali za Mita zilizomo ndani ya eneo la Kata na;
  - (g) Mjumbe mmoja atakayeteuliwa na kamati ya Maendeleo ya Kata kutoka kwenye vyama vya kijamii kutoka kwenye Kata.
- (2) Mwenyekiti wa Kamati ya Afya ya Kata anachaguliwa kutoka miongoni mwa wajumbe
- (3) Endapo Kamati ya Afya ya kata itashindwa kutekeleza kazi zake,

Halmashauri itatoa onyo au kuvunja na kufanya utaratibu wa uchaguzi wa wajumbe wengine katika muda usiozidi miezi mitatu.

**Kazi au Majukumu ya kamati ya Afya ya kata**

17. – (1) Kamati ya Afya ya kata itakuwa na majukumu yafuatayo:-
- (a) kuwahamasisha na kuandaa jamii kujiunga na mfuko wa Afya ya Jamii;
  - (b) kuandaa orodha na kuratibu idadi ya wajumbe wa Mfuko wa Jamii;
  - (c) kusimamia ukusanyaji wa michango ya Mfuko;
  - (d) kuratibu viwango vya uchangiaji kwenye huduma za afya;
  - (e) Kupitia utendaji wa Mfuko wa Afya ya jamii na kutoa mapendekezo ya ufumbuz;
  - (f) kuanzisha na kuratibu mipango ya Afya ya jamii na;
  - (g) kuendesha mikutano ya wajumbe wa Mfuko wa Afya ya Jamii.
- (2) Kamati ya Afya ya kata itakaa kila baada ya miezi mitatu; na Katibu atatoa notisi ya maandishi wiki moja kabla ya siku ya kikao.

**Matumizi ya fedha za Mfuko**

18. Fedha zitakazokusanywa na Mfuko zitatumika kwa madhumuni yafuatayo:-
- (a) masuala yanayohusiana na afya yaliyotajwa katika mpango wa afya na kuidhinishwa na Wizara; na
  - (b) Suala au shughuli yoyote muhimu ya afya kama itakavyoonekana inafaa na kama itaidhinishwa na bodi.

**Utoaji wa kadi kwa wanachama**

19. – (1) Kila mwanachama wa Mfuko na wategemezi wake, atapewa Kadi baada ya kulipa mchango wake wa mwaka, ambao utapendekezwa na kamati ya afya ya kata na kupelekwa kwa halmashauri kwa ajili ya kuidhinisha baada ya kupitia kwenye Bodi.
- (2) Kila mtu atakayepewa msamaha ni lazima apewe kati ya uanachama na Halmashauri itaweka utaratibu wa kulipia

kadi hiyo.

**Haki za  
mwanachama  
na utoaji wa  
Huduma za  
afya.**

20. Kila mwanachama na wategemezi wake watakuwa na haki zifuatazo:-

- (a) kupata huduma ya afya aliyolipia anapougua ndani ya eneo la Halmashauri husika au katika kituo cha afya kwenye Halmashauri nyingine ambayo itaingia makubaliano maalum na Halmashauri husika.
- (b) Kupata huduma ya afya kwa baba, mama na watoto wao wenye umri chini ya miaka kumi na nane;
- (c) Kutoa mapendekezo kuhusu huduma za afya kupitia kituo chake cha tiba ambayo yatafanyiwa kazi na Bodi; na
- (d) Kushirikishwa kikamilifu katika uandaaji na utekelezaji wa mpango wa upatikanaji wa huduma za afya, katika eneo la Halmashauri.

**Kiwango cha  
mchango au  
ada ya  
mwanachama**

21. – (1) (a) mtu yeyote atakayetaka kuwa mwanachama wa mfuko wa afya ya jamii atapaswa kutoa kiasi cha shilingi elfu kumi (10,000/=) kwa kila kaya kwa mwaka.

(b) mchango huo utalipwa na kila mtu anayetaka kuwa mwanachama wa mfuko mwanzoni mwa mwaka au kila mwaka wa fedha unapoanza au kama Bodi itakavyoelekeza.

- (c) Mtu yeyote ana hiari ya kulipa mchango wake wa uanachama kwa zaidi ya mwaka mmoja;
- (e) Mtu yeyote ambaye si mwanachama wa Mfuko wa afya ya jamii atapaswa kutoa shilingi elfu saba (7,000) kama malipo ya hapo kwa papo.

(2) Bila kuathiri kifungu cha 21 (c) hapo juu mtu yeyote anayelipa mchango wa uanachama kwa zaidi ya mwaka mmoja, pale inapotokea mabadiliko ya kiwango cha mchango atawajibika kulipa tofauti ya kiwango kilichozidi kile cha awali.

**Mfuko wa  
wanachama**

22. (a) Mtu yeyote atabaki kuwa mwanachama wa mfuko wa afya ya jamii wa tiba kwa kadi kila atakapolipa ada yake ya mwaka;

- (b) kila mwaka unapoisha uanachama wa mtu utafikia mwisho hadi pale atakapotimiza masharti ya kifungu (a) hapo juu.

**Malipo ya papo kwa papo**

23. – (1) Mtu yeyote ambaye hatakuwa mwanachama wa mfuko huu atalipa mchango au malipo ya papo kwa papo kila atakapoenda kupata matibabu katika kituo cha kutolea huduma za afya kama ifuatavyo:-

(a) Shilingi 10,000/=.

**Makosa**

24. Mtu yeyote ambaye:-

- (a) atakwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi; au
- (b) atafanya kitendo chochote ambacho kitazuia Bodi kufanya kazi zake kwa ufanisi; au
- (c) atatumia vibaya mali na rasilimali za Mfuko na kusababisha kutofikia malengo ya Bodi; au
- (d) anatumia vibaya madaraka aliyonayo kumzuia afisa wa bodi kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria hii;
- (e) atashindwa kwa uzembe kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa sheria ndogo hizi.

Atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilijngi laki tatu (300,000/=) au kwenda jela kwa kipindi kisichozidi miezi kumi na mbili au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

**HATI YA KUKILI KOSA**

**(Chini ya kifungu cha 13)**

Mimi.....nakiri mbele  
ya.....Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya  
Kaliua kwamba mnamo tarehe .....ya mwezi  
.....mwaka.....nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha  
.....cha Sheria Ndogo za (CHF) za Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua

ya mwaka 2014. Nipo tayari kulipa kiasi cha ada/au ushuru ninaodaiwa pamoja na faini ikiwa Mkurugenzi ataamua kutekeleza mmlaka aliyopewa chini ya Sheria Ndogo zilizotajwa hapo juu.  
Nathibitisha kwamba maelezo ya hapo juu ni kweli nimeyatoa kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu.

Tarehe.....

Saini.....

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua libandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe .....Mwezi.....mwaka 2014..... na nembo hiyo ilibandikwa mbele ya:

.....  
**ABDALLAH S.NGODU.**  
Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya wilaya ya Kaliua.

.....  
**JOHN KADUTU**  
Mwenyekiti,  
Halmashauri ya wilaya ya Kaliua

**NIMEKUBALI.**

Dodoma,  
Tarehe.....2014

.....  
MH, MIZENGO P .PINDA.(MB)  
WAZIRI MKUU



TANGAZO LA SERIKALI Na.....La tarehe.....

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA YA WILAYA)

-----  
**SHERIA NDOGO**  
-----

*Zimetungwa chini ya Vifungu vya 7(1) na 16(1)*

**SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA KUCHINJA, KUWAMBA NA KUNUNUA  
NGOZI) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KALIUA ZA MWAKA 2014.**

- |                                   |   |
|-----------------------------------|---|
| <b>Jina na mwanzo wa kutumika</b> | 1. Sheria Ndogo hizi ziiitwe Sheria Ndogo za (Ushuru wa Kuchinja, Kuwamba na Kununua Ngozi) za Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua za mwaka 2014 na zitaanza kutumia mara baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.  |
| <b>Matumizi</b>                   | 2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya Halmashauri.   |
| <b>Tafsiri</b>                    | 3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo:-<br><br>“ <i>Afisa wa Halmashauri</i> ” maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.<br><br>“ <i>Halmashauri</i> ” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.<br><br>“ <i>Mnyama</i> ” maana yake ni ng’ombe, mbuzi na kondoo.<br><br>“ <i>Ngozi</i> ” maana yake ni ngozi ya ng’ombe, mbuzi na kondoo.                   |
| <b>Ushuru</b>                     | 4. – (1) Halmashauri itatoza ushuru kwa mtu yeyote atakayechinja mnyama au wanyama kwa ajili ya biashara katika eneo la Halmashauri kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali la kwanza.<br><br>(2) Mtu yeyote atakayewamba na kununua ngozi katika eneo la Halmashauri atalipa ushuru kama ilivyoonyeshwa katika jedwali la Sheria Ndogo hizi.<br><br>(3) Ushuru huo utalipwa kwa Afisa Muidhiniwa na mlipaji atapewa stakabadhi ya malipo yaliyofanyika. |

- (4) Hautakuwa ni utetezi kwa mtu yeyote kuwa amelipa ushuru iwapo hatakuwa na stakabadhi inayoonyesha ushuru aliolipa.

Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti yoyote ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo cha miezi kumi na mbili jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

5. ada ya ukaguzi wa gari la kubebea nyama itakuwa tsh 5000/= kwa mwezi

**JEDWALI LA KWANZA**

Aina ya Mnyama	Ushuru wa Kuchinja/machinjio	Ushuru wa Kuwamba	Ushuru wa Kununua Ngozi	Ada ya ukaguzi wa nyama
Ng'ombe	2,000/=	400/=	500/=	1000/=
Mbuzi	500/=	200/=	300/=	500/=
Kondoo	500/=	200/=	300/=	500/=
Nguruwe	2000/=			1000/=
Mnyama mwingine	2,00/=	500/=	500/=	500/=

**HATI YA KUKILI KOSA**

**(Chini ya kifungu cha 13)**

Mimi.....nakiri mbele ya.....Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Kaliua kwamba mnamo tarehe .....ya mwezi .....mwaka.....nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha .....cha Sheria Ndogo za (Kuchinja, kuwamba na kununua) za Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua ya mwaka 2014. Nipo tayari kulipa kiasi cha ada/au ushuru ninaodaiwa pamoja na faini ikiwa Mkurugenzi ataamua kutekeleza mamlaka aliyopewa chini ya Sheria Ndogo zilizotajwa hapo juu.

Nathibitisha kwamba maelezo ya hapo juu ni kweli nimeyatoa kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu.

Tarehe.....

Saini.....

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua libandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe .....Mwezi.....Mwaka 2014 na nembo hiyo ilibandikwa mbele ya:

.....  
**ABDALLAH S.NGODU,**  
Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.

.....  
**JOHN KADUTU,**  
Wenyekiti wa Halmashauri,  
Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua

**NIMEKUBALI**

.....  
**MHE.MIZENGO P.PINDA (MB).**  
WAZIRI MKUU.

**Dodoma,**  
**Tarehe.....2014.**

TANGAZO LA SERIKALI Na.....La tarehe.....

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA(MAMLAKA ZA WILAYA)

(SURA 290)

-----  
**SHERIA NDOGO**  
-----

*Zimetungwa chini ya Vifungu vya 7(1) na 16(1)*

**SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA UOGESHAJI NA UCHANJAJI WA MIFUGO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KALIUA ZA MWAKA 2014**

**Jina na mwanzo wa kutumika** 1. Sheria Ndogo hizi ziiitwe Sheria Ndogo za (Ushuru wa Uogeshaji wa Mifugo) za Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua za mwaka 2014 na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

**Matumizi** 2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya Halmashauri.

**Tafsiri** 3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo:-

“*Afisa Mifugo*” maana yake ni Daktari wa Mifugo wa Wilaya, mtaalam wa fani, mtaalam wa Mifugo wa Kata na Kijiji.

“*Halmashauri*” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua;

“*Mifugo*” maana yake ni ng’ombe, punda, mbuzi na kondoo;

“*Njia ya Mifugo*” maana yake ni mapitio ya mifugo kutoka zizini kwenda malishoni, joshoni na au mnadani;

“*Uogeshaji*” maana yake ni uogeshaji wa mifugo kwa maji yaliyochanganywa na dawa ya kuua kupe na wadudu wengine wanaoathiri mifugo;

“*Vikiundi vya ushirika vya wafugaji*” maana yake ni vyama vya Ushirika wa wafugaji vilivyoandikishwa chini ya Sheria Na.20 ya mwaka 2003 ya vyama vya ushirika.

**Ushuru** 4. Kutokuwepo na ushuru wa kuogeshwa mifugo itakayoogeshwa katika

majosho yanayoendeshwa na Halmashauri kwa kiwango kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi.

**Uogeshaji wa mifugo**

5. Uogeshaji wa mifugo katika eneo la Halmashauri ni wa lazima kama itakavyoelekezwa na Afisa Mifugo wa Wilaya na Serikali ya Kijiji. Njia za mifugo ni lazima zitunzwe na zinatakiwa kuwa na upana wa mita sabini.

**Vikundi vya wafugaji**

6. – (1) Katika maeneo ambayo majosho yanaendeshwa na vikundi vya ushirika vya wafugaji utaratibu wa kuchangia gharama za uendeshaji utazingatia katiba au utaratibu uliowekwa na Wanakikundi.
- (2) Vikundi vya ushirika vya wafugaji ni lazima vizingatie maelekezo ya Afisa Mifugo wa Wilaya, Kata na Kijiji katika shughuli zote za ufugaji wa mifugo.

**Uchanjaji wa Mifugo**

- (1) Kila Mfugaji lazima achanje na kuogesha Mifugo yake.

**Makosa Na adhabu**

7. Mtu yeyote atakayekiuka au kuvunja masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo cha miezi sita jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

**JEDWALI**

Aina ya Mifugo	Ushuru(Tshs.)
Ng'ombe, Punda	500/=
Mbuzi, Kondoo, Mbwa, Paka	200/=

**HATI YA KUKILI KOSA**

**(Chini ya kifungu cha 13)**

Mimi.....nakiri mbele  
ya.....Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Kaliua  
kwamba mnamo tarehe .....ya mwezi .....mwaka.....nilitenda

kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha .....cha Sheria Ndogo za (Uogeshaji wa Mifugo) za Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua ya mwaka 2014. Nipo tayari kulipa kiasi cha ada/au ushuru ninaodaiwa pamoja na faini ikiwa Mkurugenzi ataamua kutekeleza mamlaka aliyopewa chini ya Sheria Ndogo zilizotajwa hapo juu.

Nathibitisha kwamba maelezo ya hapo juu ni kweli nimeyatoa kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu.

Tarehe.....

Saini.....

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua ilibandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe .....Mwezi.....Mwaka 2014 na nembo ilibandikwa mbele ya:

.....  
**ABDALLAH S.NGODU**  
Mkurugenzi Mtendaji  
Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.

.....  
**JOHN KADUTU,**  
Mwenyekiti wa Halmashauri,  
Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua

NAMEKUBALI.

.....  
**MIZENGO P .PINDA(MB)**  
WAZIRI MKUU

Dodoma,  
Tarehe.....2014.

TANGAZO LA SERIKALI Na.....La tarehe.....

**SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)**

(SURA 287 )

-----  
**SHERIA NDOGO**  
-----

*Zimetungwa chini ya kifungu cha 153*

**SHERIA NDOGO ZA (KILIMO NA UHIFADHI WA CHAKULA) ZA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA KALIUA 2014**

- Jina** 1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Kilimo na Uhifadhi wa chakula) za Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye gazeti la Serikali.
- Matumizi** 2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.
- Tafsiri** 3. Katika Sheria ndogo hizi isipokuwa itakapohitajika vinginevyo:-
- “*Afisa Mwidhiniwa*” maana yake ni Mtumishi wa umma atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi:
- “*Halmashauri*” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua;
- “*Mazao ya biashara*” maana yake ni Pamba, Tumbaku, Ufuta, Alizeti, Michungwa, Midimu, Mwembe, Viazi, Mananasi, Mahindi, Mtama Mpunga na Uwele
- “*Mkazi*” maana yake ni mtu mwenye umri wa miaka 18 au zaidi ambaye kwa kawaida anaishi katika eneo la kijiji au mtaa au kitongoji katika Halmashauri;
- “*Mkurugenzi*” maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri pamoja na Afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.
- Wajibu wa** 4. Kila kaya katika eneo la Halmashauri anayemiliki ardhi ya kilimo chini ya sheria yeyote ile na mwenye uwezo wa kufanya kazi, atatakiwa



- Kulima** kulima eneo lisilopungua hekari mbili ya mazao ya chakula kutoka familia yake kwa mwaka mzima
- Kuvuna** 6. Kila mkazi atakayelima shamba katika eneo la Halmashauri atatakiwa kuvuna mazao katika njia ya usafi ili kutunza ubora wake na kuhifadhi katika njia ya usalama.
- Kuthibi-Tisha** 7. Serikali ya Kijiji kupitia uongozi wa Kitongoji itakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa kila mkazi wa kijiji husika anajitosheleza kwa chakula.
- Ukaguzi** 8. Afisa mwidhiniwa anaweza:-
- (a) kuingia kwenye eneo la kilimo au katika shamba au katika kihenge kwa madhumuni ya kuelekeza kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;
  - (b) kumkamata na kumpeleka katika chombo cha sheria mtu yeyote atakayevunja Sheria Ndogo hizi.
- Makosa** 9. – (1) Itakuwa ni kosa kwa:-
- (a) anayemiliki ardhi ya kilimo kushindwa kulima mazao ya chakula.
  - (b) kutotunza shamba;
  - (c) kutovuna mazao yaliyoko shambani ambayo yamefikia wakati wa kuvunwa;
  - (d) kutokuwa na kihenge cha kuhifadhia mazao na kukitumia;
  - (e) kutohifadhi chakula cha kutosha;
  - (f) kuuza mazao bila kuweka akiba ya mwaka mzima.
- Adhabu** 10. Mtu yeyote atakayevunja masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/-) au kifungo kisichozidi miezi sita jela au adhabu zote kwa pamoja.

## HATI YA KUKILI KOSA

(Chini ya kifungu cha 13)

Mimi.....nakiri mbele  
ya.....Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Kaliua  
kwamba mnamo tarehe .....ya mwezi .....mwaka.....nilitenda kosa  
la kukiuka masharti ya kifungu cha .....cha Sheria Ndogo za (Kilimo na  
uhifadhi wa chakula) za Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua ya mwaka 2014. Nipo  
tayari kulipa kiasi cha ada/au ushuru ninaodaiwa pamoja na faini ikiwa  
Mkurugenzi ataamua kutekeleza mamlaka aliyopewa chini ya Sheria Ndogo  
zilizotajwa hapo juu.

Nathibitisha kwamba maelezo ya hapo juu ni kweli nimeyatoa kwa hiari yangu  
kadri ya ufahamu wangu.

Tarehe.....

Saini.....

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua libandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe .....Mwezi.....Mwaka 2014 na nembo ilibandikwa mbele ya:

.....  
ABDALLAH S NGODU,  
Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua

.....  
JOHN KADUTU,  
Mwenyekiti,  
Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.

**NIMEKUBALI.**

.....  
MHE,MIZENGO P.PINDA(MB)  
WAZIRI MKUU

**Dodoma**  
**Tarehe.....2014.**

TANGAZO LA SERIKALI Na.....La tarehe.....

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(Sura ya 290)

**SHERIA NDOGO**

*Zimetugwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16 (1)*

**SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KALIUA ZA MWAKA, 2014.**

- |                            |    |  |
|----------------------------|----|--|
| Jina na mwanzo wa kutumika | 1. | Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua za Mwaka, 2014 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali  |
| Eneo la matumizi           | 2. | Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua  |
| Tafsiri                    | 3. | <p>Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa kama itaelekezwa vinginevyo;</p> <p>“Ada” maana yake ni malipo yanayolipwa kwa ajili ya huduma na vibali vitolewavyo na Halmashauri;</p> <p>“Afisa mwidhiniwa” maana yake ni Afisa biashara wa Halmashauri, Afisa mtendaji na Afisa yeyote atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;</p> <p>“Afisa Mtendaji” maana yake ni:-</p> <p>(a) Linapotumika kuhusiana na kata maana yake ni Afisa Mtendaji wa Kata.</p> <p>(b) Linapotumika kuhusiana na Kijiji, maana yake ni Afisa Mtendaji wa kijiji.</p> <p>“Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.</p> <p>“Kibali” maana yake ni idhini ya maandishi kutoka Halmashauri kwa ajili ya kuendesha shughuli yoyote;</p> <p>“Mkurugenzi” maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Kaliua;</p> <p>“Ushuru” maana yake ni malipo yanayolipwa kwa ajili ya kupata</p> |

huduma au kuendesha biashara kwenye eneo la Halmashauri;

“*Vibanda*” maana yake ni vibanda vya biashara vilivyojengwa katika viwanja vinavyomilikiwa na Halmashauri au watu binafsi;

“*Wakala*” maana yake ni mtu, kikundi cha watu, kampuni au taasisi iliyoteuliwa kwa niaba ya Halmashauri kukusanya ushuru wa Halmashauri:

“*Waziri*” maana yake ni waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa.

- |                                |    |     |  |
|--------------------------------|----|-----|--|
| Utozaji wa Ada na Ushuru       | 4. | (1) | Halmashauri itatoza Ada na Ushuru kwa ajili ya huduma, vibali na leseni zitolewazo kama zilivyooneshwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi   |
|                                |    | (2) | Ada na Ushuru utakaotzwa chini ya Sheria Ndogo hizi unapaswa kulipwa kabla ya huduma kutolewa.   |
|                                |    | (3) | Halmashauri au wakala atatoa stakabadhi yenye nembo ya Halmashauri kama kielelezo cha malipo ya Ada au Ushuru;   |
| Wajibu wa kulipa ada au ushuru | 5  |     | Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayestahili kulipa Ada au Ushuru utozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kulipa Ada au Ushuru kama ilivyoelekezwa kenye jedwali la Sheria Ndogo hizi;  |
| Ukusanyaji wa ada na ushuru    | 6  | (1) | Ikiwa mtu yeyote anayetakiwa kulipa Ada na Ushuru atashindwa kulipa ndani ya muda unaotakiwa kulipa, Halmashauri inaweza kukusanya Ada hizo kwa njia ya kufungua kesi ya madai mahakamani.   |
|                                |    | (2) | Bila ya kuathiri masharti yaliyowekwa katika kifungu cha 6 (1) Halmashauri inaweza kukusanya madeni ya Ada na Ushuru kwa njia ya kukamata na kushikilia mali zinazohamishika za mdaiwa zenye thamani sawa na deni la Ada au Ushuru unaodaiwa.  |
|                                |    | (3) | Baada ya siku kumi na nne (14) kupita kuanzia tarehe ya kukamata mali za mdaiwa Halmashauri itakuwa na uwezo wa kuziua kwa njia ya mnada mali zilizokamatwa baada ya Mkurugenzi kutoa taarifa ya maandishi siku ishirini na moja (21) ya kusidio la kuuza mali hizo baada ya siku ishirini na moja kuisha, Halmashauri itauza mali hizo; |
| Wakala                         | 7. | (1) | Halmashauri inaweza kumteua wakala wa kukusanya Ada na Ushuru kwa ajili ya eneo lote au sehemu ya Halmashauri..  |
|                                |    | (2) | Halmashauri inaweza kutangaza Zabuni ya ukusanyaji Ushuru wa minada na mifugo kwa kuingia mkataba na wakala atakayeshinda  |

		zabuni hiyo. Wakala huyo atawajibika kukusanya Ushuru huo ikiwa ni mtu binafsi, kampuni, au taasisi, kutegemea na mkataba utakaosainiwa na wakala huyo na Halmashauri
	(3)	Wakala atakayeteuliwa na Halmashauri kutekeleza jukumu lolote chini ya Sheria Ndogo hizi atawajibika kusimamia ukusanyaji wa Ushuru huo kwa viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hizi na atakuwa na uwezo wa kumshitaki mtu yeyote atakayeshindwa kwa makusudi kulipa Ushuru anaotakiwa kulipa.
Wajibu wa wakala	8.	. Wakala atakuwa na majukumu yafuatayo kwa Halmashauri;- (a) Kukusanya na kupokea ushuru kwa viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hizi kwa niaba ya Halmashauri katika eneo ambalo ameteuliwa kukusanya ushuru husika; (b) Kuwasilisha makusanyo yote anayowajibika kukusanya kwa kuzingatia mkataba alioingia na Halmashauri (c) Kutoa taarifa kwa Halmashauri kuhusiana na mtu yeyote ambaye kwa makusudi amekataa au ameshindwa kulipa Ushuru husika; na (d) Pale inapowezekana kuishauri Halmashauri juu ya kuboresha ukusanyaji wa Ushuru; (e) Kutoa taarifa ya mwenendo wa mapato kila baada ya Miezi mitatu (3)
Kutowajibika kwa Halmashauri	9.	Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote na kwa namna yoyote ile itakayo tokea aidha wakati wa kukusanya madeni au kwa mali zitakazokamatwa na kushikiliwa na Halmashauri;
Wajibu wa mfanyabiashara	10	Itakuwa ni wajibu wa kila mfanyabiashara ndani ya Halmashauri kuendesha shughuli zake za biashara katika maeneo ya masoko.
Wajibu wa kila mtu	11	Itakuwa ni wajibu wa kila mtu binafsi, taasisi, au kampuni zinazojihusisha na shughuli za utafiti, uchimbaji, au uuzaji wa rasilimali za madini katika eneo la Halmashauri kuhakikisha kwamba wamejisajili katika rejesta maalum ya Halmashauri kabla ya kuanza shughuli zozote ndani ya eneo la Halmashauri.
Makosa	12 (1)	. Itakuwa ni kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi endapo mtu yeyote;- (a) Atakataa au atashindwa kutii agizo lolote atakalopewa na Afisa mwidhiniwa au wakala (b) Atakataa au atajaribu kukataa kulipa Ada na Ushuru; (c) Atashawishi mtu, watu, au kundi la watu kukataa kulipa Ushuru na/au Ada; (d) Atakwepa au kujaribu kukwepa kulipa Ada na/au Ushuru; (e) Atamzuia Afisa mwidhiniwa kutekeleza majukumu yake kisheria (f) Atafanya biashara nje ya maeneo yaliyoainishwa kama eneo la kufanyia biashara.

(2)

Adhabu

13

Mtu yeyote atakayekiuka Sheria Ndogo hizi atakiri kosa hilo kwa kujaza fomu maalumu mbele ya mkurugenzi ili kufifilisha kosa kama ilivyo katika Sheria Ndogo hizi.

Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa la na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi Elfu Hamsini (50,000/=) au kifungo cha miezi sita jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

**JEDWALI**

**SEHEMU: A**

**ADA NA USHURU WA MAZAO YA MALIASILI**

<b>AINA YA ZAO</b>	<b>KIWANGO CHA USHURU</b>
Kibali cha kuvuna mti/ miti	1000/= kwa kila mti
Ada ya usajili wa biashara ya mazao ya misitu	100,000/= kwa mwaka

**SEHEMU: B**

**ADA YA MBAO ZA MATANGAZO YA BIASHARA NA PROMOSHENI**

<b>AINA YA TANGAZO</b>	<b>KIWANGO CHA USHURU</b>
Sigara	30,000/= kwa mwaka
Bia	30,000/= kwa mwaka
Coca cola /pepsi	30,000/= kwa mwaka
Sabuni	15,000/= kwa mwaka
Benki	30,000/= kwa mwaka
Simu- TTCL	30,000/= kwa mwaka
Simu za mikononi	30,000/= kwa mwaka
Posta	30,000 kwa mwaka
Vituo vya mafuta	50,000/= kwa mwaka
Bar	20,000/= kwa mwaka
Nyumba za wageni	20,000/= kwa mwaka
Hoteli	10,000/= kwa mwaka
Maduka ya kawaida	10,000/= kwa mwaka
Mbao za samani	10,000/= kwa mwaka
Mashine za nafaka	10,000/= kwa mwaka
Karakana	20,000/= kwa mwaka
Duka la dawa	5,000/= kwa mwaka
Ushauri wa kitaalamu	15,000/= kwa mwaka
Vitalu na vifaa vya ofisni	10,000/= kwa mwaka
Kununua na kuuza mazao	10,000 kwa mwaka
Kuvumisha matangazo kwenye vyombo vya barabara kwa kutumia vipaza sauti	20,000/= kwa kila tukio

**SEHEMU: A**  
**USHURU WA KUEGESHA MAGARI YANAYOINGIA KATIKA**  
**MAGULIO, MASOKO NA MINADA.**

AINA YA GARI	USHURU KWA SIKU
Gari / basi kubwa	1500/=
Magari madogo (hiace)	1000/=
Taxi	500/=
Pikipiki	200/=
Magari binafsi yasiyo ya biashara	500/=
Gari dogo la mizigo (lori au pick up) chini ya tani 7	2000/=
Gari kubwa la mizigo zaidi ya tani 7	3000/=

**SEHEMU: B**

**II: MATANGAZO YANAYONG'AA**

Yasiyozidi sq ft 1	50,000/= kwa mwaka
Yanayozidi sq ft 2 lakini siyo zaidi ya sq mt 2	100,000/= kwa mwaka
Yanayozidi sq mt 2	120,000/= kwa mwaka

**SEHEMU C.**

**USHURU WA MACHINJIO**

Aina ya Mifugo	Kiwango cha ushuru
Ng'ombe	3000
Mbuzi	1000
Kondoo	1000
Nguruwe	3000

**SEHEMU: D**

**USHURU KATIKA MASOKO NA MAGULIO.**

AINA YA BIASHARA	USHURU KWA SIKU
Biashara ya nguo za mitumba	500/=
Biashara za nguo za madukani	500/=
Biashara ya viatu vya mitumba	500/=
Biashara ya mama lishe	500/=
Biashara ya vileo	500/=
Biashara ya kuuza nyama	500/=
Michezo mbalimbali katika soko	500/=
Biashara za bidhaa za urembo	500/=
Biashara ya vyombo vya ndani	500/=
Biashara ya samaki mbalimbali	500/=
Minada ya hadhara ( auctioner's charge)	5,000/=
Miwa	2,000/= kwa tela



**SEHEMU: E**  
**USHURU WA NGOZI**

AINA YA NGOZI	KIWANGO CHA USHURU
Ngozi ya ng'ombe	300/= kwa kipande
Ngozi ya mbuzi	200/= kwa kipande
Ngozi ya kondoo	200/= kwa kipande

**SEHEMU: F**  
**ADA ZA BURUDANI**

<b>Aina ya burudani na utamaduni</b>	<b>Ada na ushuru wa kibali</b>
Mziki wa disiko	50,000/= kwa tukio
Muziki na dansi	50,000/= kwa tukio
maigizo ya mazingaombwe kwa siku moja	2,000/= kwa tukio
kuonyesha video au sinema kwa siku moja	5,000/= kwa tukio
Leseni ndogo kwa waganga wa kienyeji	30,000/= kwa mwaka
Matangazo au promosheni	50,000/= kwa tukio
Mshindani ya urembo (miss)	50,000/= kwa tukio
Salon	20,000/= kwa mwaka
Wasambazaji wa kebo (cables)	10,000/= kwa mwezi
Muziki wa taarabu	10,000/= kwa kila tukio
Vituo vya Tv, na radio	50,000/= kwa mwezi
Mchezo wa puli (pool table)	30,000/= kwa mwaka
Wamiliki wa kumbi za burudani	10,000/= kwa mwezi
Kupiga picha za video	5000/= kwa tukio
Burudani nyinginezo	5000/= kwa kila tukio
Usajili wa vikundi vya sanaa	75,000/=

**SEHEMU: G**  
**ADA YA UKAGUZI NA IDHINI YA UJENZI**

<b>AINA YA JENGO</b>	<b>KIASI (SHILING)</b>
Minara ya simu (telephone tower)	250,000/=
Ghorofa (2 stores and above)	150,000/=
Nyumba za biashara ( gesti, hoteli, maduka)	50,000/=
Kituo cha mafuta	100,000/=
nyumba za makazi	5,000/=
Nyumba za makazi na biasahara	20,000/=
Shule binafsi, na Hospitali binafsi	50,000/=
Ofisi binafsi	100,000/=
Maghala na Bohari	100,000/=
Uzio wa ujenzi	50,000/=
Majengo mengine ambayo hayajatajwa	20,000/=

**SEHEMU: H**  
**ADA YA MABADILIKO YA JENGO LILILOPO**

<b>AINA YA JENGO</b>	<b>KIASI (SHILINGI)</b>
Nyumba ya kuishi	5,000/=

Nyumba ya biashara	10,000/=
Gholofa	100,000/=
Kiwanda, bohari, ghala, n.k	100,000/=
Majengo mengine ambayo hayajatajwa hapa	10,000/=

SEHEMU: I

ADA YA KUKODI MAGARI YA HALMASHAURI	
AINA YA GARI	ADA YA KUKODI
GARI NDOGO.....	1,600/= Kwa kila kilomita moja
MALORI.....	250,000/= Kwa masaa
GREDA .....	650,000/= kwa masaa manane

SEHEMU: J

ADA YA KUOMBA ZABUNI	
AINA YA ZABUNI	KIASI CHA ADA
Uwakala	100,000/=
Zabuni zingine	100,000/=

SEHEMU: K

USHURU WA KITUO CHA MABASI YA ABIRIA	
Idadi ya abiria	Kiwango cha ushuru kwa siku
4 – 9	1,000/=
10 – 25	1,500/=
26 – 35	2,000/=
36 – 65	3,000/=
66 au zaidi	5,000/=

SEHEMU: L

USHURU WA KUEGESHA MAGARI YA MIZIGO	
Uzito wa gari	Kiwango cha ushuru kwa siku
Chini ya tani 3	1,000/=
Tani 3-6	2,500/=
Tani 7-10	5,000/=
Zaidi ya tani 10	10,000/=

SEHEMU: M

USHURU WA MIFUGO MINADANI

Aina ya Mifugo	Kiwango cha ushuru
Ng'ombe	5,000/=

Mbuzi	1500/=
Kondoo	1500/=
Kuku /Bata	200/=
Punda.....	5000/=

**SEHEMU: O**

Vibanda vya mama lische ndani na nje ya soko sh 200/=kwa siku  
 Vyumba vya maduka ndani ya Soko sh 50,000/= kwa mwezi  
 Kukodi meza ndani ya soko sh 15,000/=  
 Ushuru wa meza ndani ya Soko sh 200 kwa siku  
 Meza za nje ya soko mitaani sh 200 kwa siku  
 Meza za samaki sh 200/=  
 Meza za matunda sh 200/= kwa siku  
 Wauza kuku sh 5000/=kwa mwezi  
 Wauza mitumba ndani ya soko sh 200 kwa siku  
 Kukodi ukumbi wa Halmashauri 150,000/=

**HATI YA KUKIRI KOSA**

Tarehe.....

Hati Na..... ya mwaka 20.....

Mimi.....  
 ..... nakiri Chini ya kifungu cha 8  
 cha Sheria Ndogo hizi za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya  
 Wilaya ya Kaliua za mwaka 2014 kutenda makosa yafuatayo:-

- 1.....
- 2.....
- 3.....

Kwa hiari yangu ninakubali kuadhibiwa kwa kulipa faini ya  
 Shilingi.....(kwa maneno.....)  
 badala ya kushitakiwa mahakamani kwa makosa haya.

Saini ya Mkosaji.....  
 Tarehe.....

**ADHABU/FAINI HII IMETOLEWA NA:-**

Jina.....  
 Cheo.....  
 Saini.....  
 Tarehe.....

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua ilibandikwa katika Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe.....mwezi.....mwaka 2014 na nembo hiyo ilibandikwa mbele ya;-

.....  
**ABDALLAH S.NGODU**  
Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.

.....  
**JOHN KADUTU**  
Mwenyekiti,  
Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.

NIMEKUBALI.

.....  
**MHE.MIZENGO P.PINDA(MB)**  
WAZIRI MKUU.

Dodoma  
Tarehe.....2014.

TANGAZO LA SERIKALI Na. .... La tarehe .....

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(Sura ya 290)

**SHERIA NDOGO**

*Zimetugwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16 (1)*

**SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MINADA YA MIFUGO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KALIUA ZA MWAKA 2014**

- Jina na tarehe ya kuanza kutumika** 1. Sheria ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ushuru wa Minada ya Mifugo) za Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua 2014 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali
- Matumizi** 2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililoko chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua;
- Tafsiri** 3. Katika Sheria hii, isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo:
- “*Afisa mwidhiniwa*” maana yake ni Afisa Mtendaji wa kijiji, Afisa Mtendaji wa Kata au Mtumishi aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;
- “*Bidhaa*” maana yake ni vitu mbalimbali vinavyoweza kupatikana katika duka au eneo la mnada;
- “*Halmashauri*” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua;
- “*Mkurugenzi*” maana yake ni Mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri pamoja na Afisa yeyote wa umma aliyeteuliwa kufanya kazi za Mkurugenzi;
- “*Mfugaji*” maana yake ni Mtu yeyote au kikundi cha watu au chama kinachojishughulisha na ufugaji wa mifugo;
- “*Mifugo*” maana yake ni aina zote za wanyama wanaofugwa au wanaoweza kufugwa na binadamu ikiwa ni pamoja na Ng’ombe, Mbuzi, Kondoo, Punda, Nguruwe, kuku na Bata;
- “*Ushuru*” maana yake ni malipo ya mnada wa mifugo na bidhaa zinginezo zinazouzwa kwenye eneo la mifugo;

“Wakala” maana yake ni Mtu binafsi, Kikundi au Watu, Kampuni, au Taasisi aliyeteuliwa kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri.

**Wajibu wa kulipa Ushuru**

4. – (1) Kutakuwepo na ushuru wa minada ya mifugo utakaolipwa na kila mnunuzi wa mifugo kwenye eneo la Sheria Ndogo hizi;
- (2) Ushuru huo utalipwa siku ya mnada katika eneo la Halmashauri ambapo mnada huo unafanyika;

**Ukusanyaji wa Ushuru**

5. – (1) Halmashauri itakusanya Ushuru huo kwa kumtumia Afisa mwidhiniwa au wakala ambaye atawasilisha mapato ya ushuru kwa Halmashauri.
- (2) Halmashauri itatoa vitabu vya ushuru kwa Afisa mwidhiniwa au wakala kama stakabadhi kwa ajili ya ukusanyaji wa ushuru wa minada ya mifugo;

**Usimamizi na Ukaguzi vitabu vya Ushuru**

6. – (1) Afisa mwidhiniwa anaweza kukusanya vitabu vya Ushuru wa mnada kwa ajili ya kufanya uchaguzi;
- (2) Mnunuzi atawajibika kuonyesha stakabadhi ya malipo ya Ushuru kwa Afisa mwidhiniwa mara atakapohitajika kufanya hivyo.
7. – (1) Mtu yeyote ambaye anasafirisha mifugo atatakiwa kuwa na kibali cha kusafirisha mifugo hiyo kutoka kwa Afisa mifugo wa sehemu ambapo mifugo hiyo inatoka.
- (2) Mtu yeyote atakayechinja mfugo au mifugo atatakiwa kuhakikisha kuwa nyama hiyo imepimwa na kupata kibali toka kwa Afisa mifugo.

**Makosa na Adhabu**

8. – (1) Mtu yeyote ambaye:-
- (i) atashindwa au kukataa kuonyesha stakabadhi ya malipo ya ushuru;
  - (ii) atasafirisha mifugo bila kibali cha Afisa mifugo;
  - (iii) atakataa au kukwepa kulipa ushuru.
  - (iv) Atakataa au kukwepa kulipa ushuru
  - (v) Atamshawishi mtu au kundi la watu wasilipe ushuru.

(vi) Atamzuia Afisa Muidhiniwa kutekeleza majuukumu yake.

Atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini (Tsh.50,000.00) au kifungo kisichozidi miezi sita jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

(2) Bila kuathiri masharti yaliyowekwa chini ya kifungu cha (1) endapo uvunjaji wa Sheria Ndogo hizi umesababisha hasara kwa Halmashauri, mtuhumiwa atawajibika kulipa fidia ya hasara iliyotokana na uvunjaji wa Sheria Ndogo hizi.

**JEDWALI ‘A’**  
**Chini ya kifungu cha 4**

Bidhaa	Ushuru
Ng’ombe .....	5,000.00
kwa siku	
Punda .....	5,000.00
kwa siku	
Nguruwe.....	5,000.00
kwa siku	
Mbuzi .....	1500.00
kwa siku	
Kondoo .....	1500.00
kwa siku	
Kuku .....	200.00
kwa siku	
Bidhaa ndogo ndogo .....	1,000.00 kwa siku

**JEDWALI ‘B’**  
**ORODHA YA MNADA**

- (a) Kasungu
- (b) King’wangoko

- (c) Ulyankulu
- (d) Upele
- (e) Makubi
- (f) Nhwande
- (g) Mwabayanda
- (h) Mwamunange
- (i) Mkuyuni
- (j) Usinge
- (k) Na minada yote itakayoanzishwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.

## **HATI YA KUKILI KOSA**

**(Chini ya kifungu cha 13)**

Mimi.....nakiri mbele ya.....Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Kaliua kwamba mnamo tarehe .....ya mwezi .....mwaka.....nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha .....cha Sheria Ndogo za (Minada na Mifugo) za Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua za mwaka 2014. Nipo tayari kulipa kiasi cha ada/au ushuru ninaodaiwa pamoja na faini ikiwa Mkurugenzi ataamua kutekeleza mamlaka aliyopewa chini ya Sheria Ndogo zilizotajwa hapo juu.

Nathibitisha kwamba maelezo ya hapo juu ni kweli nimeyatoa kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu.

Tarehe.....

Saini.....



Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua ilibandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe .....Mwezi.....Mwaka 2014 na nembo hiyo ilibandikwa mbele ya:

.....  
ABDALLAH S .NGODU,  
*Mkurugenzi Mtendaji,*  
*Halmashauri ya wilaya ya Kaliua*

.....  
JOHN KADUTU  
*Mwenyekiti.*  
*Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.*

NIMEKUALI,

.....  
MHE. MIZENGO P.PINDA (MB)  
WAZIRI MKUU

Dodoma  
Tarehe.....2014.

TANGAZO LA SERIKALI Na.....la tarehe.....

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA YA WILAYA)

(SURA 290)

-----  
**SHERIA NDOGO**  
-----

*Zimetungwa chini ya vifungu vya 7(1) na (16(1))*

**SHERIA NDOGO ZA (KODI YA HUDHUMA) ZA HALMASHAURI  
YA WILAYA YA KALIUA. 2014.**

**Jina na mwanzo wa kutumika** 1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria ndogo za (Kodi ya Huduma) za Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua, 2014 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

**Matumizi** 2. Sheria ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.

**Tafsiri** 3. Katika sheria ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:-

“*Afisa Muidhiniwa*” maana yake ni Afisa yeyote wa umma au mtu mwingine aliyeteuliwa na halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria ndogo hizi;

“*Halmashauri*” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.

“*Hesabu*” maana yake ni jumla ya mauzo au manunuzi ikiwa pamoja na kodi na ada, katika mwaka wa mapato;

“*Hesabu za mwisho*” ina maana ya Hesabu za mwisho zinazowasilishwa na Taasisi yoyote ya kibiashara baada ya kipindi cha hesabu kwa mujibu wa aya ya 9 ya Sheria Ndogo hizi pamoja na nyaraka au maelezo yatakayotakiwa kutolewa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

“*Jumuisho*” ina maana ya taarifa, nyaraka au hesabu au maelezo yoyote yahusuyo kiasi na thamani ya kifedha ya bidhaa au huduma zilizozalishwa, zilizosambazwa, zilizotolewa na au kuuzwa kibiashara na ikiwa ni pamoja na jumuisho la awali au la mwisho.

“*Kipindi cha hesabu*” ina maana ya muda ambao mfanyabiashara anatakiwa kuwasilisha hesabu za biashara zake;

“*Mkurugenzi*” maana yake ni Mkurugenzi wa halmashauri ya Wilaya ya Kaliua pamoja na Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

“*Mkusanya ushuru*” maana yake ni mtumishi au wakala aliyeteuliwa na Halmashauri kukusanya Ushuru kwa mujibu wa Sheria ndogo hizi;

“*Mwaka wa Mapato*” maana yake ni kipindi cha miezi kumi na mbili ya kalenda ya mwaka;

“*Taasisi ya kibiashara*” ina maana ya Taasisi iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni au Sheria ya Majina ya kibiashara inayojihusisha na shughuli za kiuchumi za uzalishaji wa bidhaa au mazao ya kilimo, usambazaji wa bidhaa, au utoaji wa huduma na, au biashara ikiwemo uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi.

- Utozaji wa kodi** 4. Halmashauri itatoza na kukusanya kodi ya huduma kwa mujibu wa Sheria ndogo hizi kutoka kwa kila taasisi ya kibiashara katika kila mwaka wa mapato ambayo ni sawa na asilimia sifuri nukta tatu (0.3%) yas hesabu ya shughuli zote zikiwemo uzalishaji wa bidhaa za huduma kutoka nje ya nchi zinazofanyika katika eneo la halmashauri ukiondoa kodi ya ongezeko toa thamani na kodi ya mlaji.
- Uwasilishaji wa taarifa kuhusu shughuli za kibishara** 5. Mkurugenzi wa taarifa ya maandishi, anaweza kutaka mlipa kodi au mkusanya kodi yeyote kuwasilisha hesabu zenye taarifa kamili za shughuli za kibiashara zikionesha kiasi cha thamani ya kifedha au bidhaa au huduma zilizozalishwa, kutolewa, kuingizwa, kusambazwa au kuuzwa kibishara na taarifa ya fedha katika kipindi maalum kisichozidi siku thelathini tangu tarehe ya taarifa hiyo.
- Uwasilishaji wa taarifa** 6. Mkurugenzi anaweza kwa taarifa ya maandishi kumutaka mtu yeyote mwenye taarifa au maelezo kuhusu taasisi yoyote ya kibiashara inayopaswa kulipa kodi kwa mujibu wa sheria Ndogo hizi, kuwasilisha kwake taarifa au maelezo hayo katika kipindi kisichopungua siku thelathini tangu tarehe ya agizo hilo.
- Uwezo wa kuingia kwenye** 7. Mkurugenzi anaweza kumwagiza kwa maandishi Afisa Muidhiniwa kuingia kwenye jingo au eneo la taasisi ya kibiashara au la mlipa au mjkusanya kodi yeyote kwa nia ya kufanya uchunguzi na tathmini ya

- jengo** kumbukumbu za biashara, vitabu vya hesabu, na taarifa nyinginezo kama atakavyoona inafaa kufanyiwa uchunguzi kwa ajili ya kupata na kujua kiwango sahihi cha kodi anachotakiwa kulipa mlipa kodi au mkusanya kodi hiyo.
- Uwasilishaji** 8. – (1) Mkurugenzi anaweza, kwa taarifa ya maandishi, kumtaka mlipa kodi au mkusanya kodi yeyote kuwasilisha kwake kumbukumbu za biashara na vitabu vya hesabu, kwa nia ya kupata taarifa kwa ajili ya kufanyiwa tathmini au kukusanya kodi ya huduma.
- (2) Kwa nia ya kupata taarifa kwa mujibu wa Sheria ndogo ya 8(1) Mkurugenzi anaweza kumtaka mtu yeyote kufika mbele yake au kwa Afisa Muidhiniwa katika muda na mahali kadiri atakavyoona inafaa.
- Uteuzi wa mkusanya kodi** 9. Kila mlipa au mkusanya kodi ya huduma atatakiwa kutoa na au kuwasilisha hesabu za awali na kulipa kodi anayotakiwa katika muda kama ifuatavyo:-
- (a) kwa waagizaji bidhaa kutoka nje ya nchi watalipa kodi katika muda kama itakavyokuwa imeelekezwa na kamishina wa ushuru wa forodha na kodi ya mlaji.
- (b) Waszalishaji wa bidhaa za viwandani watalipa ushuru kama itakavyokuwa imeelekezwa na kamishina wa kodi ya Ongezeko la thamani (VAT) isipokuwa haitakuwa zaidi ya muda wa kulipa ushuru wa mlaji au (VAT).
- (c) Watu wengine wanalipa katika awamu nne (4) awamu ya kwanza ikianzia katika kipindi cha miezi mitatu baada ya kuanzia kipindi cha mahesabu.
- Jumla ya riba kutozwa kwenye kodi isiyolipwa** 10. Mkurugenzi anaweza kuteua Kamishina wa ushuru wa forodha au kodi ya mapato kutathimini na kukusanya kodi ya huduma na kuwasilisha kwa Halmashauri kwa wakati kama ilivyoelekezwa kwenye Sheria ndogo ya 9 kwa lengo la kufanya tathmini, kukusanya na kupata ushuru pamoja na madeni yake.
- Kushindwa kutimiza maagizo** 11. – (1) Kiwango cha kodi kitakuwa ni asilimia 0.3% ya hesabu ya shughuli zote baada ya kuondoa kodi ya ongezeko la thamani ya kodi ya mlaji.

- (2) Mkusanya kodi au mlipa kodi yeyote akishindwa kuwasilisha kodi yake au ya mlipa kodi, atachukuliwa kama hajalipa kodi na anastahili au kiuwajibika kulipa kodi hiyo kama vile ndiye mlipa kodi wa Halmashauri, na njia zote za kukusanya madeni zitatumika dhidi yake kama vile ndiye mlipa kodi husika.
- (3) Bila ya kuathiri masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hizi Mkurugenzi anaweza kuteua wakala kukusanya kodi ya huduma kwa niaba yake na wakala huyo atakuwa na jukumu la:
  - (a) kuwasilisha majumuisho kwa Mkurugenzi au Afisa muidhiniwa;
  - (b) kuwasilisha kodi iliyokusanywa katika kipindi maalum.

**Utoaji wa taarifa ya uongo**

12. – (1) Kila mlipa kodi au mkusanya kodi atatakiwa kuwasilisha kwa Halmashauri hesabu za mwisho katika kipindi cha miezi mine tangu kumalizika kwa kipindi cha hesabu ya kodi anachostahili katika mkupuo mmoja.
- (2) Mlipa kodi au mkusanya kodi anapowasilisha hesabu zake, Afisa muidhiniwa anaweza:-
  - (a) kupokea na kukubali hesabu hizo na kutathmini kodi katika msingi huo;
  - (b) kufanya tathmini katika kiwango cha hesabu chamlipa kodi huyo iwapo atakuwa na hisia za kimsingi za kuamini kuwa hesabu hizo siyo sahihi.
- (3) Iwapo mlipas kodi hajawasilisha majumuisho ya hesabu zake kwa mwaka wowote wa pato aidha ametakiwa kufanya hivyo na Mkurugenzi au Afisa muidhiniwa anafikiri kwamba mlipa kodi huyo ana wajibu wa kulipa kodi kwa mwaka huo, anaweza kwa kadri atakavyoona, kuamua kiwango cha hesabu za mlipa kodi huyo, isipokuwa tathmini hiyo haitaathiri wajibu wowote wa mlipa kodi anayostahili kwa mujibu wa sheria Ndogo hizi, kwa kushindwa kwake kuwasilisha hesabu hizo.
- (4) Kodi iliyotathminiwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, italipwa katika siku thelathini tangu tarehe ya kufanya tathmini.

**Adhabu**

13. – (1) Mtu yeyote anayetakiwa kulipa kodi akishindwa kuwasilisha hesabu zake kama inavyotakiwa kwa mjibu wa Sheria Ndogo hizi katiia kipindi kilichoongezwa atatozwa riba ya asilimia 1.5 kwa mwezi au shilingi elfu hamsini kutegemea kiwango kipi kitakuwa kikubwa.
- (2) Iwapo mtu yeyote atasema uongo au ataficha baadhi ya hesabu zake kwa nia ya kupunguza kiwango cha kodi anachotakiwa kulipa, na inapobainika kuwa ufichaji au upunguzaji huo aliufanya kwa makusudi, mtu huyo atatozwa ushuru pamoja na nyongeza ya kodi ya asilimia hamsini (50%) ya tofauti kati ya kodi anayotakiwa kulipa na hesabu alizowasilisha pamoja na kiwango cha kodi halisi.

**Kufifisha  
kosa**

14. – (1) Kodi ambayo haijalipwa kwa wakati kama ilivyoelezwa kwenye Sheria ndogo hizi, itatozwa riba ya jumla ya asilimia 15% kwa mwezi na itatakiwa kulipwa pamoja na kodi inayodiawiwa.
- (2) Riba itozwayo katika Sheria ndogo hizi itachukuliwa kama kodi inayostahili kulipwa na njia zote na kukusanya kodi na madeni zitatumika kukusanya riba hiyo kama kodi inayolipwa na mlipa ushuru huo.
15. Mtu yeyote ambaye bila ya sababu ya msingi:-
- (a) atashindwa kuwasilisha sababu za msingi na za kweli;
  - (b) atashindwa kuwasilisha nyaraka, maelezo au taarifa inayotakiwa kuwasilishwa kwa Halmashauri katika muda uliowekwa;
  - (c) atashindwa kutunza kumbukumbu kitabu au hesabu;
  - (d) atashindwa kuonyesha kumbukumbu yoyote au nyaraka kwa ajili ya uchunguzi atakuwa ametenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizil
- (a) akifanya hesabu za uongo kwa kupunguza au kutoa hesabu zisizokuwa sahihi;
  - (b) akitoa taarifa isiyokuwa sahihi kuhusu jambo lolote linaloweza kuathiri jukumu lake au la mtu mwingine la kulipa ushuru.
  - (c) Akiandaa au kutengeneza au kusababisha kuandaliwa au kutengenezwa kwa vitabu vya uongozi vya mahesabu au kumbukumbu;
  - (d) Atamzuia au kujaribu kumzuia Afisa muidhiniwa kutekeleza majukumu

yake aliyopewa kwa mujibu wa Sheria ndogo hizi; Atakuwa ametenda kosa.

17. – (1) Mtu yeyote atakayevunja masharti ya Sheria Ndogo hizi, atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi hamsini elfu (50,000/=) au atatumikia kifungo cha miezi isiyozidi kumi nambili jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.
- (2) Pamoja na adhabu atakayopewa mkosaji katika Sheria Ndogo ya 17(1) atawajibika kulipa Halmashauri gharama iliyoingia kutokana na kuvunja Masharti ya Sheria ndogo hizi.
18. Enapo mtu ametenda kosa na kukiri kwa maandishi kwa mujibu wa Sheria ndogo hizi, Mkurugenzi anaweza kushughulikia kosa hilo na kuagiza kuwa mtu huyo alipe deni analodaiwa pamoja na adhabu ya kulipa faini isiyozidi shilingi hamsini elfu.

## **HATI YA KUKILI KOSA**

### **(Chini ya kifungu cha 13)**

Mimi.....nakiri mbele  
ya.....Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Kaliua  
kwamba mnamo tarehe .....ya mwezi .....mwaka.....nilitenda  
kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha .....cha Sheria Ndogo za (kodi  
ya huduma) za Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua ya mwaka 2014. Nipo tayari  
kulipa kiasi cha ada/au ushuru ninaodaiwa pamoja na faini ikiwa Mkurugenzi  
ataamua kutekeleza mmlaka aliyopewa chini ya Sheria Ndogo zilizotajwa hapo  
juu.  
Nathibitisha kwamba maelezo ya hapo juu ni kweli nimeyatoa kwa hiari yangu  
kadri ya ufahamu wangu.

Tarehe..... Saini.....

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua libandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano waHalmashauri uliofanyika tarehe .....Mwezi.....Mwaka 2014 na nembo hiyo ilibandikwa mbele ya:

.....  
*ABDALLAH S.NGODU*  
*Mkurugenzi Mtendaji Wilaya*  
*Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua*

.....  
*JOHN KADUTU,*  
*Mwenyekiti ,*  
*Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.*

*NIMEKUBALI.*

.....  
**MHE. MIZENGO P.PINDA (MB).**  
**WAZIRI MKUU**

Dodoma  
Tarehe.....2014.



TANGAZO LA SERIKALI Na. .... La tarehe .....

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(Sura ya 290)

**SHERIA NDOGO**

*Zimetugwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16 (1)*

**SHERIA NDOGO ZA( USHURU WA STENDI) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KALIUA, 2014.**

- |                         |   |
|-------------------------|---|
| Jina na kuanza kutumika | 1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za Ushuru wa Stendi za Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua, 2014, na zitaanza kutumia baada ya Kutangazwa katika Gazeti la Serikali. |
| Tafsiri                 | 2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.  |
|                         | 3. Katika Sheria Ndogo hizi, isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo  |
|                         | “ <i>Afisa aliyeidhinishwa</i> ” maana yake ni mtumishi wa Halmashauri ya Wilaya au mtu mwingine ambaye ameteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.              |
|                         | “ <i>Gari la Abiria</i> ” maana yake ni basi kubwa au dogo, au chombo chochote kinachotumia injini ambalo kwa kawaida husafirisha abiria;                                   |
|                         | “ <i>Gari la mizigo</i> ” maana yake ni lori, gari dogo, mkokoteni au aina nyingine yoyote ya gari linalotumika kubeba mizigo;  |
|                         | “Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua;  |
|                         | “ <i>Kituo cha mizigo</i> ” au kituo maalum cha kushusha na kupakia mizigo;   |
|                         | “ <i>Kupiga debe</i> ” maana yake ni kuita kwa sauti au kushawishi abiria wapande gari la abiria au la mizigo;  |
|                         | “ <i>Mkokoteni</i> ” maana yake ni nyenzo yoyote inayotumika kurahisisha ubebaji au uhamishaji wa vifurushi na mizigo;  |
|                         | “ <i>Mkurugenzi</i> ” maana yake ni Mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua, au Afisa mwingine wa Halmashauri aliyekaimishwa                                 |

madaraka hayo;

“*Stendi*” ni kituo maalum cha kushusha na kupandisha abiria;

“*Stendi kuu*” maana yake ni stendi kuu ya Halmashauri ya wilaya kaliua pamoja na stendi nyingine itakayotangazwa na Halmashauri kuwa stendi kuu;

“*Ushuru*” ni kiasi cha fedha taslimu kitakachotozwa kwa kila mwenye gari la abiria au la mizigo litakaloingia au kutoka katika eneo la Stendi

- Kuanzishwa stendi ya magari ya abiria.** 4. Kutaanzishwa stendi ya magari ya abiria, ambayo itatumika na kusimamiwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.
- Ushuru** 5. – (1) Kila mmiliki au dereva wa gari la abiria anayekusudia kutumia huduma ya Stendi kushusha au kupandisha abiria katika eneo la Halmashauri atalipa ushuru wa stendi kwa kiwango kilichotajwa katika nyongeza ya Sheria Ndogo hizi.
- Marufuku** 6. –(1) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote, dereva au mmiliki wa gari:-  
 (a) kushusha au kupandisha abiria katika eneo ambalo siyo stendi;  
 (b) kupiga debe katika eneo la stendi;  
 (c) kupanda na kushusha katika gari la abiria katika eneo ambalo siyo stendi.
- (3) Bila kuathiri masharti yanayotajwa katika fungu la (1) la Sheria Ndogo hizi, isipokuwa malipo ya kiwango cha ushuru kinachotajwa katika nyongeza ya Sheria Ndogo hizi, mtu anaweza kuruhusu abiria kupanda au kushuka kutoka gari katika eneo ambalo siyo stendi iwapo:-  
 (a) anamiliki eneo hilo;  
 (b) ameomba na kuruhusiwa na Halmashauri kutumia eneo hilo kwa shughuli hiyo kushusha au kupandisha abiria katika eneo hilo hakusababisha usumbufu kwa watumiaji wengine au wakazi wa jirani na eneo hilo.
- Jinsi ya kulipa ushuru** 7. – (1) Mmiliki wa gari la abiria au la mizigo anatakiwa kulipa ushuru wa standi kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali A la Sheria Ndogo hii.  
 (2) Kila mtu atakayeingia au kutoka ndani ya stendi ya Mabasi lazima alipe tsh 200/= isipokuwa kwa aliye na tiketi ya basi ya kusafiria.
- Ushuru wa kulaza magari** 8. Kutakuwa na ushuru wa kulaza magari katika eneo la Halmashauri kwa kuzingatia kiwango cha ushuru kinachotajwa katika jedwali A la Sheria Ndogo hii.
- Kuzuia na kukamata gari.** 9. – (1) Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kukamata na kuzuia gari lolote la mizigo au abiria ambalo halijalipiwa ushuru unaostahili.  
 (2) Gari lolote ambalo litakamatwa au kuzuiliwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizo zitahesabiwa kama lililotelekezwa, na Halmashauri itatoza shilingi elfu moja (1,000/=) kila baada ya Masaa kama gharama ya kutunza gari hilo.

- (3) Mmiliki ama mwangalizi wa gari ambalo litakamatwa au kuzuiliwa Chini ya sheria ndogo hii, asipolipia gharama zote na kuchukua gari lake kutoka mikononi mwa Halmashauri kwa zaidi ya siku tatu mfululizo atakuwa ametenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi.

**Ushuru wa  
mkokoteni**

10. Kila mkokoteni utakaolingia katika eneo la stendi utatozwa kiasi cha ushuru kinachotajwa katika nyuonjeza ya kwanza ya Sheria ndogo hizi.

**Kuosha na  
kufanya  
matengenezo  
ndani ya  
eneo la  
stendi**

11. Ni marufuku kuosha, kufanya matengenezo makubwa au madogo au kuhifadhi gari la mizigo, gari la abiria, baiskeli au mkokoteni ndani ya eneo la stendi.

**Muda wa  
kupakia na  
kushusha  
abiria  
stendi**

12. Shughuli zote za kupatika na kushushaabiria katika eneo la stendi au eneo lolote jingine ambalo limeruhusiwa kufanya shughuli ambazo kwa kawaida hufanyika stendi zitafanywa kati ya saa kumi na mbili (12.00) asubuhi na saa nne (4.00) usiku.

13. Ni marufuku kwa gari lolote la abiria au la mizigo kuendelea kuwepokatika eneo la stendi kwa zaidi ya masaa mawili.

**Kibao cha  
kuonyesha  
gari  
liendako.  
Matumizi  
ya stendi.**

14. Kila gari la abiria sharti litakuwa na kibao kinachoonyesha mahali ambako gari hilo linakwenda kutokea.

15. Kutakuwa na eneo maalum la kushushia abiria na eneo maalum la kushushia mizigo, na ni marufuku kwa gari lolote la abiria au la mizigo kupakia au kushusha katika eneo ambalo halikutengwa kwa ajili hiyo.

16. Katika eneo la stendi ni marufuku kwa mtu yeyote:-  
(a) kuuza vyakula au vinywaji isipokuwa kwa utaratibu maalum ambao utapangwa na Halmashauri.  
(b) kuuza bidhaa zozote za mikononi.  
(c) Kufanya shughuli za kupakua au kubeba mizigo isipokuwa kwa utaratibu maalumu utakaopangwa na kutangazwa na Halmashauri

**Makosa  
Na Adhabu.**

17. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi:-

- (a) iwapo kitendo chake kimesababisha ukosefu wa mapato kwa

Halmashauri.

- (b) endapo atasababisha uvunjifu au upotevu wa amani katika eneo la stendi.
- (c) Endapo atasababisha usumbufu kwa abiria;
- (d) Anakataa, atashawishi mtu au watu kukataa kulipa au kushindwa kulipa ushuru;
- (e) Endapo atamzuia mkusanya ushuru au afisa mwidhiniwa kufanya kazi yake; au
- (f) Atafanya kitendo chochote kinyumed cha Sheria Ndogo hizi.

**Adhabu**

- 18. Mtu yeyote atakayetenda kosa chini ya sheria Ndogo hizi Akipatikana na hatia atalipa faini isiyozidi shilingi laki tatu (3000,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili jela au vyote viwili faini na kifungo.
- 19. Inapotokea mtu ametenda kosa na kukiri kwa maandishi ndani ya kipindi cha masaa ishirini na nne (24) baada ya kosa kutendeka, Mkurugenzi anaweza kushughulikia kosa hilo kwa kuagiza kuwa mtu huyo alipe deni analodaiwa pamoja na faini isiyopungua shilingi elfu (20,000/=) na isiyozidi shilingi laki moja (100,000/=) kwa kosa hilo.

**JEDWALI A**

**USHURU WA KULAZA MAGARI NA KUINGIA STANDI YA MABASI**

Na	Aina ya gari	Kulaza Kituoni au sehemu iliyotengwa na Halmashauri	Ushuru wa Standi (Tsh)	muda
1	Basi kubwa	2000/=	3,000/=	Kwa siku
	(Abiria 45 na zaidi)	2000/=	2000/=	Kwa siku
3	Basi dogo (Chini ya Abiria 45 )	2000/=	2,000/=	Kwa siku
4	Taxi, Pick-up, Stasion wagon	1000/=	1000/=	Kwa siku
5	Malori	3,000/=	3000/=	Kwa siku
6	Kulaza gari kituoni	2000/=	-	Kwa siku
7	Pikipiki		500/=	Kwa siku
8	Matololi au mkokoteni	200	200	Kwa siku

## HATI YA KUKILI KOSA

### (Chini ya kifungu cha 13)

Mimi.....nakiri mbele  
ya.....Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Kaliua  
kwamba mnamo tarehe .....ya mwezi .....mwaka.....nilitenda  
kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha .....cha Sheria Ndogo za  
(ushuru wa Standi) za Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua ya mwaka 2014. Nipo  
tayari kulipa kiasi cha ada/au ushuru ninaodaiwa pamoja na faini ikiwa  
Mkurugenzi ataamua kutekeleza mmlaka aliyopewa chini ya Sheria Ndogo  
zilizotajwa hapo juu.

Nathibitisha kwamba maelezo ya hapo juu ni kweli nimeyatoa kwa hiari yangu  
kadri  
ya ufahamu wangu.

Tarehe.....

Saini.....

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua ilibandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufutia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe .....Mwezi.....Mwaka 2014 na nembo hiyo ilibandikwa mbele ya:

.....  
ABDALLAH S NGODU,  
*Mkurugenzi Mtendaji,*  
*Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua*

.....  
JOHN KADUTU,  
*Mwenyekiti,*  
*Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.*

NIMEKUBALI,

.....  
MHE. MIZENGO P.PINDA(MB)  
WAZIRI MKUU

Dodoma.  
Tarehe.....2014

TANGAZO LA SERIKALI Na. .... La tarehe .....

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(Sura ya 290)

**SHERIA NDOGO**

*Zimetugwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16 (1)*

**SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA VIBAO VYA MATANGANO YA  
BIASHARA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KALIUA 2014.**

**Jina na  
Mwanzo  
Wa  
kuanza  
Kutumika**

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ushuru wa Vibao vya matangazo ya Biashara) za halmashauri ya Wilaya ya Kaliua, 2013 itaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

**Matumizi**

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.

**Tafsiri**

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa kama itakapoelezwa vinginevyo:-

*“Afisa mwishiniwa”* maana yake ni pamoja na Afisa Biashara na Wilaya au wasaidizi wake, Mhandisi ujenzi wa Wilaya na Afisa mwingine yeyote atakayeteuliwa na Mkurugenzi kutekeleza Sheria ndogo hizi.

*“Halmashauri”* maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua;

*“Matangazo”* maana yake ni maandishi yoyote yaliyoandikwa au kubandikwa kwenye vibao, ukuta wa jingo au chombo chochote kwa ajili ya kutangaza biashara.

*“Mfanyabiashara”* maana yake ni mtu yeyote anayefanya biashara yoyote chini ya sheria ya leseni za biashara au sheria yoyote iliyoandikwa au Sheria Ndogo za halmashauri;

*“Mkurugenzi”* maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri na ni pamoja na Afisa yeyote wa Umma atakayeteuliwa kukasimia utekelezaji wa majukumu ya Mkurugenzi;



“Vibao vya matangazo” maana yake ni ubao, ukuta au mahali popote au chombo chochote ambacho kimewekewa tangazo la biashara.

- Ushuru** 4. Kutakuwa na Ushuru wa mbao za matangazo yatakayowekwa katika sehemu yoyote ya halmashauri kwa viwango vilivyoonyeshwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi isipokuwa kwa matangazo ya Serikali na Taasisi zake
- Majukumu ya mfanyabiashara** 5. – (1) Litakuwa ni jukumu la kila mfanyabiashara kuweka kibao cha tangazo kutangaza biashara yake.
- (2) Mfanyabiashara yeyote ambaye ameweka kibao cha matangazo ya biashara katika maeneo ya Halmashauri atatakiwa kulipia ada ya vibao vya matangazo.
6. – (1) Afisa Muidhiniwa anaweza kutoa taarifa ya maandishi kwa mfanyabiashara yeyote ambaye atashindwa kulipa ada ya vibao vya matangazo chini ya Sheria Ndogo hizi kumtaka alipe ada hiyo katika muda utakaoneshwa katika taarifa hiyo.
- (2) Endapo mfanyabiashara huyo atashindwa kulipa ada hiyo katika Muda uliotajwa katika taarifa. Afisa mwishiniwa anaweza kuondoa tangazo hilo na kudai gharama za kuondoa tangazo hilo kutoka kwa mfanyabiashara huyo.
- (3) Bila kuathiri masharti ya kifungu cha 1 na 2 hapo juu, Halmashauri inaweza kudai ushuru wa matangazo kwa njia ya Mahakama.
- Uwezo wa Kuingia Kwenye Jengo. Makosa na Adhabu** 7. Afisa Muidhiniwa anaweza kuingia katika jengo lolote wakati wa saa za kazi kufanya ukaguzi kuona utekelezaji wa Sheria ndogo hizi.
8. Mtu yeyote ambaye:-
- (a) ataweka vibao vya matangazo kwenye eneo la halmashauri bila kibali;
- (b) atashindwa au kukataa kulipa ada au ushuru wa mbao za matangazo.
- (c) Atamshawishi mtu yeyote au kundi la watu wasilipe ushuru;
- (d) Atamzuia afisa Muidhiniwa kutekeleza majukumu yake; atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyoziidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo kisichozidi miezi sita jela au

adhabu zote mbili pamoja yaani faini na kifungu.

### **JEDWALI**

Na. Aina ya Tangazo	Ushuru (Tsh) kwa mwaka
1. Ada ya Tangazo lenyewe	1,000/=
2. Matangazo yanayotoa mwanga mraba	8,000/= kwa kila mita moja ya mraba
3. Matangazo yasiyotoa mwanga mraba.	6,000/= kwa kila mita moja ya mraba.
4. Matangazo yanayotoa na yasiyotoa Mwanga yasiyofika mita moja ya mraba	4,000/=

### **HATI YA KUKILI KOSA**

**(Chini ya kifungu cha 13)**

Mimi.....nakiri mbele ya.....Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Kaliua kwamba mnamo tarehe .....ya mwezi .....mwaka.....nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha .....cha Sheria Ndogo za (ushuru wa vibao vya matangazo ya biashara) za Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua ya mwaka 2014. Nipo tayari kulipa kiasi cha ada/au ushuru ninaodaiwa pamoja na faini ikiwa Mkurugenzi ataamua kutekeleza mamlaka aliyopewa chini ya Sheria Ndogo zilizotajwa hapo juu.

Nathibitisha kwamba maelezo ya hapo juu ni kweli nimeyatoa kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu.

Tarehe.....  
Saini.....

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua libandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe .....Mwzi.....Mwaka 2014 na nembo hiyo ilibandikwa mbele ya:

.....  
ABDALLAH S NGODU,  
Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua

.....  
JOHN KADUTU,  
Mwenyekiti,  
Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.

NIMEKUBALI,

.....  
MHE. MIZENGO P.PINDA(MB)  
WAZIRI MKUU

Dodoma.  
Tarehe.....2014.

TANGAZO LA SERIKALI Na. ....La tarehe.....

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)

(SURA YA 287)

## SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya Kifungu cha 153*

SHERIA NDOGO ZA (HIFADHI YA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KALIUA ZA MWAKA, 2014

### SEHEMU YA KWANZA UTANGULIZI

- |                            |   |   |
|----------------------------|---|---|
| Jina na mwanzo wa kutumika | 1 | Sheria Ndogi hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Hifadhi ya Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua, 2014 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.  |
| Matumizi                   | 2 | Sheria Ndogo hizi zitatumika katika maeneo yoyote ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.   |
| Tafasiri                   | 3 | <p>Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:-<br/>“<i>Afisa Mwidhinishwa</i>” maana yake ni afisa Maliasili, Afisa Kilimo na Mifugo pamoja na Afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;<br/>“<i>Eneo la Hifadhi</i>” ni maeneo ya milima, maeneo ya vyanzo vya maji, hifadhi ya misitu, miteremko na maeneo mengine ambayo yatatangazwa na Halmashauri kuwa ni maeneo ya hifadhi;<br/>“<i>Halmashauri</i>” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua;<br/>“<i>Hifadhi ya Mazingira</i>” maana yake ni utunzaji endelevu wa ardhi; mimea, hewa, viumbe hai na visivyo hai na vyanzo vya maji vinavyozingatia masharti na maelekezo yatakayotolewa na Afisa Mwidhinishwa chini ya Sheria ya Ndogo chini ya Sheria Ndogo hizi au Sheria nyingine yoyote.<br/>“<i>Kiwanda</i>” maana yake ni jengo au kundi la majengo au eneo ambapo vitu vinatengenezwa;<br/>“<i>Kuvuna misitu</i>” maana yake ni pamoja na kufyeka, kukata au kung’oa misiti, visiki;<br/>“<i>Maeneo ya malisho</i>” maana yake ni pamoja na sehemu zote ambazo</p> |

zimetengwa na Halmashauri;

*“Maji”* kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi Mazingira Na. 20 ya Mwaka 2004 ni pamoja na maji ya kunywa, ya mito,, vijito, maji yanayotiririka, yaliyohifadhiwa, yaliyo katika visima, mabwawa, mifereji, madimbwi, maziwa, maji yaliyoko chini ya ardhi, na maji yaliyoko katika mkondo;

*“maji taka”* kama ilivyo katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 ni pamoja na taka zinazotokana na kinyesi, mkojo na jasho, uchafu wa majimaji kutoka majumbani, Taasisi, majengo ya biashara na viwandani;

*“Mazao ya Misitu”* maana yake kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Misitu Na. 14 ya mwaka 2002 chini ya kifungu Na. 2 ni kitu cho chote kinachopatikana au kuzalishwa kutokana na miti, mazao yanayoota au kupatikana msituni, ambayo ni pamoja na mianzi, magamba, mkaa, kuni, miti, fito, mbao, mbegu za miti, nta, asali, utaa, matunda, upapi, majani ya kulalia wanyama, majani, mizizi, gundi,, utomvu, maranda, matete, kamba, makuti (mawale), nyuzi za wanyama, mimea (miti) na kitu chochote chenye uhai au kisicho na uhai kitakachotangazwa katika gazeti la Serikali kuwa ni zao la msitu;

*“Mazingira”* kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 yanahusisha maumbile halisi ya wazungukao binadamu ikiwa ni pamoja na hewa, ardhi, maji, tabia nchi, sauti, mwanga, harufu, ladha, vijiumbe hali za kibiolojia za wanyama na mimea, rasilimali za kitamaduni na masuala ya uchumi jamii na inahusisha mazingira asilia na yaliyoundwa na binadamu na jinsi yanavyoingiliana;

*“Mfugaji”* maana yake ni mtu yeyote anayejishughulisha na ufugaji mifugo katika eneo la Halmashauri;

*“Mkurugenzi”* maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi pamoja na Afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

*“Mifugo”* maana yake ni mifugo yoyote inayofugwa na binadamu;

*“Misitu”* maana yake ni eneo la ardhi ambalo limefunikwa angalau kwa asilimia 10 ya miti, uoto wa asili au iliyopandwa, au asilimia 50 au zaidi ya vichaka na miti inayoota upya ambayo itajumuisha aina yote ya misitu ya hifadhi ambayo itatangazwa chini ya Sheria ya Misitu Na. 14 ya mwaka 2002 na mazao yote ya misitu ikijumuisha majani na nyasi ndani ya eneo la Halmashauri;

*“Taka”* kama ilivyo katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 maana yake ni kitu cho chote kimiminika, kigumu, gesi na mionzi, kinachotoa harufu mbaya, au kilichohifadhiwa katika mazingira ya hali ya ujazo, uozo au hali nyingine yo yote inayosababisha uharibifu wa mazingira, ambayo inajumuisha taka;

*“Taka Ngumu”* kama ilivyo katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 ni taka ambazo haziko katika

umajimaji kutoka majumbani. Katika majengo ya biashara, viwandani na kutoka katika shughuli za kilimo, pamoja na taka za vyakula, karatasi plastic au taka laini zinazotokana na ujenzi au ubomoaji majengo, utengenezaji bustani na shughuli za uchimbaji madini, mizoga ya wanyama na mabaki ya magari mabovu(scrap); “*Taka za Viwandani*” kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004, maana yake ni uchafu unaotokana na uzalishaji viwandani au uchafu usiotokana na uzalishaji viwandaji ambao ni chanzo cha nishati, maji, mimea iliyotiwa dawa, au mawasiliano, pamoja na taka nyingine ngumu kama zilivyotafsiriwa katika Sheria ya Mazingira 2004 sehemu ya IX.

“*Uchafu hatari*” kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 ni mabadiliko ya hali ya hewa ya moja kwa moja au yasiyo moja kwa moja, joto, kemikaji, biolojia, au zana za mionzi katika mazingira ambayo zana hizo zinafanyia kazi au kutoa harufu mbaya, mrundikano wa taka ambao unaathiri watumiaji, au unaosababisha hali ya hatari kwa afya ya jamii, usalama, au ustawi au hatari kwa wanyama, ndege, wanyamapori, samaki, au viumbe vyote vya baharini, mimea au kusababisha hali mbaya ya hewa, upungufu, au kizuizi ambacho ni sehemu katika sheria hizi.

“*Udongo*” kama ilivyo katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 maana yake ni pamoja na dunia, mchanga, miamba, miamba tope, madini, uoto wa mimea na wanyama iliyoko chini ya udongo pamoja na vumbi;

“*Vitu hatari*” maana yake kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004, ni kemikali yoyote, taka gesi, madawa, vidonge, mimea, wanyama au viumbe hai visivyoonekana ambavyo ni hatari kwa afya ya binadamu, maisha au mazingira;

“*Waziri*” maana yake ni Waziri wenye dhamana ya Serikali za Mitaa.

## **SEHEMU YA PILI MASHARTI YA UFUGAJI**

- |                   |   |   |
|-------------------|---|---|
| Wajibu wa mfugaji | 4 | <p>(1) Kila mfugaji chini ya Sheria Ndogo hizi:-</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>(a) atatakiwa kufuga idadi ya mifugo kama itakavyoamuriwa na Halmashauri;</li> <li>(b) atatakiwa kufuga na kulisha mifugo yake katika maeneo ya malisho yaliyopangwa na Halmashauri;</li> <li>(c) atatakiwa kupitisha mifugo yake katika njia (stock routes) zilizopangwa na kutengwa na Halmashauri;</li> <li>(d) atatakiwa kuwa na kadi ya mifugo itakayoonyesha idadi na aina ya mifugo aliyonayo;</li> <li>(e) atatakiwa kupeleka mifugo katika majosho kama</li> </ul> |
|-------------------|---|---|

atakavyoagizwa na Halmashauri;

- (f) atatakiwa kupeleka mifugo yake katika vituo vya chanjo kama itakavyoamuriwa na Halmashauri, na atalipia chanjo hiyo kama atatakiwa kufanya hivyo;
- (g) atatakiwa kuchangia gharama za ukarabati wa majosho kama sehemu ya mchango wake, pale itakapobidi kufanya hivyo, na kwa gharama itakayopendekezwa na Halmashauri;
- (h) atatakiwa kuchangia gharama za uboreshaji wa maeneo ya malisho yaliyotengwa na Halmashauri;
- (i) atatakiwa kuweka alama kwenye mifugo yake (Branding, ear tags) na katika viungo vya mifugo vinavyopendekezwa ili kutoharibu zao la ngozi;
- (j) atatakiwa kuhudhuria mafunzo ya ufugaji kama atakavyohitajiwa na Halmashauri;
- (k) kutokata miti kwa lengo la kufukuza mbug'o;

(2) Ni marufuku kwa mfugaji yeyote:-

- (a) Kuchunga, kulisha, au kunywesha maji mifugo katika maeneo yote ambayo hayakutengwa kwa ajili hiyo;
- (b) Kusafirisha mifugo kwa kuiswaga barabarani;
- (c) Kusafirisha au kuhamisha mifugo kutoka eneo moja hadi lingine bila kibali kutoka kwa Halmashauri;
- (d) Kibali cha kuingiza mifugo katika eneo la Halmashauri kitatolewa na Afisa Kilimo na Mifugo;
- (e) Kuuza au kununua mifugo katika maeneo ambayo siyo mnada, masoko au magulio ya mifugo yaliyoidhinishwa na Halmashauri;
- (f) Kufunga mifugo mingi katika eneo dogo la Halmashauri;
- (g) Ni marufuku kwa mfugaji yeyote kupitisha mifugo katika maeneo ambayo hayakuidhinishwa na Halmashauri kupitisha mifugo.

Kudhibiti  
Mifugo  
Inayozurura  
ovyoo

- 5 (1) Halmashauri itakamata mifugo au mfugo wowote utakaoonekana unazurura ovyo katika eneo la Halmashauri ambapo hapajaruhusiwa kuchungia mifugo;
- (2) Mfugo wowote utakaokamatwa utalipiwa faini kama itakavyoamuriwa na Halmashauri;
- (3) Endapo mwenye mifugo au mfugo hatatokea ndani ya siku saba (7) tangu kukamatwa kwa mifugo hiyo, Mkurugenzi wa Halmashauri atakuwa na haki ya kuuza kwa mnada mfugo au mifugo hiyo baada ya kupata idhini ya Mahakama;
- (4) Baada ya mauzo, Mkurugenzi atakata fedha za faini, gharama za mnada na gharama za ulinzi na fedha zitakazobaki atapewa mwenye mifugo na kama hataonekana ndani ya siku kumi na nne (14)

Halmashauri itarudisha fedha zake;

- (5) Endapo mwenye mifugo hiyo atakuwa na sababu za msingi za kutofika kwake katika muda wa siku kumi na nne (14) Halmashauri itarudisha fedha zake;
- (6) Endapo kutatokea kufa kwa mifugo au mfugo Halmashauri haitawajibika na ulipaji wa gharama zozote.

Ukaguzi  
wa Mifugo

- 6 (1) Itakuwa halali kwa Afisa Kilimo na Mifugo, Maafisa Watendaji wa kata na vijiji, na Afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi kuingia katika nyumba au jengo lo lote wakati wowote kwa madhumuni ya kukagua na kuhesabu idadi ya midugo iliyomo katika nyumba hiyo.
- (2) Mtu yeyote atakayewazuia Maafisa waidhinishwa katika kifungu cha 6(1) kutekeleza wajibu wao chini ya Sheria Ndogo hii atakuwa ametenda kosa

Wajibu wa  
Halmashauri

- 7 (1) Ni wajibu wa Halmashauri kutenga maeneo maalum kwa ajili ya shughuli za malishi kwa kuzingatia idadi ya mifugo ndani ya eneo la Halmashauri na kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Sura ya 113 na 114 pamoja na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004.
- (2) Halmashauri itatenga njia maalum ya kupitisha mifugo kwenda na kurudi malishoni au minadani
- (3) Halmashauri itafanya sensa ya mifugo na kutoa kadi za mifugo na elimu ya ufugaji bora kwa jamii.

Taratibu za  
Ufugaji

- 8 (1) Wafugaji wote watatakiwa kuzingatia masharti ya kufuga kama yalivyo katika Sheria Ndogo hizi au Sheria yoyote iliyotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
- (2) Kila mfugaji atatakiwa kupeleka mfugo au mifugo yake machinjioni au mahali huduma hiyo inapopatikana na itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuchinjia nyama mahali pengine popote.
- (3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kununua, kuuza au kufanya Biashara ya kubadilishana aina yoyote ya mifugo katika eneo lolote la Halmashauri isipokuwa kwenye minada au magulio yaliyotengwa kwa shughuli hiyo.



## SEHEMU YA TATU

### KILIMO NA UHIFADHI WA ARDHI

- Taratibu za kilimo 9 (1) Mtu atakayetaka kuendesha shughuli za kilimo katika Halmashauri atatakiwa kuzingatia taratibu za kilimo kama zitakavyotolewa na Halmashauri kwa kuzingatia Sheria ya Ardhi Sura ya 113 na 114 na Sheria nyingine zitakazotungwa na Bunge.
- (2) Itakuwa halali kwa Afisa Kilimo kuingia katika shamba lo lote kwa madhumuni ya kufanya ukaguzi na kuhakikisha utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.
- Marufuku 10 (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kulima katika miteremko, karibu na vyanzo vya maji, kandokando ya mito, mabwawa na maziwa au kufanya jambo lo lote litakaloharibu hifadhi ya mazingira bila kuzingatia ushauri wa Afisa Kilimo.
- (2) Ni marufuku kwa mtu yeyote kutumia kinyume ardhi iliyotengwa kwa matumizi ya kilimo kama ilivyopangwa na kuidhinishwa na Halmashauri
- (3) Ni marufuku kwa mtu ye yote kusafisha shamba kwa ajili ya kilimo kwa njia ya kuchoma moto isipokuwa kwa kibali maalum kutoka kwa Halmashauri.
- (4) Kibali kitakachotolewa chini ya Sheria Ndogo hizi kitakuwa cha maandishi na kitaonyesha jina la mwenye kibali, tarehe na eneo analotaka kuchoma moto.
- (5) Muda unaotakiwa kuchoma moto chini ya Sheria Ndogo hizi ni kuanzia saa 12:00 asubuhi hadi saa 4:00 asubuhi.
- (6) Ni wajibu wa Halmashauri kusimamia shughuli za kilimo na kuhakikisha kuwa wanazuia kilimo cha kuhamahama na kuhimiza kilimo cha mzunguko (crop rotation).
- Uhifadhi wa uoto wa Asili 11 Ni wajibu wa wakazi wa eneo ambalo uoto wa asili au mazingira ya eneo husika yameharibiwa, kuhakikisha kuwa wanalirudisha katika hali yake ya kawaida kwa kupanda miti au kutoendelea kuharibu mazingira na kuwezesha uoto urudi katika hali yake.

Uchimbaji Mchanga na kokoto	12	Ni marufuku kwa mtu yeyote kuchimba mchanga katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri kama vile katika maeneo ya makazi ya watu, maeneo yaliyohifadhiwa kando kando ya mito au ndani yam to, bwawa au ziwa isipokuwa kwa ruhusa maalum ya Halmashauri.
Marufuku	13	Ni marufuku kwa mtu yeyote kujenga nyumba au jengo lolote katika eneo la hifadhi.

### SEHEMU YA NNE:

#### HIFADHI YA VYANZO VYA MAJI

Wajibu wa kulinda vyanzo vya maji	14	(1) Halmashauri itawajibika kuanzisha, kusimamia na kulinda vyanzo vya maji. (2) Halmashauri itachukua hatua kali za kisheria dhidi ya mtu yeyote atakayeharibu chanzo cha maji au kushindwa kushiriki katika shughuli za kuhifadhi vyanzo vya maji bila sababu ya msingi.
Kulinda eneo la Hifadhi	15	(1) Ni marufuku kwa mtu ye yote kulima, kukata miti, kuchunga mifugo katika umbali wa mita 60 kutoka vyanzo vya maji au kufanya jambo lo lote linaloharibu kwa namna yo yote chanzo cha maji na hifadhi ya mazingira. (2) Itakuwa ni wajibu wa Halmashauri kupanda miti isiyonyonya maji katika vyanzo vya maji kwa kuzingatia maelekezo ya Afisa Misitu. (3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kumiliki eneo la chanzo cha maji isipokuwa Halmashauri.
Uchafuzi wa vyanzo vya Maji	16	(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote, kiwanda, taasisi, Shirika kuelekeza mabomba ya maji machafu kwenye mito, mabwawa, ziwa, visima, mifereji, chemchemi au sehemu yo yote ambayo ni chanzo cha maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu na wanyama au viumbe vingine vilivyo hai. (2) Ni marufuku mtu yeyote kuweka kitu cho chote chenye sumu ndani ya maji ambayo tyanatumiwa na binadamu au kiumbe cho chote hai.

### SEHEMU YA TANO

#### HIFADHI YA MISITU

Kuchoma au	17	(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuchoma moto misitu kwa namna
------------	----	--

- kusababisha Moto
- yoyote ile katika Misitu iliyoko eneo la Halmashauri.
- (2) Iwapo moto utatokea katika eneo la Halmashauri, Kiongozi wa eneo husika atawajibika kutoa ishara ya hatari kwa kutumia njia iliyo zoeleka kuamuru wakati wa eneo hilo kwenda kuzima moto huo unapoonekana kuwa na madhara kwa maisha, mali za wartu na uharibifu wa mazingira katika eneo hilo.
- (3) Kila mkazi wa eneo hilo atawajibika kushiriki katika zoezi la kuzima moto huo endapo atatakiwa kufanya hivyo, kama atashindwa kushiriki katika kuzima moto bila sababu ya msingi atakuwa ametenda kosa.
- Kibali cha kuchoma Moto 18 Mtu yeyote aliyepata kibali cha kuchoma moto atalazimika kutoa taarifa ya siku saba (7) kabla ya kuchoma moto kwa majirani walioko katika eneo analotaka kuchoma na ataweka njia za kuzuia moto.
- Ukataji Miti 19 (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kukata miti katika maeneo ya misitu iliyohifadhiwa kwa ajili ya matumizi ya aina yoyote bila kupata kibali kutoka Halmashauri.
- (2) Halmashauri itatakiwa kuhakiki kama miti inayovunwa imekomaa na inafaa kwa ajili ya matumizi.
- (3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuvuna miti katika msitu ambao umehifadhiwa kwa ajili ya viumbe maalum ambao ni rasilimali kwa Taifa.
- (4) Watu wanaovuna miti kwa ajili ya kuchoma mkaa watatakiwa kuwa na eneo maalum lililoidhinishwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchoma mkaa.
- Wajibu wa kupanda miti 20 (1) Kila mkazi wa Halmashauri atawajibika:-
- (a) Kupanda na kutunza miti katika eneo lake
- (b) Kupanda na kutunza miti katika makazi yake
- (c) Kupanda na kutunza miti katika shamba au mashamba anayomiliki
- 21 (1) Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kila kijiji:-
- (a) kitawajibika kutenga eneo la hifadhi ya Msitu wa asili kwa ajili ya matumizi ya baadaye;
- (b) Kitalazimika kutunza miti yote inayopandwa katika eneo la kijiji;

- (c) Kitahakikisha ya kuwa kila kaya inapanda miti isiyopungua kumi kwenye eneo la nyumba yake;
  - (d) Mtu yeyote anayetaka kukata miti au mti wa matumizi ya kuchonga vifaa, kujenga nyumba, kutengeneza zizi na shughuli nyinginezo, itabidi apate kibali cha maandishi toka kwa Mwenyekiti wa Kijiji, Mtendaji wa Kijiji na kibali cha Afisa Maliasili wa Wilaya au Wazaidizi wake kwa miti iliyopandwa na kuhifadhiwa na Halmashauri ya Wilaya au Wasaidizi wake kwa miti iliyopandwa na kuhifadhiwa na Halmashauri ya Wilaya;
  - (e) Kila kijiji kitapaswa kutenga na kupanda shamba la miti ekari 2 kila mwaka na kulitunza;
  - (f) Kila Shule au Taasisi nyingineyo Wilayani itapaswa kupanda miti ya kuinga upepo kuzunguka majengo yake na kuwa na shamba lisilopungua miti hekta 2;
  - (g) Kijiji kitapaswa kutunza na kuhifadhi miti na nyasi kwenye milima, makorongo na vyanzo vya maji ili kuzuia mmomonyoko wa udongo;
  - (h) Kijiji kitahakikisha kuwa kila anayeandaa shamba kwa ajili ya kilimo hatumii moto na anapanda miti kwenye mipaka ya shamba lake kama kinga upepo;
  - (i) Kila mtu mwenye nyumba kwenye Mji Mdogo atawajibika kupanda miti kando ya barabara inayopita mbele ya nyumba yake na kuitunza;
- (2) Kila mwenyekiti wa Kitongoji, Mtendaji wa Kijiji, Mkuu wa Taasisi yoyote Wilayani atahakikisha kuwa Kijiji au Taasisi ina msitu wa hifadhi wa miti ya kupandwa au ya asili iliyotengwa kwa madhumuni ya kuhifadhi ardhi, mazingira na matumizi ya baadaye.

## **SEHEMU YA SITA**

### **TAKA NGUMU NA LAINI**

- |                                |    |   |
|--------------------------------|----|---|
| Utupaji wa taka ngumu na laini | 22 | <ul style="list-style-type: none"> <li>(1) Ni wajibu wa Halmashauri kutenga eneo kwa ajili ya kutupa taka ngumu na laini na kusimamia kwa karibu usafi katika eneo lake.</li> <li>(2) Mtu yeyote atakayetupa ovyo taka ngumu au laini, au kujisaidia katika kingo za mabwawa au kwenye vyanzo vya maji vilivyoko katika Halmashauri atakuwa ametenda kosa.</li> </ul> |
| Uendeshaji wa Viwanda          | 23 | Ni marufuku kuendesha shughuli za karakana, mashine ya kusaga, kuranda mbao. Kukamua maji ya matunda kucheomelea vyuma au kuendesha shughuli yo yote inayozalisha uchafu ambao unaleta athari   |

kwa binadamu na viumbe wengi katika maeneo ya makazi ya watu bila kuzingatia taratibu za ujenzi.

## SEHEMU YA SABA

### MAKOSA NA ADHABU

- |                                   |    |  |
|-----------------------------------|----|--|
| Makosa yanayohusu Mifugo          | 24 | Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa ikiwa:-<br>(a) ataingiza mifugo katika eneo la Halmashauri bila kibali;<br>(b) atasafirisha mifugo bila kuwa na kibali<br>(c) atalisha mifugo katika maeneo yasiyoruhusiwa<br>(d) atafuga mifugo zaidi ya idadi iliyoruhusiwa<br>(e) Atavua samaki kwa kutumia sumu au nyavu zenye matundu madogo (kokoro).   |
| Makosa yanayohusu Kilimo          | 25 | Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kilimo, kuchimba mchanga, kokoto, madini katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri atakuwa ametenda kosa.  |
| Makosa yanayohusu hifadhi Ardhi   | 26 | Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kuhifadhi Ardhi atakuwa ametenda kosa.   |
| Makosa yanayohusu vyanzo vya Maji | 27 | (1) Mtu yeyote atakayeharibu vyanzo vya maji au kushindwa kushiriki katika shughuli za kuhifadhi vyanzo vya maji atakuwa ametenda kosa.<br><br>(2) Mtu yeyote atakayebainika kuwa ameweka sumu ya aina yoyote kwa namna yoyote ambayo inaathiri maisha ya binadamu na viumbe wengine ambao ni rasilimali ya Taifa atakuwa ametenda kosa.   |
| Makosa yanayohusu kuharibu Misitu | 28 | Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa ikiwa:-<br>(a) atachoma au kusababisha moto katika misitu bila kibali au,<br>(b) atashindwa kushiriki katika kuzima moto au<br>(c) atavuna mazao ya misitu katika misitu iliyohifadhiwa na isiyohifadhiwa bila kibali, au<br>(d) atachoma mkaa na kukata kuni bila kibali, au<br>(e) atafyeka nyasi, kung'oa vichaka na kung'oa visiki kwenye misitu bila kibali.<br>(f) Atachoma au kusababisha moto katika misitu bila kibali au,<br>(g) Atavuna mazao ya misitu katika misitu iliyohifadhiwa |

na isiyohifadhiwa bila kibali, au

- (h) Atachoma mkaa na kukata kuni bila kibali, au
- (i) Atafyeka nyasi, kung'oa vichaka na kung'oa visiki kwenye misitu bila kibali
- (j) Atachunga mifugo kwenye eneo lolote lililopandwa miti au iliyohifadhiwa kama bustani ya miti;
- (k) Atakata miti au kuchungia mifugo kwenye miti iliyopandwa kwa ajili ya kuzuia mmomonyoko wa udongo au kinga upepo,
- (l) Atabandua magome ya miti kwa ajili ya kutengeneza vilindo, mzinga na vitu vingine bila ya kuwa na kibali,
- (m) Atalima au kukata miti katika vyanzo vya maji, milima, kando ya njia, makorongo na sehemu nyingine zozote zinazohifadhiwa ili kupunguza mmomonyoko wa udongo.

Makosa yanayohusu taka ngumu na laini	29	Mtu yeyote atakayetupa ovyo taka ngumu au laini katika maeneo yoyote yasiyoruhusiwa na Sheria Ndogo hizi au Sheria nyingine yoyote iliyotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atakuwa ametenda kosa.
Makosa yanayohusu taka za majimaji	30	Mtu yeyote atakayetiririsha maji machafu yanayoleta madhara kwa binadamu na viumbe vingine hai atakuwa ametenda kosa.
Makosa yanayohusu viwanda	31	Mtu yeyote atakayeendesha shughuli za kiwanda au viwanda vidogo, karakana, mashine za kusaga na kukoboa nafaka mashine za kuranda mbao katika makazi ya watu bila kuzingatia taratibu za mipango miji atakuwa ametenda kosa.
Adhabu	32	(1) Mtu yeyote atakayevunja masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi laki tatu (300,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.  (2) Pamoja na adhabu iliyotolewa chini ya kifungu cha (1) mkosaji anaweza kuamriwa kuilipa Halmashauri gharama za uharibifu wowote aliosababisha.

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua ilibandikwa katika Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe.....mwezi.....mwaka 2014 na nembo hiyo ilibandikwa mbele ya;-

.....  
**ABDALLAH S.NGODU**  
*Mkurugenzi Mtendaji,*  
*Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.*

.....  
**JOHN KADUTU**  
*Mwenyekiti,*  
*Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.*

NIMEKUBALI.

.....  
**MHE.MIZENGO P.PINDA(MB)**  
**WAZIRI MKUU.**

Dodoma  
Tarehe.....2014.

TANGAZO LA SERIKALI Na.....La tarehe.....

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA 290)

SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16(1)*

**SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MADINI YA UJENZI) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KALIUA, 2014**

Jina na mwanzo wa kutumika	1	Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ushuru wa Madini ya Ujenzi) za Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua za Mwaka, 2014 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.
Eneo la matumizi	2	Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua .
	3	<p>Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakavyoelekezwa vinginevyo;</p> <p>“Afisa Muidhiniwa” maana yake ni afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;</p> <p>“Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua;</p> <p>“Madini” maana yake ni kifusi, udongo, mchanga, kokoto, na mawe yanayochimbwa katika eneo la Halmashauri.</p> <p>“Maeneo yasiyoidhinishwa” maana yake ni maeneo ya mito, madaraja, barabara, mashamba ya watu, mijini pamoja na maeneo mengine yanayofanana na hayo.</p> <p>“Mkurugenzi” maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.</p> <p>“Ushuru” maana yake ni malipo yanayolipwa na mnunuzi au</p>



mchimbaji wa madini.

“Wakala” maana yake ni mtu yeyote, kikundi cha watu, kampuni, taasisi, asasi iliyoteuliwa na Halmashauri kukusanya ushuru kwa niaba yake.

- |                      |   |  |
|----------------------|---|--|
| Ukaguzi              | 4 | <p>(1) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayekusudia kuanzisha machimbo katika eneo la Halmashauri kuhakikisha kwamba anatoa taarifa kwa Mkurugenzi ili eneo hilo likaguliwe kuhakikisha kwamba uchimbaji huo hautaenda kinyume na Sheria za Mazingira.</p> <p>(2) Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kukubali au kukataa eneo lolote kuwa au kutokuwa eneo la machimbo ya madini ya ujenzi.</p>  |
| Kibali cha uchimbaji | 5 | <p>(1) Mtu yeyote anayetaka kuchimba Madini ya Ujenzi katika eneo la Halmashauri atatakiwa kuomba na kupata kibali cha kuchimba madini kutoka Halmashauri.</p> <p>(2) Kibali kitakachotolewa chini ya Sheria Ndogo hizi kitaeleza aina ya madini yanayochimbwa na eneo litakalochimbwa madini hayo. Kibali kinachotolewa chini ya Sheria Ndogo hizi kitalipiwa ada ya shilingi elfu kumi tu (10,000/=)</p> <p>Halmashauri itakuwa na uwezo wa kufunga machimbo yoyote ya madini ya ujenzi kama itaona kufanya hivyo ni kwa maslahi ya umma.</p> <p>(3)</p>   |
| Ushuru               | 6 | <p>(1) Mtu yeyote atakayesafirisha Madini ya Ujenzi kutoka eneo yaliko chimbwa kwenda maeneo mengine atalipa ushuru kwa tripu kwa viwango vilivyooneshwa katika jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.</p> <p>(2) Ushuru huo utatozwa kwa mchimbaji au mnunuzi mara baada ya kununua madini kutoka kwa mchimbaji au kupakia madini hayo katika chombo ambacho atakitumia kwa ajili ya kusafirishia.</p> <p>(3) Ushuru wa Madini ya Ujenzi utatozwa katika eneo la machimbo, barabara zinazoelekea au kutoka maeneo ya machimbo au eneo lolote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri.</p> <p>(4) Mnunuzi yeyote atakayeshindwa kulipa Ushuru anaotakiwa kulipa atatakiwa kupakua Madini ya Ujenzi kutoka katika</p> |

chombo au kutochukua madini hayo mpaka hapo atakapolipa ushuru anaodaiwa.

Wajibu wa kulipa ushuru	7	(1) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayestahili kulipa Ushuru huo kama ilivyoelekezwa katika Sheria Ndogo hizi. (2) Halmashauri itakuwa na uwezo kumzuia dereva au gari lolote kujishughulisha na usafirishaji wa madini ikithibitika kwamba kuna ukiukwaji na uvunjaji wa Sheria Ndogo hizi.
Ushuru kulipwa kwa Halmashauri	8	(1) Ushuru wa madini utalipwa kwa Halmashauri au wakala ambaye atatoa stakabadhi kama kielelezo cha malipo hayo. (2) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu aliyelipa Ushuru kudai risiti na hautakuwa utetezi kwa mtu yeyote kudai kuwa amelipa ushuru lakini hakupewa risiti.
Kufunika magari	9	Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa gari au magari yanayobeba madini kuhakikisha kwamba gari au magari yake yamefunikwa ili kuzuia uharibifu na uchafuzi wa Mazingira.
Muda wa machimbo kwa wazi	10	Maeneo yote ya machimbo ya Madini ya Ujenzi yatafunguliwa kuanzia saa kumi mbili alfajiri na kufungwa saa kumi na mbili jioni.
Vituo vya ukaguzi	11	(1) Halmashauri itaanzisha vituo kwa ajili ya ukaguzi wa magari yanayobeba Madini ya Ujenzi katika barabara zinazoingia na kutoka machimboni. (2) Itakuwa ni wajibu wa kila dereva kusimama katika kituo cha ukaguzi wa madini na kuonyesha stakabadhi aliyolipia Ushuru na endapo hatakuwa na stakabadhi hiyo atatakiwa kulipa ushuru kwa viwango vilivyoainishwa na Sheria Ndogo hizi. (3) Chombo chochote kitakachokamatwa kwenye eneo la machimbo na dereva au mmiliki wake akakimbia au kutoroka hakitaruhusiwa kutoka mpaka dereva au mmiliki huyo atakapolipa faini ya shilingi elfu hamsini(50,000/=) au muhusika kufikishwa mahakamani.
Halmashauri kutowajibika kwa hasara	12	Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote atakayopata mnunuzi au muuzaji wa Madini ya Ujenzi wakati wa kukusanya ushuru.
Uwezo wa Afisa	13	Bila kuathiri masharti ya Sheria Ndogo hizi Afisa Muidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuingia katika eneo lolote

Muidhiniwa		yanapochimbwa Madini ya Ujenzi kwa ajili ya kukagua na kukusanya Ushuru.
Kufifilisha kosa	14	Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kumtoza faini mtu yeyote iwapo mkosaji atakiri kosa kwa maandishi kwa kujaza fomu maalum iliyoambatanishwa kwenye Jedwali la pili la Sheria Ndogo hizi na kuwa tayari kulipa Ushuru pamoja na faini anayodaiwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi
Makosa	15	Mtu yeyote ambaye; <ul style="list-style-type: none"> <li>(a) atakataa au kushindwa kutii agizo lolote atakalopewa na Afisa Muidhiniwa;</li> <li>(b) atamzuia Afisa Muidhiniwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.</li> <li>(c) atakataa au kujaribu kukataa kulipa ushuru;</li> <li>(d) atashawishi mtu au kundi la watu kukataa kulipa ushuru;</li> <li>(e) atakwepa au atajaribu kukwepa kulipa ushuru;</li> <li>(f) atachimba madini katika maeneo yasiyoidhinishwa;</li> <li>(g) atachimba shimo kubwa kwa ajili ya madini na kuliacha bila kupanda miti au mimea mara baada ya madini hayo kuisha.</li> <li>(h) atachimba madini katika eneo lisiloruhusiwa na Halmashauri hasa maeneo ya barabara na maeneo ya hifadhi.</li> </ul>
Adhabu	16	Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi laki tatu tu (300,000/=) au kifungo kisichozidi miezi sita jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

### JEDWALI LA KWANZA

(Chini ya kifungu cha 6 (1) cha Sheria Ndogo hizi)

Na.	Aina ya Madini	Tani	Shilingi
1.	Changarawe	7	5,000 kwa tripu
2.	Udongo (Claysoil) kwa ajili ya kutengeneza “Slavy” ya kutengeneza saruji au shughuli yoyote	7	3000 kwa tripu
3.	Kokoto	7	5,000 kwa tripu
4.	Mchanga	7	3000 kwa tripu
5.	Udongo kwa ajili ya kutengenezea tofal	7	3000 kwa tripu
6.	Kampuni kubwa zitalipa asilimia 0.3 ya fedha za mrahaba(madini ya kokoto).		

### JEDWALI LA PILI

#### FOMU YA KUFIFILISHA KOSA

(Chini ya kifungu cha 14 cha Sheria Ndogo hizi)

Mimi ..... wa  
S.L.B..... ninaefanya biashara ya  
..... katika eneo la  
..... lililopo ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi.  
Nakiri kuwa leo tarehe .....Nilikiuka kifungu cha  
.....cha Sheria Ndogo za (Ushuru wa Madini  
ya Ujenzi) za Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua za Mwaka ,2014. Kwa hiyo, kwa hiari  
yangu mwenyewe na bila kushawishiwa na mtu yeyote, nakubali kulipa kiasi cha ushuru  
ninachodaiwa pamoja na faini iliyoainishwa kwenye Sheria Ndogo hizi iwapo  
Mkurugenzi atatekeleza madaraka aliyopewa chini ya kifungu cha 14 cha Sheria Ndogo  
hizi.

Saini .....

Mbele yangu..... (jina)

Saini .....

Wadhifa .....

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua ilibandikwa katika Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe.....mwezi.....mwaka 2014 na nembo hiyo ilibandikwa mbele ya;-

.....  
**ABDALLAH S.NGODU**  
Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.

.....  
**JOHN KADUTU**  
Mwenyekiti,  
Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.

NIMEKUBALI.

.....  
**MHE.MIZENGO P.PINDA(MB)**  
WAZIRI MKUU.

Dodoma  
Tarehe.....2014.

TANGAZO LA SERIKALI Na. ....La tarehe .....

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA

(MAMLAKA ZA WILAYA)

(SURA YA 287)

SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya Kifungu cha 153*

SHERIA NDOGO ZA (UANZISHAJI WA BODI YA MFUKO WA ELIMU) ZA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA KALIUA ZA MWAKA, 2014

Jina mwanzo wa kutumika	na 1	Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Uanzishaji wa Bodi ya Mfuko wa Elimu) za Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua za mwaka 2014 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.
Matumizi	2	Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililoko chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.
Tafsiri	3	Katika Sheria Ndogo hizi, isipokuwa kama itaelezwa vingineyo:-  “Afisa Elimu wa Halmashauri” maana yake ni Mtumishi wa Umma ambaye ndiye Msimamizi Mkuu wa utoaji wa huduma za elimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua;  “Bodi” maana yake ni Bodi ya Mfuko wa Elimu ya Halmashauri ya Wilaya iliyoanzishwa chini ya Kifungu cha 4((1) cha Sheria Ndogo hizi;
Sura ya 287		“Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua;  “Kamati ya Huduma za Jamii ya Halmashauri” maana yake ni Kamati ambayo imeanzishwa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya);  “Kamati ya Utendaji ya Mfuko wa Elimu” maana yake ni Kamati iliyoteuliwa kwa mujibu wa kifungu cha 30 cha Sheria Ndogo hizi;

Sheria Na.  
19 ya mwaka  
1997

“Katibu Mtendaji” maana yake ni Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Elimu wa Halmashauri aliyejiririwa na Bodi ya Mfuko wa Elimu kwa mujibu wa Kifungu cha 22 cha Sheria Ndogo hizi;

“Mfuko wa Elimu” maana yake ni Mfuko wa Elimu ulioanzishwa kwenye Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

“Mkuu wa Wilaya” maana yake ni Mkuu wa Wilaya ya Kaliua aliyeteuliwa kwa mujibu wa Sheria ya Tawala za Mikoa ya mwaka 1997;

“Mkurugenzi” maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua pamoja na Afisa yoyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

Na 5/1992

“Timu ya uendeshaji ya Mfuko” maana yake ni Timu ya Wataalamu inayoshughulikia shughuli za kila siku za Mfuko;

“Viwango vya elimu” maana yake ni viwango vya elimu ya awali na Msingi, Elimu ya Sekondari na Ufundi vilivyowekwa kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Elimu na Mafunzo;

“Wadhifa kwenye Chama cha Siasa” maana yake ni kuwa na madaraka ya kuteuliwa au kuchaguliwa kwenye Chama cho chote cha Siasa kilichoandikishwa chini ya Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992.

Bodi

4

(1) Kutakuwa na Bodi itakayojulikana kama Bodi ya Mfuko wa Elimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.

Wajumbe wa  
Bodi

(2) Bodi itaundwa na Wajumbe wafuatao:-

- (i) Mwenyekiti ambaye atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa mwaka wa Mfuko kutoka miongoni mwa watu wenye uzoefu na masuala ya elimu;
- (ii) Katibu Tawala wa Wilaya ya Kaliua.
- (iii) Wawakilishi wawili watakaochaguliwa na Mkutano Mkuu ambapo mmoja kutoka miongoni mwa Wakuu wa Shule za Sekondari za Serikali katika Halmashauri;
- (iv) mwakilishi mmoja kutoka Wamiliki wa Shule za binafsi;
- (v) mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii wa

Baraza la Halmashauri;

(vi) wawakilishi wawili kutoka miongoni mwa walimu wakuu wa Shule za Msingi;

(vii) mwakilishi mmoja kutoka miongoni mwa makatibu tarafa.

(3) Bila kuathiri masharti ya Kifungu cha 4(2) cha Sheria Ndogo hizi Bodi pia itakuwa na Wataalam wafuatao:-

(i) Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri;

(ii) Afisa Elimu wa Halmashauri;

(iii) Mweka Hazina wa Halmashauri.

Ofisi ya Bodi	5	Ofisi za Bodi zitakuwa katika eneo la Halmashauri au sehemu nyingine kama Bodi itakavyoamua.
Bodi kualika watu wengine	6	Bodi inaweza kualika watu wengine kwenye vikao vyake kama kutakuwa na haja ya kufanya hivyo lakini hawatakuwa na haki ya kupiga kura.
Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Bodi	7	Mwenyekiti wa Bodi atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa mwaka wa Mfuko baada ya nafasi hiyo kutangazwa katika magazeti yanayosomwa katika eneo la Halmashauri.
Kipindi cha kushika madaraka	8	(1) Wajumbe wa Bodi watahika madaraka kwa kipindi cha miaka mitatu, lakini mjumbe anaweza kuchaguliwa tena na kuendelea kuwa madarakani kwa kipindi cha miaka mitatu.  (2) Ufikapo wakati wa Uchaguzi wa wajumbe wapya au baada ya kipindi cha muda wa Bodi kuisha, Mkurugenzi Mtendaji atatangaza nafasi wazi na watu wenye sifa hizo watajaza fomu maalum za maombi na kuzirejesha kwenye Halmashauri ndani ya kipindi kitakachowekwa.
Utaratibu wa kujaza nafasi wazi	9	(1) Pale ambapo nafasi katika Bodi zitakuwa wazi aidha kwa kifo, kujiuzulu, ugonjwa, au kwa sababu nyingine yoyote ile mjumbe mwingine atachaguliwa kujaza nafasi hiyo kwa kipindi kilichobaki.  (2) Hakuna uchaguzi utakaofanywa endapo kipindi kilichobaki ni chini ya miezi sita.  (3) Mjumbe atakayechaguliwa kutokana na Sheria Ndogo ya 9(1) hapo juu ataweza kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitatu.



Uteuzi wa mwisho wa Bodi kuthibitishwa na Baraza la Madiwani Uzinduzi wa Bodi	10	(1) Uteuzi wa wajumbe utathibitishwa na Baraza la Madiwani baada ya kupendekezwa na Kamati ya Utendaji ya Mfuko wa Elimu.
		(2) Bodi itazinduliwa rasmi kwa kushuhudiwa na Mkuu wa Wilaya baada ya kuidhinishwa na Baraza la madiwani.
Bodi kuvunjwa kwa kuzembea kazi	11	(1) Endapo Bodi itazembea kazi au itashindwa kutekeleza kazi zake, Halmashauri itaionya Bodi mara mbili kwa maandishi au kuivunja Bodi na kuandaa uchaguzi mpya ndani ya miezi miwili.
		(2) Endapo Bodi itavunjwa, wajumbe wote wa kuchaguliwa watapoteza nafasi zao na hawatachaguliwa tena kuwa wajumbe wa Bodi ya Mfuko wa Elimu
		(3) (3) Wakati Bodi imevunjwa, Timu ya Uendeshaji ya Mfuko wa Elimu itatekeleza majukumu ya Bodi hadi hapo Bodi mpya itakapochaguliwa.
Vikao vya Bodi	12	(1) Bodi itafanya vikao vyake vya kawaida kila baada ya miezi mitatu, na vikao vyote vya bodi vitaendeshwa na Mwenyekiti. Endapo Mwenyekiti hatakuwepo, Mjumbe mmoja atachaguliwa kutoka miongoni mwa wajumbe kuwa Mwenyekiti wa kikao.
		(2) Vikao vya dharura vitafanywa pale tu Mwenyekiti atakapoomba au kuombwa kufanya hivyo kwa maandishi na kupata idhini ya Wajumbe wasiopungua theluthi moja ya Wajumbe wote wanaopiga kura.
		(3) Mjumbe yeyote ambaye bila taarifa au sababu ya msingi atashindwa kuhudhuria vikao vitatu mfululizo vya Bodi atakuwa amepoteza sifa za kuendelea kuwa Mjumbe wa Bodi na nafasi yake itatangazwa kuwa wazi.
Kumbu-kumbu za mikutano ya Bodi	13	Bodi itahakikisha kumbukumbu za Mikutano yake yote zinaandikwa na kuhifadhiwa, pia kumbukumbu za kila mkutano zitathibitishwa na Bodi kwenye mkutano unaofuata na zitatiwa saini na Mwenyekiti wa mkutano pamoja na Katibu.
Akidi ya kikao uwezo wa	14	(1) Nusu ya Wajumbe wote ndiyo itakuwa akidi kamili katika Vikao vyote vya Bodi.

kuamua

- (2) Uamuzi wa Bodi utakuwa ni ule unaoungwa mkono na Wajumbe zaidi ya nusu ya Wajumbe kamili wa Bodi.
- (3) Wajumbe wa kuchaguliwa wa Bodi ndio watakaokuwa na uwezo wa kupiga kura na kupitisha uamuzi wa Bodi.
- (4) Wataalam na waalikwa hawatakuwa na haki ya kupiga kura.
- (5) Kila Mjumbe wa Bodi atakuwa na kura moja na iwapo itatokea kura kufungana Mwenyekiti wa Bodi atakuwa na kura ya ziada mbali na kura yake ya kawaida.

Sifa za kuwa 15  
mjumbe wa  
Bodi

- (1) Mtu anaweza kushika nafasi ya ujumbe wa Bodi kama atakuwa na sifa zifuatazo:-
  - (a) awe raia wa Tanzania;
  - (b) awe na umri usiopungua miaka ishiriki na mitano na asizidi miaka sabini;
  - (c) awe na akili timamu;
  - (d) awe na Elimu ya Sekondari, yaani kidato cha nne na kuendelea, isipokuwa endapo hakuna mtu mwenye elimu ya Sekondari basi Halmashauri itatoa idhini ya kuajiri bila kujali elimu yake, na
  - (e) asiwe na madaraka yoyote kwenye chama cha siasa.
- (2) Mfanyakazi wa Halmashauri hataruhusiwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi.

Majukumu 16  
ya kazi za  
Bodi

Majukumu na kazi za Bodi zitakuwa kama ifuatavyo:-

- (a) kubuni Mipango na Mikakati kwa ajili ya maendeleo ya elimu katika Halmashauri;
- (b) kusimamia mgawanyo wa misaada ya fedha kwa Shule kufuatana na Bajeti iliyoidhinishwa na Mkutano Mkuu wa mwaka wa bodi;
- (c) kusimamia utekelezaji na kutathmini Mipango ya Elimu katika Halmashauri;
- (d) kujadili na kurekebisha Mipango na Bajeti ya elimu na kuiwasilisha kwenye Mkutano Mkuu a mwaka wa utendaji

kwa ajili ya kuidhinishwa;

- (e) kupokea, kuchambua na kuidhinisha taarifa za utekelezaji wa Mfuko wa Elimu wa Halmashauri;
- (f) kubuni vyanzo mbalimbali vya mapato na rasilimali za kutosha kuendesha Mfuko wa Elimu wa Halmashauri;
- (g) kushirikiana na Kamati ya Huduma za Jamii ya Halmashauri;
- (h) kuratibu na kusimamia shughuli za maendeleo ya Elimu katika Halmashauri kulingana na programu za kitaifa;
- (i) kupitisha Kanuni za Utengaji na Utumiaji wa Fedha kutoka kwenye Mfuko kwa ajili ya kuendeleza madhumuni ya Mfuko;
- (j) kusimamia Ujenzi wa Shule za Sekondari katika Halmashauri;
- (k) kufanya jambo lolote litakalofanikisha maendeleo ya Elimu katika Halmashauri.

Mamlaka ya 17  
Bodi

Bodi itakuwa na mamlaka yafuatayo:-

- (a) kusimamia mgawanyo wa fedha zinazolingizwa kwenye Mfuko wa Elimu wa Halmashauri;
- (b) kuajiri na kuachisha kazi watumishi wa Bodi.

Maagizo na 18  
maelekezo

Maagizo, maelekezo, taarifa au hati nyingine zilizotengenezwa au kutolewa kwa niaba ya Bodi zitatiwa saina na:-

- (a) Mwenyekiti wa Bodi au;
- (b) katibu Mtendaji au Afisa mwingine ye yote aliyeidhinishwa kwa maandishi na Katibu Mtendaji wa Bodi kwa ajili hiyo.

Uhusiano wa 19  
Bodi na  
Wadau na  
Mamlaka  
nyingine

(1) Uhusiano wa bodi na Jamii, wadau na mamlaka nyingine utakuwa kama ifuatavyo:-

- (a) Bodi itahakikisha kuwa jamii inashirikishwa kikamilifu katika kutambua matatizo, kuweka kipaumbele, kupanga, kuchangia, kufuatilia na

kutathmini utoaji wa huduma za elimu;

(b) Bodi itawajibika mbele ya Halmashauri ambapo mipango ya elimu ya robo mwaka na mwaka pamoja na taarifa za kiutaalam za fedha zinapitiwa na Kamati ya Huduma za Jamii na Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango na baadaye kuthibitishwa na Baraza la Halmashauri;

(c) Bodi itaendesha shughuli zake kwa utaratibu wa uwazi na ambao utakuwa na ufanisi wa Halmashauri na vyombo vyake vingine vya utendaji bila ya Halmashauri kuingilia uhuru wa Bodi.

(2) Bila ya kuathiri maelezo yaliyomo katika Sheria Ndogo ya (1) ya Sheria Ndogo hizi Bodi inaweza kukasimu baadhi ya madaraka yake pale inapoona inafaa.

Kamati ya 20  
Huduma za  
Jamii ya  
Halmashauri

Kamati ya Huduma za Jamii ya Halmashauri itafanya kazi zifuatazo:-

- (a) itapokea Mipango yote ya Maendeleo ya Mfuko;
- (b) itapokea taarifa za Ukaguzi wa Hesabu za Mfuko na kupitia hoja za Ukaguzi na baadaye kuziwasi lisha kwenye Halmashauri ambayo itaijadili na kuiwasilisha kwa Mkuu wa Wilaya.

Jukumu 21  
Wizara na  
Mamlaka ya  
Elimu

Jukumu la Wizara zinazoshughulikia Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Elimu pamoja na Mamlaka ya Elimu itakuwa ni kuandaa Sera, kupanga viwango, kufuatilia na kusimamia shughuli za Bodi kwa mujibu wa Sheria zilizopo.

Katibu 22  
Mtendaji

Bodi kwa idhini ya Mkutano Mkuu wa mwaka, itamteua Katibu Mtendaji wa Mfuko wa Elimu wa Halmashauri.

Uteuzi wa 23  
Katibu  
Mtendaji

- (1) Nafasi ya Katibu Mtendaji itatangazwa katika magazeti yanayosomwa zaidi nchini na Bodi itamteua mtu ambaye atakidhi vigezo vya uteuzi na ambaye atakuwa na sifa zinazofaa.
- (2) Bodi itaamua sifa za watu ambao wataomba nafasi ya Katibu Mtendaji.
- (3) Katibu Mtendaji atakuwa na muda maalum wa kushika madaraka

kama itakavyopangwa na Bodi.

Isipokuwa tu kwamba kipindi kimoja cha madaraka kisizidi miaka mitatu na mtu aliyeko madarakani anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitatu.

Kazi za 24  
Katibu  
Mtendaji

Kazi za Katibu Mtendaji wa Bodi zitakuwa:-

- (a) kuwa Mtendaji Mkuu wa shughuli zote za Mfuko na Katibu wa Vikao vyote vya Bodi;
- (b) kuongoza, kupanga na kuratibu utendaji wa shughuli za Mfuko;
- (c) kubuni, kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Mfuko;
- (d) kubuni na kushauri vyanzo mbalimbali vya mapato vya Mfuko wa Elimu wa Halmashauri;
- (e) kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Elimu wa Halmashauri;
- (f) kubuni na kushauri mbinu mbalimbali za kukuza na kuendeleza Mfuko wa Elimu wa Halmashauri.

Vyanzo vya 25  
Mapato

Vyanzo vya mapato ya Mfuko wa Elimu vitakuwa kama ifuatavyo:-

- (a) michango ya kila mwaka ya kila Mwananchi mwenye uwezo wa kufanya kazi anayeishi katika eneo la Halmashauri kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi;
- (b) ruzuku mbalimbali;
- (c) misaada mbalimbali kutoka Nchi mbalimbali, taasisi za kimataifa na kitaifa, Mashirika ya watu binafsi na kiseikali, Makampuni binafsi, na madhehebu ya Dini;
- (d) mikopo; na
- (e) vyanzo vingine halali vya mapato.

Fedha za 26  
Mifuko

Fedha zote zitakazokusanywa kama fedha za Elimu zitalipwa kwenye akaunti za Benki kama bodi itakavyoona inafaa au

kulipwa kwenye Akaunti Akaunti maalum ya Mfuko wa Elimu		kuagiza.
	27	<p>(1) Kutakuwa na Akaunti Maalum ya Mfuko wa Elimu wa Halmashauri ambapo fedha zote zitawekwa na kutunzwa;</p> <p>(2) Wawekaji saini wa akaunti ya Mfuko wa Elimu pamoja na taratibu nyignine za Mfuko huo zitakuwa kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Mfuko wa Elimu Namba 8 ya mwaka 2001;</p> <p>(3) Bodi itaajiri Mweka Hazina atakayesimamia Akaunti za Mfuko wa Elimu na kutunza mahesabu yote ya mapato na matumizi.</p>
Matumizi ya Fedha	28	Fedha zitakazowekwa kwenye Mfuko wa Elimu zitatumika kwa madhumuni ya kuendeleza, kukuza na kuboresha Elimu kama itakavyokuwa katika Mpango wa Maendeleo ya Elimu wa Halmashauri.
Bodi kuidhinisha malipo	29	<p>Bodi inaweza kuidhinisha malipo ya fedha kutoka kwenye Mfuko kwa madhumuni ya kulipia gharama za:-</p> <p>(a) ujenzi wa Shule za Sekondari na Msingi katika Halmashauri;</p> <p>(b) uendeshaji wa bodi na Kamati ya Utendaji;</p> <p>(c) miradi na programu zinazogharimiwa na Mfuko;</p> <p>(d) udhamini wa masomo kwa wanafunzi yatima na wale wasio na uwezo wa kulipia masomo yao;</p> <p>(e) shughuli nyingine yoyote au zozote ambazo kwa maoni ya Bodi zina manufaa kulingana na malengo na madhumuni ya Mfuko.</p>
Kamati Tendaji	30	<p>(1) Kutakuwa na kamati ya Utendaji ya Mfuko wa Elimu wa Bodi.</p> <p>(2) Kamati Tendaji itakuwa na Wajumbe wafuatao:-</p> <p>(a) mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri ambaye atakuwa Mwenyekiti;</p> <p>(b) katibu Mtendaji wa bodi ambaye atakuwa Katibu;</p> <p>(c) afisa Elimu wa Halmashauri ambaye atakuwa Mjumbe;</p> <p>(d) mweka Hazina wa Halmashauri ambaye atakuwa Mjumbe</p>

(e) Mchumi wa Halmashauri ambaye atakuwa Mjumbe.

Kazi za Kamati tendaji 31

Kazi za Kamati Tendaji zitakuwa kama ifuatavyo:-

- (a) kuandaa mipango kabambe ya elimu ya Halmashauri ambayo itatilia mkazo mahitaji yote ya Elimu ya Halmashauri kwa kuzingatia Mwongozo wa Kitaifa wa Mpango wa Elimu;
- (b) kuwezesha na kuratibu Vikao vya Bodi ya Mfuko wa Elimu pamoja na Mkutano Mkuu wa mwaka;
- (c) kuchambua na kubainisha maeneo ya kipaumbele kwa masuala ya elimu katika Halmashauri;
- (d) kuweka taratibu na vigezo vya ufadhili wa wanafunzi na utoaji ruzuku kwa miradi ya Elimu katika Halmashauri;
- (e) kuandaa taarifa za utekelezaji za Mfuko wa Elimu na maendeleo ya elimu katika Halmashauri.

Mkutano Mkuu wa mwaka 32

Kutakuwa na Mkutano Mkuu wa mwaka wa Mfuko wa Elimu utakaokuwa na wajumbe wafuatao:-

- (a) wajumbe wote wa bodi ya Mfuko wa Elimu
- (b) kamati Tendaji ya Mfuko wa Elimu
- (c) wawakilishi toka madhehebu ya Dini;
- (d) wajumbe wa kamati ya Huduma za Jamii.

Majukumu ya Mkutano Mkuu 33

Bila kuathiri uwezo wa Bodi, Mkutano Mkuu wa mwaka kitakuwa ndicho chombo cha:-

- (a) kupokea taarifa za Ukaguzi wa Mahesabu na Utendaji wa Mfuko za mwaka;
- (b) kumteua Mwenyekiti wa Bodi na Wakaguzi wa Hesabu za Mfuko;
- (c) kuchagua wawakilishi wawili wa Bodi kutoka miongoni mwa Wadau wa Elimu.

Taarifa za mapato na matumizi 34

Katibu Mtendaji atatarisha na kuwasilisha kwenye Bodi kila miezi mitatu taarifa iliyo na:-

- (a) viashiria vya utendaji na taarifa nyingine zinazohusiana na shughuli za Bodi;
- (b) kazi zilizofanyika na mafanikio yaliyopatikana;
- (c) taarifa nyingine kwa kadri Bodi itakavyoona inafaa.

- Taarifa za 35 (1) Katibu Mtendaji atatumza hesabu na kumbukumbu za shughuli ukaguzi wa zake, na atahakikisha kuwa fedha zote zilizopokelewa zinaingizwa Hesabu za kwenye Akaunti na kwamba malipo yote kutoka kwenye Mfuko yanafanywa kwa usahihi baada ya kuidhinishwa na ataweka udhibiti wa kutosha wa mali zake pamoja na madeni.
- Sheria Na. (2) Hesabu za mwaka za Mfuko wa Elimu wa Halmashauri 33 ya mwaka zitakaguliwa na Mkaguzi na mtaalamu mwenye sifa ya ukaguzi 1972 aliyesajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi ya mwaka 1972 na ambaye ameteuliwa na Mkutano Mkuu.
- (3) Ndani ya kipindi cha miezi sita baada ya mwisho wa kila mwaka wa fedha Bodi itatayarisha na kuwasilisha kwa Halmashauri Taarifa ya Fedha ya mwaka huo ambayo itajumuisha:-
- (a) taarifa za Fedha
  - (b) viashiria vya utendaji na taarifa nyingine zinazohusiana nazo;
  - (c) taarifa ya utekelezaji Mfuko wa Elimu wa Halmashauri.
- Mkuu wa 36 Mkuu wa Wilaya atawasilisha nakala ya Taarifa ya kila mwaka Wilaya kuwasilisha kwenye Mkutano Mkuu wa mwaka wa Mfuko. Taarifa ya mwaka
- Bodi kuwa 37 Bodi itakuwa na madaraka kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa na uwezo wa kukagua hesabu za Mfuko wa Elimu.
- Adhabu 38 Mtu yeyote ambaye:-
- (a) atakwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi au;
  - (b) atakayefanya kitendo cho chote ambacho kitazuia Bodi au Kamati Tendaji kufanya kazi zake kwa ufanisi, au;
  - (c) atatumia vibaya mali na rasilimali za Mfuko wa Elimu na kusababisha kutofikiwa kwa malengo yaliyowekwa, au;
  - (d) kwa uzembe atashindwa kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atalipa faini isiyozidi shilingi laki tatu (300,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote faini na kifungo kwa pamoja.



## JEDWALI

### A. WAFANYABIASHARA

### Kiasi kwa Mwaka

(i)	Maduka ya Jumla	20,000/=
(ii)	Maduka ya rejareja	5,000/=
(iii)	Migahawa	5,000/=
(iv)	Maduka ya vifaa vya Ujenzi	20,000/=
(v)	Nyumba za kulala wageni	10,000/=
(vi)	Viosk	5,000/=
(vii)	Bar	10,000/=
(viii)	Wauza mitumba	5,000/=
(ix)	Stationaries	10,000/=
(x)	Vituo vya Mafuta (Petrol Station)	50,000/=
(xi)	Magari ya Biashara	
	(a) Magari ya kusafirisha abiria	
	(i) Mabasi Makubwa	20,000/=
	(ii) Mabasi Madogo	10,000/=
	(b) Malori ya Mizigo	10,000/=
	(c) Teksi	5,000/=
	(d) Pick-up	5,000/=

### B: WATUMISHI

(i)	Serikali za Mitaa	10,000/=
(ii)	Serikali Kuu	10,000/=
(iii)	Mashirika ya kidini	20,000/=
(iv)	Wakuu wa Idara za Serikali na Taasisi	25,000/=
(v)	Mashirika binafsi	30,000/=

### C: WAKAZI:

Mkazi mwenye umri wa miaka 18 na  
kuendelea

5,000/=

**D: TAASISI:**

(i)	Wazabuni	30,000/=
(ii)	Mwakala	30,000/=
(iii)	Wanunuzi wa mazao	30,000/=
(iv)	Benki	50,000/=
(v)	Taasisi zingine ambazo hazijatajwa	25,000/=

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua ilibandikwa katika Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe.....mwezi.....mwaka 2014 na nembo hiyo ilibandikwa mbele ya;-

.....  
**ABDALLAH S.NGODU**  
Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.

.....  
**JOHN KADUTU**  
Mwenyekiti,  
Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.

NIMEKUBALI.

.....  
**MHE.MIZENGO P.PINDA(MB)**  
WAZIRI MKUU.

Dodoma  
Tarehe.....2014

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA(MAMLAKA ZA WILAYA)

(SURA YA 287 )

SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya kifungu cha 153.*

**SHERIA NDOGO ZA (UTUNZAJI WA BARABARA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KALIUA 2014**

- |                           |   |
|---------------------------|---|
| Jina na mwazo wa kutumika | 1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Utunzaji wa Barabara) za Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua za mwaka 2014 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali   |
| Eneo la matumizi          | 2. Sheria Ndogo hizi zitaanza kutumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.   |
| Tafsiri                   | 3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo;<br>"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.<br>'Barabara' maana yake ni barabara zote zinazopitika kwa magari katika eneo lote la Halmashauri;<br>'Mkurugenzi' maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri pamoja na Afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.                        |
| Wajibu wa Halmashauri     | 4. Halmashauri itakuwa na wajibu wa kuhakikisha kwamba;<br>(a) Barabara zote zilizo kwenye eneo lake zinapitika kwa kipindi cha mwaka mzima.<br>(b) Magari yanayopita katika barabara hizo ni yale yanayokubalika kulingana na uzito unaotakiwa;<br>(c) Itatengwa njia maalumu ya kupitisha mifugo(cattle track) wakati wa kwenda na kurudi malishoni na minadani au mahali pengine;<br>(d) Inaendeleza na kutunza barabara zote kwa kuzifanyia ukarabati wa mara kwa mara; |

5. Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayetumia barabara kuhakikisha kwamba;
- (a) Wanaangalia na kufuata alama za barabara;
  - (b) Wanazingatia takataka kwenye maeneo ya barabara.
- Ukaguzi
6. Afisa Muidhiniwa atakuwa na wajibu wa kukagua uzito wa magari yanayopita katika maeneo ya Halmashauri.
- Hifadhi ya barabara
7. Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuendesha shughuli yoyote itakayosababisha uharibifu wa ndani ya ;-
- (a) Upana wa mita therathini, kutoka katikati ya barabara ni mita kumi na tano kwa kila upande kwa barabara za Halmashauri; na
  - (b) Upana wa mita ishirini na tano , kutoka katikati ya barabara ni mita kumi na mbili na nusu kwa kila upande kwa barabara ya jumuiya.
- Makosa
8. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo;-
- (a) Atapitisha gari lenye uzito au mzigo unaozidi tani kumi kwenye barabara za Halmashauri
  - (b) Atakaelekeza maji machafu au kutupa takataka kwenye barabara;
  - (c) Atafanya shughuli yeyote ya binadamu pembeni ya barabara;
  - (d) Ataangusha miti na kuacha majani barabarani, kuweka magogo;
  - (e) Atatelekeza gari bovu barabarani bila alama za tahadhari.
  - (f) Atachimba au kukata barabara kwa kutengeneza mifereji.
- Adhabu
9. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na mashauri ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatika na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini (50,000) au kifungo kisichopungua miezi mitatu jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungu.

## HATI YA KUKILI KOSA

(Chini ya kifungu cha 10)

Mimi.....nakiri mbele  
ya.....Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Kaliua  
kwamba mnamo tarehe .....ya mwezi .....mwaka.....nilitenda  
kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha .....cha Sheria Ndogo za  
(Utunzaji wa Barabara) za Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua ya mwaka 2014.  
Nipo tayari kulipa kiasi cha ada/au ushuru ninaodaiwa pamoja na faini ikiwa  
Mkurugenzi ataamua kutekeleza mamlaka aliyopewa chini ya Sheria Ndogo  
zilizotajwa hapo juu.  
Nathibitisha kwamba maelezo ya hapo juu ni kweli nimeyatoa kwa hiari yangu  
kadriya ufahamu wangu.

Tarehe.....

Saini.....

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua libandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe .....Mwezi.....mwaka 2014 na nembo hiyo ilibandikwa mbele ya:

.....  
ABDALLAH S.NGODU,  
Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua

NIMEKUBALI,

.....  
JOHN KADUTU,  
Mwenyekiti,  
Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua

.....  
MHE. MIZENGO P. PINDA(MB)  
WAZIRI MKUU

Dodoma,  
Tarehe.....2014.

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA  
(Sura ya 290)

**SHERIA NDOGO**

*Zimetugwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16 (1)*

**SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MAZAO YA MISITU) ZA HALMASHAURI YA  
WILAYA YA KALIUA ZA MWAKA 2014.**

- |                            |    |  |
|----------------------------|----|--|
| Jina na mwanzo wa kutumika | 1. | Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ushuru wa Mazao ya Misitu) za Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua za Mwaka, 2014 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali   |
| Eneo la matumizi           | 2. | Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua  |
| Tafsiri                    | 3. | <p>Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo, maneno yafuatayo yatakuwa na maana hizi zifuatazo:</p> <p>“<i>Afisa mwidhiniwa</i>” maana yake ni afisa aliyeteuliwa na halmashauri kwa madhumuni ya kusimamia Sheria Ndogo hizi.</p> <p>“<i>Afisa mwidhinishwa</i>” maana yake ni afisa maliasili pamoja na afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.</p> <p>“<i>Chanzo cha maji</i>” maana yake ni chemchem, mito, vijito ,bwawa, ziwa, kisima au tetema,</p> <p>“<i>Eneo lililokatazwa</i>” maana yake ni eneo lenye upana wa mita sitini katika kila upande wa ukingo wa mto au kijito au chemchem au vijito au korongo au chanzo cha mto au chanzo cha kijito au vijito.</p> <p>“<i>Eneo lililotengwa</i>” maana yake ni eneo ambalo shughuli za kilimo au mifugo zitafanyika kwa kufuata masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hizi na ni</p> |



pamoja na eneo lolote ambalo ni mwinuko, au mteremko au bonde.

*“Eneo lililohifadhiwa”* maana yake ni eneo lililotengwa au lililokatanzwa kwa madhumuni ya kuhifadhi misitu au kuhifadhi ardhi au milima au mteremko ya milima au vilima au makorongo au kuhifadhi chanzo au vyanzo cha maji;

*“Halmashauri”* maana yake ni Halmashauri ya wilaya Kaliua.

*“Kibali”* maana yake ni idhini ya maandishi inayotolewa na Halmashauri kufanya shughuli inayohusiana na misitu au mazingira.

*“Kitongoji”* maana yake ni sehemu ya kijiji iliyosajiliwa na Halmashauri.

*“Miteremko”* maana yake ni mteremko au miteremko yoyote ya milima au vilima ambavyo mwinuko wake hauzidi nyuzi ishirini;

*“Mazingira”* kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya usimamizi wa Mazingira no 20 ya mwaka 2004 yanahusisha maumbile halisi yawazungukao binadamu ikiwa ni pamoja na hewa, ardhi, maji, tabia nchi, sauti, mwanga, harufu, ladha, vijiumbe hali za kibiolojia za wanyama na mimea, rasilimali za Kitamaduni na mausala ya uchumi jamii na inahusisha mazingira asilia na yaliyouondwa na binadamu na jisi yanavyoingiliana.

*“Mazao ya misitu”* maana yake kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Misitu na.14 ya mwaka 2002 chini ni kitu chochote kinachopatikana au kuzalishwa kutokana na miti, mazao yanayoota au kupatikana msitu ni, ambayo ni pamoja na mianzi, magamba, mkaa, kuni, miti, fito mbao, mbegu za miti, nta, asali, utaa, matunda, upapi, majani ya kulalia wanyama, majani, mizizi, gundi, utomvu, maranda, matete, kamba, makuti (mawale), nyuzi za wanyama, mimea (miti) na kitu chochote chenye uhai au kisicho na uhai kitakachotangazwa katika gazeti la Serikali kuwa ni zao la msitu.

*“Misitu”* maana yake ni eneo la ardhi ambalo

limefunikwa angalau kwa asilimia 10 ya miti, uoto wa asili au iliyopandwa, au asilimia 50 au zaidi, ya vichaka na miti na miti inayoota upya ambayo itajumuisha aina yote ya misitu ya hifadhi ambayo itatangazwa chini ya Sheria ya Misitu Na.14 ya mwaka 2002 na mazao yote ya misitu ikijumuisha majani na nyasi ndani ya eneo la Halmashauri

“*Udongo*” kama ilivyo katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 maana yake ni pamoja na dunia, mchanga, miamba, miamba tope, madini, uoto wa mimea, mimea na wanyama iliyoko chini ya udongo pamoja na vumbi

“*Ushuru*” maana yake ni fedha inayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya mazao ya Misitu.

- |  |    |  |
|--|----|--|
| Ushuru wa Mazao ya misitu              | 4. | (1) Kutakuwa na Ushuru wa Mazao ya misitu utakaotowza na Halmashauri kwa mazao ya misitu yatakayouzwa ndani ya eneo la Halmashauri.  |
| Kibali cha biashara ya Mazao ya misitu |    | (2) Ni wajibu wa Mfanyabiashara ya mazao ya Misitu kuwa na kibali cha kufanya biashara hiyo kitakachotolewa na Halmshauri baada ya kuwasilisha maombi ya kibali kwa maandishi.           |
|  |    | (3) Ushuru huo utalipwa kwa Afisa Mwidhiniwa au wakala aliyeteuliwa kukusanya Ushuru kwa niaba ya Halmashauri kwa mujibu wa viwango vilivyoonyeshwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi. |
|  |    | (4) Ni haki ya kila mnunuzi kupewa Stakabadhi ya Malipo ya Ushuru wa Mazao ya misitu baada ya kutozwa Ushuru.  |
|  |    | (5) Stakabadhi ya Malipo itakuwa ushahidi pekee kuonyesha kuwa mazao ya misitu yamelipiwa Ushuru.  |
| Wakati wa kulipa ushuru                |    | (6) Ushuru huu utalipwa kabla ya mnunuzi kusafirisha mazao yake, au wakati wowote Mnunuzi atakapokutwa akisafirisha Mazao ya misitu isiyolipiwa Ushuru.                                  |
| Marufuku                               | 5. | (1) Ni marufuku kwa Mtu yeyote kununua au kusafirisha mazao ya misitu bila kuwa na kibali cha Halmashauri;   |
| Maeneo yaliyohifadhiwa                 |    | (2) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyoye kuvuna mazao ya misitu kwenye maeneo yaliyohifadhiwa.   |

- Makosa na adhabu
6. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa iwapo;
- atavuna na kusafirisha mazao ya misitu bila kabali;
  - atakiuka masharti ya kibali;
  - atachoma au kusababisha moto;
  - atakataa au kukwepa kulipa Ushuru;
  - atamshawishi mtu au kundi la watu wasilipe Ushuru;
- atakuwa ametenda kosa na atashitakiwa mahakamani na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini(50,000/=) au adhabu ya kifungo kisichopungua miezi sita jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.
- Kufifilisha kosa
7. Mkurugenzi anaweza kumsamehe mtu yeyote iwapo mkosaji atakayekiri kosa kwa maandishi kwa kujaza fomu ya kukiri kosa iliyoambatanishwa kwenye jedwali la nne la Sheria Ndogo hizi na kukubali kulipa Ushuru anaodaiwa pamoja na faini isiyozidi shilingi elfu hamsini;

## JEDWALI LA KWANZA

### Chini ya kifungu cha 4(3)

#### USHURU WA MAZAO YA MISITU

Na	Aina ya zao	Ushuru (TShs.)
1.	Mbao za aina zote na saizi zote ujazo wa m <sup>3</sup>	5% ya bei ya kununulia
2.	Nguzo miti laini ujazo wa m <sup>3</sup>	5% ya bei ya kununulia
3.	Nguzo miti migumu /asili ujazo wa m <sup>3</sup>	5% ya bei ya kununulia
4.	Nguzo mzigo ujazo wa m <sup>3</sup>	5% ya bei ya kununulia
5.	Kuni kwa mzigo ujazo wa m <sup>3</sup>	5% ya bei ya kununulia
6.	Kuni ujazo wa m <sup>3</sup>	5% ya bei ya kununulia
7.	Mkaa ujazo wa m <sup>3</sup>	5% ya bei ya kununulia
8.	Miche ya miti ya kawaida ujazo wa m <sup>3</sup>	5% ya bei ya kununulia
9.	Miche ya miti ya matunda na mapambo ujazo wa m <sup>3</sup>	5% ya bei ya kununulia
10.	Viwanda vya useremala	20,000 Kwa mwaka
11.	Nyungo	5% ya bei ya kununulia
12.	Mikeka	5% ya bei ya kununulia
13.	Vinu –kidogo	5% ya bei ya kununulia
14.	Vinu –kikubwa	5% ya bei ya kununulia
15.	Pinde	5% ya bei ya kununulia

16. Fagio	5% ya bei ya kununulia
17. Kamba	5% ya bei ya kununulia
18. Asali	5% ya bei ya kununulia
19. Ushuru wa pumba za kuchomea tofari ujazo wa m <sup>3</sup>	5% ya bei ya kununulia

**JEDWALI LA NNE**

**HATI YA KUKIRI KOSA**

Tarehe.....

Hati Na..... ya mwaka 20.....

Mimi.....  
 .... nakiri Chini ya kifungu cha 8 cha Sheria Ndogo hizo za (Ushuru wa Mazao ya Misisitu) za Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua za Mwaka, 2014kutenda makosa yafuatayo:-

- 1.....
- 2.....
- 3.....

Kwa hiari yangu ninakubali kuadhibiwa kwa kulipa faini ya Shilingi.....(kwa maneno:.....)  
 badala ya kushitakiwa mahakamani kwa makosa haya.

Saini ya Mkosaji..... Tarehe.....

**ADHABU/FAINI HII IMETOLEWA NA:-**

Jina.....  
 Cheo.....

Saini..... Tarehe.....

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua libandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe .....Mwezi.....mwaka 2014 na nembo hiyo ilibandikwa mbele ya:

.....  
ABDALLAH S.NGODU,  
Mkurugenzi Mtendaji ,  
Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua

NIMEKUBALI,

.....  
JOHN KADUTU,  
Mwenyekiti,  
Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua

.....  
MHE. MIZENGO P. PINDA(MB)  
WAZIRI MKUU

Dodoma,  
Tarehe.....2014.

TANGAZO LA SERIKALI Na. .... La tarehe .....

**SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)**

(SURA YA 287)

**SHERIA NDOGO**

Zimetungwa chini ya Kifungu cha 153

**SHERIA NDOGO ZA (USAFI WA MAZINGIRA) ZA HALMASHURI YA WILAYA YA KALIUA ZA MWAKA ,2014**

- |                            |    |   |
|----------------------------|----|---|
| Jina na mwanzo wa kutumika | 1. | Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua za mwaka, 2014 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali   |
| Eneo la matumizi           | 2. | Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua   |
| Tafsiri                    | 3. | <p>Katika sheria ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo;-</p> <p>“<i>Afisa mwidhiniwa</i>” maana yake ni Afisa biashara, Afisa afya wa Halmashauri na Afisa yeyote atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa sheria ndogo hizi ni pamoja na Afisa Mtendaji wa kata au Kijiji;</p> <p>“<i>Chakula</i>” maana yake ni kitu chochote kinacholiwa au kunywewa na binadamu isipokuwa madawa.</p> <p>“<i>Choo</i>” maana yake ni chumba maalum ambacho kimejengwa kwa ajili ya kuhifadhi kinyesi cha binadamu;</p> <p>“<i>Eneo lililowazi</i>” maana yake ni eneo lililochini ya Halmashauri ambalo limekatanzwa kufanyia shughuli ambayo haihusiani na matumizi yaliyokusudiwa</p> <p>“<i>Halmashauri</i>” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua</p> <p>“<i>Kero</i>” maana yake ni kitu chochote ambacho kipo katika hali yoyote au kinatumika, kimewekwa, kimejengwa, au ni</p> |

kichafu kiasi cha kusababisha’ -

(a) hatari kwa viumbe au maisha ya wanadamu

(b) harufu mbaya na ya kuudhi

“*Mkurugenzi*” maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Kaliua;

“*Mkazi*” maana yake ni raia wa Tanzania ambaye kwa kawaida anaishi kwenye eneo lililoko chini ya mamlaka ya Halmashauri na ambaye ama ana kaya au anaishi katika kaya au taasisi iliyopo katika eneo la Halmashauri’

“*Majani*” maana yake ni majani yote marefu vichaka vyenye urefu wa sentimita 15 au zaidi vinavyopatikana sehemu yoyote ndani ya Halmashauri hii ni pamoja na mazao marefu yanayolimwa kando ya barabara;

“*Maji taka*” kama ilivyo katika sheria ya usimamizi wa mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 ni pamoja na taka zinazotokana na jasho, uchafu wa majimaji kutoka majumbani, taasisi, kampuni, majengo ya biashara au viwandani;

“*Mabomba ya maji machafu*” maana yake ni mabomba yanayotumika kuchukua maji kutoka majumbani au kwenye mifereji ya maji machafu au ya mvua ni pamoja na bomba lolote lililowazi kupisha maji machafu au ya mvua;

“*Taka*” kama ilivyo kwenye sheria ya usimamizi wa mazingira ya mwaka 2004 maana yake ni kitu chochote kimiminika, kigumu, gesi na mionzi kinachotoa harufu mbaya au kinachohifadhiwa katika mazingira ya hali ya ujazo uozo au hali nyingine yoyote inayosababisha uharibifu wa mazingira ambayo inajumuisha taka;

“*Usafi wa mazingira*” maana yake ni usafi wa mazingira yanayozunguka binadamu kuwa katika hali isiyoweza kuleta madhara kwake na wengine hii ni pamoja na maji, miti, hewa, ardhi na wanyama, pamoja na viumbe visivyo hai kama vile nyumba;

“*Vyanzo vya maji*” maana yake ni maziwa, mabwawa, visima vya aina zote, chemichemi za mito.

“*Waziri*” maana yake ni waziri mwenye dhamana ya serikali za mitaa.

Wajibu wa  
mkazi

4. (1) Itakuwa ni wajibu wa kila mwenye nyumba au mpangaji kuhakikisha kwamba;-

(a) Mazingira yanayozunguka eneo la nyumba yake yanakuwa safi wakati wote

(b) Takataka zote au uchafu wote unakusanywa na kufukiwa au kuondolewa kwa njia itayoelekezwa na Halmashauri;

(c) Anachimba shimo la kutupia takataka litakalokuwa na upana usiopungua kimo cha futi 3 na upana usiopungua futi 2;

(d) Anajenga choo imara cha kudumu kilichojengwa kwa matofali na kuezekwa kwa bati chenye mlango unaofunga na kufunguka na kuhakikisha kwamba choo kinatumika wakati wote;

(e) Eneo lake analofanyia biashara liko katika hali ya usafi na kwa yale maduka ya chakula na dawa yatatakiwa kuwa yamesajiliwa na Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA)

(2)

(f) Eneo lilomzunguka halina mazalia ya mbu na wadudu wengine wahalibifu.

Itakuwa nikosa kwa mtu yeyote kumwaga takataka za aina yoyote katika mtaa, uchochoro, au mahali popote hadharani au katika eneo lolote la wazi bila idhini ya Halmashauri;

Maji taka

5. Itakuwa nimarufuku kwa mtu yeyote kuacha shimo la maji machafu wazi au kumwaga maji au taka, kutapisha au kuruhusu kumwaga au kutapisha au kuruhusu kufurika choo, 'septic tank', 'soakage' 'pit', 'cepool', au kuruhusu kupasuka au kuziba bomba la maji taka toka ndani ya nyumba na kuyatiririsha barabarani, njia kichaka, eneo la burudani, ama



sehemu yoyote isiyokusudiwa.

- |                                |     |   |
|--------------------------------|-----|---|
| Upikaji na uuzaji wa vyakula   | 6.  | (1) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kuzuia upikaji na uuzaji wa vyakula katika mazingira yasiyoridhisha kiafya.<br><br>(2) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kutengeneza au kuuza chakula mtaani, uchochoroni, magengeni au kwenye nyumba yeyote mpaka awe ametimiza masharti ya kanuni za afya na amepata kibali kutoka Halmashauri;  |
| Wajibu wa wahudumu kupima afya | 7.  | Itakuwa ni wajibu wa kila mhadumu wa hoteli, migahawa,. Baa, nyumba za kulala wageni, bucha, waoka mikate, au watu wanaoshughulika na kuuza vyakula vilivyopikwa kuhakikisha kwamba wanapima afya zao mara moja kila baada ya miezi sita pamoja na kuwa na kibali cha Halmashauri kinachomruhusu kuendesha biashara hiyo atachokilipia ada ya shilingi 5000/= kwa kila baada ya miezi sita.   |
| Uwezo wa Afisa mwidhiniwa      | 8.  | Afisa mwidhiniwa atakuwa na uwezo wakati wa kazi kuingia katika jengo lolote ndani ya Halmashauri ili kukagua kama kuna kero yoyote na kumtaka mtu yeyote anayehusika na kero hiyo kuiondoa katika muda atakaopewa na Afisa mwidhiniwa;   |
| Sauti ya muziki                | 9.  | Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kufungulia mziki kwa sauti ya juu ambayo itasababisha kelele na kuwa kero kwa wakazi wengine;  |
| Wajibu wa kila mwananchi       | 10. | (1) Itakuwa ni wajibu wa kila mwananchi anayeishi au kufanya shughuli zake katika eneo la Halmashauri kuchangia gharama za kuzoa takataka kutoka kwenye vyombo maalum vitavyowekwa mitaani kwa Mwezi kama ifuatavyo:-<br><br>(a) Shilingi 500/= kwa wakazi wa kawaida<br>(b) Shilingi 2,000/= kwa kila mfanyabiashara<br>(c) Shilingi 5000/= kwa malori ya mizigo.<br><br>(2) Afisa mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuingia katika eneo lolote kabla ya saa 12:30 jioni kwa lengo la kukagua usafi wa mazingira. |

- Kutenga maeneo maalumu 11. Halmashauri itatenga eneo maalumu (dampo) kwa ajili ya kutupa takataka na kutoa huduma ya uzoaji takataka kutoka majumbani, viwandani au sehemu yeyote zilipokusanywa takataka hizo.
- Marufuku 12. Ni marufuku kwa mtu yeyote kuendesha biashara ya upulizaji dawa (fumigation) au biashara ya kuua wadudu au wanyama waharibifu katika nyumba yoyote au mahali popote bila cheti cha taaluma kinachotambuliwa na Serikali na leseni kutoka Halmashauri.
- Makosa 13. (1) Itakuwa ni kosa chini ya sheria ndogo hizi kwa mtu yeyote;-
- (a) Kujenga choo chini ya umbali wa mita 60 kutoka kisimani, bwawani, ziwani, mtoni, au chanzo kingine cha maji yanayotumika, kwa matumizi ya binadamu;
  - (b) Kutoa kinyesi au kusababisha kinyesi, mkojo, maji machafu, yenye kinyesi kutoka kwenye choo chake au bafu lake au karo la kuoshea nyombo au nguo au kutoka kwenye bomba lolote linalochukua maji machafu, na kuyatitirisha kwenye barabara, mitaa, au kwenye mifereji ya maji ya mvua, au mfereji wowote uliowazi;
  - (c) Kutupa takataka au kusababisha mtu mwingine atupe takataka au kusababisha mrundikano wa takataka mahali popote palipokataliwa na Halmashauri;
  - (d) Kutiririsha maji machafu yanayoweza kusababisha kero kwa wakazi wa maeneo husika;
- (2)
- (e) Kuuza chakula nje ya maeneo yaliyotengwa kwa ajili hiyo.
- Mtu yeyote atakayekiuka sheria ndogo hizi atalazimika kukiri kosa hilo kwa kujaza fomu maalumu mbele ya mkurugenzi kama ilivyo katika sheria ndogo hizi;
- Upulizaji wa dawa 14. Halmashauri itatoa huduma ya kupuliza dawa kuua wadudu katika nyumba za biashara, Ofisi mbalimbali, na nyumba za kuishi kwa ada kama ifuatavyo;-
- (a) Nyumba ya biashara Shilingi 10,000/= kwa kila hitaji

(b) Nyumba ya kuishi Shilingi 5,000/= kadiri ya mahitaji

(c) Maofisi na majengo mengine kama makanisa na misikiti Shilingi 15,000/= kadiri ya mahitaji

Adhabu 15. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya sheria ndogo hizi atakuwa ametenda kosa la jinai na akipatikana na hatia atalazimika kulipa faini isiyoziidi shilingi laki tatu (300,000/=) au kifungo cha miezi kumi na miwili jela au adhabu zote mbili kwa pamoja faini na kifungo

### **HATI YA KUKIRI KOSA**

Chini ya kifungu cha 13 (2)

Tarehe.....

Hati Na..... ya mwaka 20.....

Mimi.....  
.... nakiri Chini ya kifungu cha 13 cha Sheria Ndogo hizi za (Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua za mwaka 2014 kutenda makosa yafuatayo:-

- 1.....
- 2.....
- 3.....
- 4.....

Kwa hiari yangu ninakubali kuadhibiwa kwa kulipa faini ya Shilingi.....(kwa maneno:.....)  
badala ya kushitakiwa mahakamani kwa makosa haya.

Saini ya Mkosaji..... Tarehe.....

**ADHABU/FAINI HII IMETOLEWA NA:-**

Jina..... Cheo.....  
Saini..... Tarehe.....

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua ilibandikwa katika Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe.....mwezi.....mwaka 2014 na nembo hiyo ilibandikwa mbele ya;-

.....  
**ABDALLAH S.NGODU**  
Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.

.....  
**JOHN KADUTU**  
Mwenyekiti,  
Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.

NIMEKUBALI.

.....  
**MHE.MIZENGO P.PINDA(MB)**  
WAZIRI MKUU.

Dodoma  
Tarehe.....2014.

TANGAZO LA SERIKALI Na. .... La tarehe .....

**SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)**

(SURA YA 287)

**SHERIA NDOGO**

Zimetungwa chini ya Kifungu cha 153

**SHERIA NDOGO ZA (Usafi na Uhifadhi wa Mazingira) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KALIUA ZA MWAKA 2014.**

Jina na mwanzo wa kutumika	1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za usafi na hifadhi ya mazingira za Halmashauri ya wilaya a Kaliua za mwaka 2014 na zitaanza kutumika mara baada ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali
Eneo la matumizi	2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya wilaya ya Kaliua
Tafsiri	<b>3.</b> Katika Sheria Ndogo hizi, isipokuwa tu kama itaelekezwa vingnevyo “ <b>Afisa Afya</b> ” maana yake ni Afisa wa Afya aliyeajiriwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua anayeshauri kusimamia na kuratibu masuala yote ya afya na kinga katika mamlaka ya Halmashauri; “ <b>Afisa Mazingira</b> ” maana yake ni Afisa Mazingira aliyeajiriwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua anayeshauri, kusimamia na kuratibu masuala yote ya mazingira katika mamlaka ya Halmashauri; “ <b>Ardhi hatarishi</b> ” maana yake hi ardhi ambayo ikiendelezwa inaweza kuleta hatari katika maisha au kusababisha uharibifu wa mazingira katika ardhi hiyo au nyingine inayopakana nayo.“ <b>Chukizo</b> ” maana yake ni kero au kitu chochote kinachoweza kuleta madhara au kuhatarisha afya ya binadamu; “ <b>Chakula</b> ” maana yake ni kitu chochote kinachofaa kuliwa na kutoleta madhara kwa binadamu.; “ <b>Afisa muidhiniwa</b> ” maana yake ni mtumishi yeyote wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua anayesimamia sheria ndogo hizi;

**“Kelele”** ni kila aina ya uchafuzi au usumbufu usababishwao na sauti ambayo iwezayo kusababisha athari mbaya kwa afya ya binadamu na mazingira;

**“Halmashauri”** maana yake ni Halmashauri ya wilaya ya Kaliua;

**“Hifadhi ya mazingira”** maana yake ni eneo lolote lile lililotengwa na Halmashauri kama hifadhi kama vile maeneo ya misitu, mabonde, vyanzo vya maji na milima;

**“Makazi”** ni pamoja na nyumba, kiwanja na kila aina ya milki ikiwa ni pamoja na mashine, mitambo au gari litumikalo katika kazi yoyote ifanywayo katika makazi hayo;

**“Kiwanda”**Maana yake ni jengo au kundi la majengo au eneo ambapo vitu vinatengenezwa

**“Mamlaka”** maana yake ni mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.

**“Mazingira”** yanahusisha maumbile halisi yamzungukayo binadamu ikiwa ni pamoja na hewa, ardhi, maji, tabianchi, sauti, mwanga, harufu, hali za kibaolojia za wanyama na mimea, rasilimali za kitamaduni na masuala ya kiuchumi, kijamii, majengo na mambo mengine yaliyoundwa na au kutengenezwa na binadamu na yale ya asili;

**“Mifugo”** ni pamoja na ng’ombe, kondoo, mbuzi, nguruwe, kuku, farasi, mbwa, punda na wanyama wengine wanaofugwa na kudhibitiwa na binadamu;

**“Misitu”** inahusisha ardhi yenye uoto wa mimea na uwingi wa miti ya kimo chochote ivunwayo na isiyovunwa;

**“Rasilimali za mazingira”** ni pamoja na rasilimali za hewa, ardhi, maji, misitu na uoto mwingine wa asili, wanyama na mimea;

**“Sheria”** maana yake ni Sheria za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) sura ya 288 toleo la mwaka 2002;

**“Taka hatarishi”** maana yake ni taka ngumu, miminika na hewa ambazo zina kiwango kikubwa cha kemkali ambazo husababisha sumu na kuathiri maisha ya binadamu pamoja na mazingira kwa ujumla wake;

**“Udongo”** hujumuisha ardhi, mchanga, mwamba, mwambatope, madini, uoto, mimea na viumbe waishio humo na vyote vitokanavyo kama vile vumbi;

**“Uharibifu”** maana yake ni mabadiliko ya moja kwa moja ya rasilimali za kimaumbile, hali ya joto, kemikali, kibaolojia ambazo kwazo ni sehemu ya mazingira na hivyo kuleta madhara kwa matumizi yenye manufaa, au kusababisha hali ambayo ni hatari kwa jamii kiafya, kiusalama au ustawi wa binadamu na mazingira;

**“Jengo”** maana yake ni nyumba, kibanda, kontena na hema;

**“Kibali cha ujenzi”** maana yake ni idhini ya maandishi

inayotolewa na Mkurugenzi au Afisa muidhiniwa chini ya sheria ndogo hizi kwa ajili ya ujenzi au ukarabati wa jengo;

**“Mkurugenzi”** maana yake ni mtendaji mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua

**“Usimamizi wa mazingira”** ni pamoja na kulinda, kuhifadhi na kutumia kwa njia endelevu sehemu ya rasilimali ya mazingira.

**“vyanzo vya maji”** maana yake ni pamoja na chemchem, mito, mabwawa, ardhi owevu, mabonde ya mito na maeneo ya milima; na

**“Zizi”** maana yake ni jengo maalum kwa ajili ya matumizi ya kufugia mifugo.

**“chukizo”** maana yake ni kitu chochote ambacho kimewekwa au kujengwa katika hali ya uchafu na kinaweza kusababisha madhara kwa maisha ya binadamu, adha, mazalia ya wadudu na wanyama hatari au madhara kwenye chakula na vyanzo vya maji;

**“eneo la mbele ya nyumba”** maana yake ni eneo lote la mbele ya nyumba na eneo lililoko kati ya nyumba na barabara inayopana na nyumba hiyo au kuungana na eneo la nyumba pamoja na eneo la hifadhi ya barabara linalopitisha maji ya nvua hadi katikati ya barabara hiyo;

**“gharama za uzoaji taka”** maana yake ni gharama zilizopangwa na mamlaka kwa madhumuni ya kulipia huduma za uzoaji taka;

**“huduma”** maana yake ni pamoja na usafishaji, ukusanyaji, uondoaji na usafirishaji wa taka;

**“kaya”** maana yake ni pamoja na mtu, familia au watu waishio pamoja;

**“lundo kubwa la taka”** maana yake ni pamoja na vifaa na zana chakavu, mabaki ya samani, ambayo haihusishi mabaki ya vifaa vya ujenzi au wanyama waliokufa wenye uzito mkubwa zaidi ya ule uliobainishwa kwenye mzigo wa taka;

**“mmiliki”** maana yake ni mmiliki yeyote wa jengo au ardhi;

**“mzigo wa taka”** maana yake ni pamoja na sehemu ya mabaki ya miti, vichaka, magazeti, majarida au taka ngumu zilizofungwa pamoja;

**“nyumba ya makazi”** maana yake ni pamoja na jengo lolote linalotumiwa kwa kuishi, pia inajumuisha ardhi ambayo haijaendelezwa lakini imetolewa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya kuishi;

**“soko”** maana yake ni pamoja na soko lililoidhinishwa kisheria na mamlaka au eneo lililoainishwa kwa madhumuni ya kufanyia biashara;

**“taka hatari”** maana yake ni pamoja na taka zenye sumu, taka zinazoweza kuwaka, kumeng’enyua mwili, taka zenye mionzi

au taka hatari kama ilivyobainishwa na Taasisi ya kuhifadhi mazingira ya Taifa na inajumuisha mafuta ya diseli, mafuta ya taa, mafuta ya petroli, rangi, mafuta ya kuyeyushia, betri za tochi, betri za magari, madawa ya kuulia wadudu waharibifu, taka za hospitali, mafuta mazito ya kuteleza, mafuta ya kulainisha na kuchanganya na vitu vingine viwandani, madawa ya kuulia wadudu, madawa ya kugeuza maumbile, mizoga na maiti;

“**taka ngumu**” maana yake ni aina zote za taka zinazozalishwa majumbani, kwenye taasisi, maeneo ya biashara na viwandani lakini haihusishi majitaka au taka miminika;

“**taka za majengo ya biashara**” maana yake ni taka zote zinazozalishwa kutoka katika majengo ya biashara na viwanda pamoja na taka zitokanazo na utoaji wa huduma mbalimbali lakini haihusishi taka zizalishwazo majumbani.

“**ufugaji wa ndani**” maana yake ni ufugaji wa ndani ya jengo; “**wakala**” maana yake ni mzabuni aliyeteuliwa kisheria na mamlaka ili kutoa huduma ya uzoaji taka kwa niaba yake;

## **SEHEMU YA II HIFADHI YA MAZINGIRA NA VYANZO VYA MAJI**

*Upandaji na utunzaji  
Miti*

**(1) Litakuwa ni jukumu la Halmashauri kuhakikisha kwamba:-**

(a) Inatenga eneo maalum kwa ajili ya kuotesha miche ya miti ambayo itapandwa katika maeneo mbalimbali ndani ya Halmashauri kwa utaratibu utakaopangwa.

(b) Inatenga eneo au maeneo kwa ajili ya kupanda miti au kutunza miti

iliyokwisha pandwa kama hifadhi ya misitu na hakuna shughuli zozote

zitakazo ruhusywa kufanyika katika eneo au maeneo hayo.

(c) Inasimamia utunzaji wa rasilimali za misitu iliyomo katika mamlaka yake.

(d) Inasimamia kampeni za kitaifa, kimkoa na kiwilaya za kupanda miti na kuhifadhi mazingira.

(e) Inapanga siku moja au zaidi kwa kila mwaka kwa ajili ya kupanda miti

ambapo watu wote watakaotakiwa kushiriki katika zoezi hilo watalazimika

(f) Inatenga maeneo maalum kwa ajili ya shughuli za uchimbaji mchanga

kokoto, mawe, udongo, kifusi, kuoshea magari, karakana, mashine za



mbao na nafaka na shughuli hizi zitafanywa baada ya kuomba na kupata

Kibali cha hifadhi ya mazingira cha Halmashauri.

(2) Mmiliki yeyote wa ardhi atapaswa kupanda na kuhifadhi miti isiyopungua mitano katika eneo lake na mmiliki mpya wa ardhi hatapata kibali cha ujenzi hadi atakapo kuwa amepanda na kutunza miti isiyopungua mitano katika kiwanja chake kwa kuzingatia aina na maelekezo yatakayotolewa na Halmashauri.

(3) Kila asasi na taasisi zilizomo ndani ya mipaka ya Halmashauri zitahakikisha kwamba:-

(a) zinapanda na kutunza miti katika maeneo yaliyo chini ya uangalizi wao.

(b) zinashiriki vema katika shughuli za kupanda miti na kuhifadhi mazingira

pale watakapo takiwa kufanya hivyo.

(c) zinatoa taarifa mara moja kwa mamlaka pale inapobainika kuwa kuna

(4) Taasisi au mtu yeyote atamiliki kitalu cha miti baada ya kupata kibali cha maandishi kutoka Mamlaka.

#### ***Ukataji miti***

5 (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kukata mti au sehemu ya mti pasipo kupata kibali cha Mamlaka.

(2) Halmashauri itatenga maeneo ya misitu ambayo miti itaruhusiwa kukatwa kwa ajili ya matumizi mbali mbali baada ya kupata kibali cha Mamlaka

#### ***Uwashaji moto***

6. Mtu yeyote atakayewasha moto au kufanya au kutokufanya jambo ambalo litasababisha kuwaka moto katika maeneo ya misitu isipokuwa kwa kibali cha mamlaka atakuwa ametenda kosa

#### ***Ardhi hatarishi***

7. -(1) Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi maeneo ambayo ni vyanzo vya maji, pembezoni mwa mito, visima vya maji, chemichemi za maji pamoja na miteremko ya milima ni maeneo ya ardhi hatari.

(2) Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kufanya shughuli zifuatazo katika maeneo yaliyoainishwa katika kifungu kidogo cha (1) hapo juu bila kupata kibali cha Halmashauri:-

(a) Kuweka, kujenga, kurekebisha, kuondoa au kubomoa aina yoyote ya jengo.

(b) Kuchimba au kulima kwa madhumuni yoyote yale.

(c) Kupanda mmea au sehemu fulani ya mmea uwe wa asili au usio wa asili

pasipo idhini ya Halmashauri.

(d) Kuchepusha maji ya mto au mfereji kutoka katika mkondo wake pasipo kibali cha Mamlaka.

- (e) Kufanya shughuli za kilimo.
- (f) Kupitisha barabara, njia au mfumo wowote wa miundombinu.
- (g) Kukata miti au kuathiri ukuaji wake.
- (h) Uanziswaji wa fukwe (beach)

### **Ufugaji**

- 8.-(1) Hakuna mtu atakayeruhusiwa kufuga mifugo ndani ya mipaka ya Halmashauri bila ya kuwa na kibali cha maandishi cha Halmashauri.
- (2) Halmashauri itatoa kibali cha ufugaji baada ya kuridhika kwamba ufugaji huo hautakuwa kero kwa jamii.
- (3) Ufugaji ambao utaruhusiwa katika maeneo mjini ni ule tu wa ndani ambao utakuwa umethibitishwa na Halmashauri.
- (4) Katika kibali hicho Afisa Mifugo wa Halmashauri atataja aina na idadi ya mifugo inayoruhiwa kufugwa kulingana na ukubwa wa eneo la mfugaji pamoja na masharti mengine.
- (5) Kibali kikitakachotolewa chini ya Sheria Ndogo hizi kitadumu kwa muda wa mwaka mmoja kuanzia tarehe ya kibali hicho na kitalipiwa.

### **Usafi wa zizi**

- 9.-(1) Kila mfugaji atahakikisha kwamba sehemu yake anayotumia kufugia inakuwa katika hali ya usafi wakati wote na anakuwa na shimo au chombo cha kuhifadhia uchafu unaozalishwa na mifugo yake.
- (2) Afisa muidhiniwa atakuwa na mamlaka ya kumtaka mfugaji kuondoa uchafu wowote ule uliopo kwenye jengo analotumia kufugia.
- (3) Afisa muidhiniwa atakuwa na mamlaka ya kuingia katika jengo lolote lile linalotumiwa kwa kufugia kwa lengo la kukagua usafi.

### **Usafirishaji wa mifugo**

- 10.-(1) Hakuna mtu yeyote atakaye ruhusuwa kusafirisha mfugo wake kutoka katika sehemu mmoja ya Halmashauri kwenda katika sehemu nyingine bila ya kuwa na kibali kutoka Halmashauri. Hata hivyo sheria hii haitahusu mifugo inayokwenda katika machinjio ambayo itakuwa inasafirishwa kwenye gari au ambayo ina kibali kilichotolewa na Serikali.
- (2) Kibali cha kusafirisha mifugo kutoka katika sehemu moja kwenda nyingine kitadumu kwa muda wa siku kilipotolewa tu na kitalipiwa kama itakavyoelekezwa na Mamlaka.

***Kuhamisha mifugo***

11.-(1) Mkurugenzi wa Halmashauri chini ya sheria ndogo hizi kuamuru mifugo ihamishwe kutoka katika sehemu inayofugiwa iwapo ufugaji huo unakinzana na sheria za mipango miji hivyo kuwa kero kwa wakazi wa eneo husika.  
(2) Iwapo Mkurugenzi atatoa amri hiyo Halmashauri haitahusika na ghrama wala hasara ambayo mfugaji atakuwa amepata.

***Ukamataji wa mifugo***

12. -(1) Afisa muidhiniwa atakuwa na mamlaka ya kukamata mifugo ambayo:-  
(a) inafugwa bila kibali;  
(b) inafugwa nje ya jengo la kufugia;  
(c) inasafirishwa bila ya kuwa na kibali; na  
(d) inazurura katika eneo la Halmashauri.  
(2) Pasipo kuathini kifungu kidogo cha (1) hapo juu mamlaka inaweza kuchukua uamuzi wa kuuu mbwa wataokutwa wanazurura ovyo mitaani pasipo kuwa na kibali cha Halmashauri.

***Gharama za ukamataji na utunzaji wa mnada***

13.-(1) Halmashauri itakuwa na uwezo wa aidha kuuza kwa mnada wa hadhara mfugo uliokamatwa baada ya kutoa tangazo la siku saba ya nia ya kuuza mfugo huo kwa mnada.  
(2) Kama mtu atakamatiwa mifugo yake kwa mara ya kwanza atalipia gharama za ukamataji na utunzaji wa mifugo iliyokamatwa kama ilivyoainishwa katika jedwali la Sheria ndogo hizi.  
(3) Endapo mtu atashindwa kilipia mifugo yake ndani ya siku saba kuanzia siku ya kukamatwa basi mifungo hiyo itauzwa katika mnada wa hadhara.  
(4) Halmashauri haitahusika na kifo, hasara na upotevu wowote ule wa mifugo itakayo kamatawa

***Uteuzi wa wakala***

14. Katika kutekeleza sheria ndogo hizi Halmashauri itakuwa na uwezo wa kumteua wakala ili kusimamia utekelezaji wa sheria hizi na hivyo kuwa na mamlaka ya kukamata, kutoza adhabu na kumshitaki mtuhumiwa katika vyombo vya sheria.

**SEHEMU YA III  
HIFADHI YA ARDHI NA SHUGHULI ZA KILIMO**

***Uchimbaji wa madini ya vito vya thamani, mawe udongo, mchanga na kokoto***

15. -(1) Ili kuzuia uharibifu wa ardhi na mmomonyoko wa udongo itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuchimba madini, mawe, udongo, mchanga na kokoto kwa ajili ya matumizi yoyote yale au kumiliki eneo kwa ajili ya shughuli

hizo pasipo kupata kibali cha mazingira cha Mamlaka na cheti cha tathmini ya athari za mazingira.

(2) Mtu yeyote atakayepewa kibali cha kuchimba, madini, mawe, udongo, mchanga kokoto au kufyatua tofali au kuchoma tofali hizo, ataruhusiwa kufanya shughuli iliyokusudiwa tu na si vinginevyo na kwa kiasi kilichoainishwa katika kibali husika na atatakiwa kulipa ada kama itakavyowekwa kisheria.

(3) Vibali vya uchimbaji mdogo wa madini ya vito vya thamani vitatolewa kwa watu waliojiunga katika vikundi vilivyosajiliwa na mamlaka ya Halmashauri na vitatakiwa kukata leseni na kulipia ushuru wa uchimbaji wa madini .

(4) wachimbaji wote wadogo wadogo hawataruhusiwa kusafisha madini kwa kutumia kemikalihatarishi mfano “cynide”, Zebaki n.k bila kibali kutoka katikamamlaka .

***Kibali cha mazishi***

16 -(1) Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi shughuli zote za mazishi zitafanyika katika maeneo yaliyotengwa kwa shughuli hiyo baada ya kuwasiliana na kupata kibali cha Halmashauri na kufuata maelekezo yote yatakayotolewa na Afisa anayehusika.

(2) Mtu yeyote atakayebainika kuhusika katika kufanya shughuli za mazishi katika makaburi yaliyofungwa au katika maeneo ya makazi au maeneo yasiyoruhusiwa kisheria atakuwa ametenda kosa kwa mujibu wa sheria ndogo hizi

***Uharibifu wa barabara***

17. (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote:-

(a) kukata, kuweka matuta na vizuizi vingine katika eneo lolote la barabara;

(b) kufanya uchafuzi wa aina yoyote katika eneo la barabara; na

(c) kuingiza maji machafu katika mifereji ya barabara.

pasipo kupata kibali cha Mamlaka na kulipa ada iliyowekwa kisheria.

(2) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuharibu miundombinu ya aina yoyote, kalvati, kujitengenezea mifereji ya maji ya mvua au kujitengenezea barabara bila idhini ya Mamlaka.

***Ujenzi kwenye eneo la barabara***

18.-(1) Mtu yeyote ambaye atakuwa amejenga au ameweka jengo lolote katika eneo la barabara atatakiwa kuondoa au kubomoa ujenzi huo baada ya kupewa taarifa ya maandishi ya siku kumi na nne.

(2) Iwapo baada ya kupewa taarifa ya siku kumi na nne mtu huyo atashindwa kutekeleza amri hiyo, Halmashauri itabomoa

na kumpelekea gharama za ubomoaji huo mhusika.

***Shughuli za kilimo  
Sheria Na. 8/2007***

19. Ni marufuku kuendesha shughuli za kilimo cha mazao marefu ya zaidi ya futi tatu katika maeneo yote ya Halmashauri na kama itabidi ni baada ya kupata kibali cha Mamlaka.

***Biashara ya mazao  
ya misitu***

20. –(1) Mtu yeyote haruhuwi: si  
(a) kufanya biashara ya mazao ya misitu bila ya kuwa na leseni kutoka katika Mamlaka.  
(b) kusafirisha mazao ya misitu nje au kuingiza na kuteremsha pasipo kupata kibali ambacho kitalipiwa.

(2) Kwa madhumuni ya sheria ndogo hii na pasipo kuathiri vifungu vya sheria ndogo hii hairuhusiwi kusafirisha au kuteremsha mazao ya misitu kuanzia saa 12.00 jioni hadi saa 1.30 asubuhi.

***Ukiukwaji wa  
matumizi ya ardhi***

21. Itakuwa ni ukiukwaji wa Sheria Ndogo hizi endapo mtu yeyote atabainika kutumia ardhi kwa matumizi ambayo ni kinyume na masharti ya matumizi ya kiwanja alichopewa kisheria au eneo hilo.

***Kamati ya Mazingira***

22. –(1) Kutakuwa na Kamati ya Mazingira kwa kila Kata, Kijiji na Mtaa/Kitongiji itakayohusika na usimamizi wa mazingira kwa Kata, Kijiji na Mtaa/Kitongiji husika.  
(2) Kamati katika kusimamia mazingira itashirikiana na askari mgambo kupita na kukagua usafi nyumba kwa nyumba na maeneo yote ya biashara, na iwapo itabaini ukiukwaji wa Sheria ndogo hizi kamati itatoza papo kwa papo faini isiyopungua elfu hamsini kwa kila kosa.  
(3) Mtu yeyote atakaye kaidi kulipa faini chini ya kifungu cha (2) hapo juu, atashitakiwa na akitiwa hatiani atatozwa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Elfu hamsini ua kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja yaani faini na kifungu.  
(4) Mapato yatakayo kusanywa chini ya kifungu cha (2) hapo juu yatagawanywa katika mafungu matatu, asilimia 40% kama posho ya askari mgambo, asilimia 40% itabaki kwa matumizi ya ofisi na asilimia 20% itaingizwa Halmashauri.

***Uharibifu na  
uchafuzi wa***

23. (1) Ili kuepuka uharibifu unaoweza kujitokeza katika maeneo ya vituo vya mabasi, barabarani na maeneo mengine

*mazingira*

ya wazi itakuwa ni kosa chini ya sheria ndogo hizi kufanya matengenezo, kubadilisha mataili au kuosha vyombo vya usafiri wa barabara katika maeneo hayo.

(2) Kwa mujibu wa sheria ndogo hii si ruhusa kwa mtu yeyote kukojoa katika eneo lolote lile isipokuwa katika sehemu iliyoandaliwa kwa matumizi hayo.

(3) Mtu yeyote atakayepatikana na hatia kwa kuvunja kifungu kidogo cha (1) hapo juu, pamoja na adhabu nyingine atakayopewa pia atalazimika kulipa fidia kutokana na uharibifu atakaosababisha kwenye barabara husika.

(4) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuondoa chombo chochote cha usafiri ambacho ni kibovu au kimetelekezwa barabarani na kuhifadhi kwa gharama za mmiliki wa chombo husika.

*Vituo vya kuoshea magari na ujenzi wa majengo*

24. –(1) Hakuna mtua atakayeruhusiwa kujenga kituo cha kuoshea magari pasipo kwanza kusajiliwa na kupata cheti cha tathmini ya athari ya mazingira.

(2) Mtu yeyote atajenga jengo kubwa na kituo cha mafuta baada ya kukaguliwa na kupata cheti cha tathmini hya athari ya mazingira

**SEHEMU YA IV**

**UDHIBITI WA UCHAFUZI WA HEWA**

*Udhibiti wa hewa chafu*

25. Ili kuepuka madhara ambayo binadamu anaweza kupata kutokana na hewa chafu ni marufuku mtu yeyote:

(a) kufanya shughuli yoyote inayoweza kuzalisha moshi na hewa chafu katika maeneo ya makazi, maeneo ya ofisi, maeneo ya wazi, barabarani na maeneo ya biashara.

(b) kuachia hewa chafu au kali hewani ambayo inaweza kuathiri mfumo wa anga na hewa.

(c) kuendesha mtambo chakavu ambao unatoa moshi mkali hasa katika makazi, barabarani na ofisini.

*Shughuli za viwanda na vyombo vya usafiri*

26. –(1) Wamiliki wote wa viwanda watahakikisha kuwa:-

(a) wanakagua mashine zao mara kwa mara ili kuhakikisha kwamba zinafanya kazi vizuri na kuzuia moshi na hewa chafu;

(b) mabomba ya kutolea moshi na hewa chafu yanafungwa vifaa maalum ili kuepuka na au kupunguza madhara kwa viumbe hai na mazingira; na

(2) Shughuli zote za viwanda ikiwa ni pamoja na karakana, mashine kubwa za kusaga na kukoboa na mashine za mbao zitafanyika tu katika maeneo yaliyotengwa kwa kazi hiyo ili kuepusha hewa chafu, vumbi, kelele na madhara mengine

katika maeneo ya makazi na shughuli nyinginezo za binadamu isipokuwa kwa mashine ndogo za kusaga nafaka kwa umeme.  
(3) Viwanda vyote vitatakiwa kuwa na cheti cha tathmini ya mazingira kilichotolewa na Serikali na kuorodheshwa kwa ukaguzi.

***Uzuiaji wa vyombo vitoavyo kelele kubwa***

27. -(1) Ni marufuku kupitisha vyombo vya usafiri wa barabara vitoavyo kelele kubwa katika maeneo yanayohitaji utulivu, hasa katikati ya mji, hospitali, ofisi za taasisi mbalimbali na makazi ya watu, na kama itaruhusiwa ni baada ya kupata kibali cha mamlaka.  
(2) Halmashauri itachukua hatua za kisheria dhidi ya mtu yeyote atakayeendesha shughuli za kibiashara kama vile muziki, mihadhara na mahubiri, mnada na kufanya matangazo ya biashara kwa kutumia vipaza sauti kwa sauti ya juu na kusababisha kero kwa watu katika maeneo ya makazi na yale yanayohitaji utulivu mkubwa bila kupata kibali cha Mamlaka.

***Nyumba kuwa na hewa safi***

28. Kila mkazi wa Halmashauri atahakikisha kwamba nyumba yake inakuwa na:-  
(a) milango na madirisha ili kuruhusu hewa na mwanga wa kutosha; na  
(b) mfumo bora wa kupitisha moshi kutoka jikoni na maeneo mengineyo yanayotoa au kuzalisha moshi

**SEHEMU YA V  
UJENZI MJINI**

**Kibali cha ujenzi  
Sura ya 379**

29. -(1) Bila kuathiri Sheria ya Mipango Miji hakuna mtu atakayeruhusiwa kujenga katika eneo la Halmashauri kabla ya kupata kibali kutoka Halmashauri.  
(2) Pamoja na masharti mengine yatakayokuwemo katika kibali cha ujenzi, umbali kutoka katikati ya barabara na najengo litakalo jengwa utakuwa ni Mita 10 kwa baranara kuu na mita 5 kwa barabara za mitaani.

30.-(1) Kutakuwa na mpango wa ujenzi ambao utaaanisha aina ya nyumba za kujengwa katika maeneo ambayo yatakuwa yameainishwa katika mpango huo.  
(2) Kila mtu atakayetaka kujenga atahakikisha kwamba jengo analotaka kujenga linaoana na mpango wa ujenzi.

31.-(1) Litakuwa ni jukumu la mwenye nyumba au mpangaji kuhakikisha kwamba jengo na mazingira yake yanakuwa katika hali ya usafi wakati wote.

(2) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kumtaka mwenyenyumba au mpangaji kukarabati nyumba ikiwa ni pamoja na kupaka frangi endapo nyumba hiyo imechakaa

#### **JEDWALI**

#### **VIWANGO VYA ADHABU KWA WANYAMA WANAOKAMATWA**

(Chini ya kifungu cha 13(2))

<b>NA</b>	<b>AINA YA MIFUGO</b>	<b>VIWANGO VYA ADHABU VYA SASA KWA SIKU</b>	<b>VIWANGO VYA ADHABU VYA ZAMANI KWA SIKU</b>
1	Ng'ombe/Nguruwe/Punda	10,000/=	3000/=
2	Mbuzi/Kondoo	7000/=	2000/=
3	Wanyama wengine	5000/=	-

#### **SEHEMU YA VI**

#### **UDHIBITI WA TAKA NGUMU NA TAKA MIMINIKA**

32. -(1) Kila mmiliki wa nyumba au mpangaji wa nyumba ya makazi au biashara atalazimika kuweka na kutunza vyombo vya kutunzia taka vyenye mifuniko na mishikio na ujazo usiopungua Lita 25 kama ambavyo mamlaka itaridhia.

(2) Itakuwa ni jukumu la mwenye nyumba au mpangaji kutunza takataka zilizohifadhiwa kwenye vyombo na kuzipeleka kwenye sehemu maalum ya kukusanyia taka au katika mahala ambapo Mamlaka itaelekeza.

(3) Kila mmiliki wa nyumba au mpangaji atalazimika kutenganisha taka atakazozalisha kama vile mabaki ya chakula, karatasi, chupa, makopo na plastiki katika vyombo tofauti.

#### ***Wajibu wa kutunza usafi***

33. -(1) Itakuwa ni wajibu wa mwenye nyumba au mpangaji kusafisha, kuondoa taka na kulitunza eneo lake katika mandhari ambayo mamlaka itaridhia.

(2) Pasipo kuathiri kifungu cha 4 cha Sheria Ndogo hizi, ni marufuku kwa mtu yeyote kuweka, kusababisha na kuruhusu



taka kutupwa katika eneo lolote la jengo lake.

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kutupa taka katika maeneo ya wazi, mitaani, barabarani, mitaro ya maji ya mvua, vyanzo vya maji na maeneo mengine yasiyoruhusiwa.

(4) Kila mmiliki na dereva wa chombo cha kusafirishia mizigo atahakikisha anaweka vifaa vya kufunika bidhaa anazosafirisha ili kutoruhusu bidhaa hizo kudondoka au kumwagika na hivyo kuchafua mazingira.

(5) Wamiliki au madereva wote wa vyombo vya kusafirisha abiria watahakikisha wanaweka vyombo vya kuhifadhi taka zitakazozalishwa ndani ya gari husika na kuzitupa katika sehemu maalum zilizowekwa na mamlaka kwa madhumuni hayo.

#### ***Mabaki ya ujenzi***

34. –(1) Mtu yeyote hataruhusiwa kubomoa au kusababisha kubomoka jengo au sehemu ya jengo bila kibali cha mamlaka na ubomoaji huo utafanyika kuanzia saa 1.00 usiku hadi saa 10.00 alfajiri ili kuepuka kero kwa watumiaji wa maeneo yaliyo karibu na jengo husika.

(2) Kila mtu atakayeomba kibali cha ubomoaji atalazimika kuondoa na kulipa kwa Mamlaka gharama za ubomoaji na uondoaji wa mabaki ya jengo lililobomolewa kama ilivyoainishwa katika jedwali “B” la sheria ndogo hizi.

#### ***Taka hatari***

35. Kila mmiliki na mkazi wa jengo ambalo taka hatari huzalishwa atakuwa na jukumu la kuhifadhi na kuzitupa taka hizo katika maeneo yanayostahili kama itakavyoelekezwa au kuamriwa na mamlaka.

#### ***Ukusanyaji wa taka***

36. Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi Mamlaka itaandaa utaratibu wa ukusanyaji wa taka kutoka katika maeneo mbalimbali ambako taka huzalishwa na kuzikusanya kisha kuzisafirisha na kuzitupa katika maeneo yaliyoandaliwa.

#### ***Matumizi ya vifaa vya kubebea mizigo***

37. –(1) Ni kinyume chini ya Sheria Ndogo hizi kwa kila mzalishaji, mfanyabiashara, dalali au mtu yeyote anayejihusisha na biashara ya usafirishaji wa mazao ya chakula au bidhaa nyinginezo kuingiza sokoni bidhaa hizo zikiwa zimehifadhiwa na kufungwa kwa kutumia majani, matawi ya miti au matenga.

(2) Mamlaka inaweza kuzuia uingizaji sokoni wa mazao ya

chakula au bidhaa nyinginezo zitakazoingizwa kinyume na ilivyoagizwa katika kifungu kidogo cha (1) hapo juu au kuamuru kuchukuliwa hatua muafaka kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

***Wajibu wa kulipa  
ada***

- 38 –(1) Kila mkazi au kaya atalipa ada za ukusanyaji taka kila mwisho wa mwezi kwa kiwango cha fedha kama ilivyoainishwa katika Jedwali “A” la Sheria Ndogo hizi.
- (2) Kaya kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi zitagawanyika katika makundi matatu:
- (a) kundi lenye kipato cha juu;
  - (b) kundi lenye kipato cha kati; na
  - (c) kundi lenye kipato cha chini
- na gharama zake ni kama ilivyoainishwa katika Jedwali “A” la Sheria Ndogo hizi.
- (3) Mmiliki wa biashara na taasisi yoyote atawajibika kulipa gharama za ukusanyaji taka kama ilivyoainishwa katika Jedwali “A” la Sheria Ndogo hizi.
- (4) Pasipo kujali kifungu chochote cha Sheria Ndogo hizi, mtu yeyote atakayeshindwa au kukataa kulipa ada kwa wakati atatozwa adhabu ya 25% ya ada ya ukusanyaji taka.
- (5) Ada kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii zitalipwa hadi kufikia tarehe 5 ya mwezi unaofuata.

***Wakala***

39. –(1) Mamlaka inaweza kumteua mtu, kampuni au kikundi cha kijamii kuwa wakala wa kutoa huduma za usafishaji na ukusanyaji taka kama itakavyoelekezwa na mamlaka mara kwa mara kadiri itakavyo lazimika.
- (2) Wakala atakayeteuliwa chini ya Sheria Ndogo hizi atahakikisha kuwa anakusanya na kuzitupa taka hizo kwenye sehemu maalum iliyoandaliwa kwa madhumuni hayo.
- (3) Ili kuhakikisha kwamba kila mtu anashiriki ipasavyo katika kulinnda usafi wa mazingira Mamlaka inaweza kumtumia wakala atakayeteuliwa kwa mujibu wa kifungu cha 11(1) hapo juu au kuteua kampuni au kikundi cha kijamii kufanya kazi ya kuwakamata na kuwatoza adhabu za papo kwa papo au kuwapeleka mahakamani watu watakao bainika kuchafua mazingira.

***Ukaguzi***

40. Mamlaka itakuwa na uwezo wa kufanya ukaguzi katika majengo na maeneo yote mengine yaliyoko ndani ya mipaka yake katika usimamizi na utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi na inaweza kutoa taarifa ya maandishi kwa mmiliki wa jengo au eneo au mkazi wa jengo husika ili kuondoa chukizo lililopo.

***Kiwanja kisicho endelezwa***

41. –(1) Ili kuepuka madhara yatokanayo na uchafu mmiliki wa eneo lolote lisiloendelezwa hataruhusiwa kutupa au kuweka taka za aina yoyote katika eneo lake.  
(2) Itakuwa ni kosa chini ya Sheria Ndogo hizi kwa mmiliki wa kiwanja chochote kuweka na kuviacha vifaa vya ujenzi katika kiwanja chake zaidi ya muda uliowekwa kwenye kibali cha ujenzi.

***Gharama za matumizi ya jaa la taka***

42. Mamlaka italazimika kutoza gharama za utupaji wa taka katika jaa kutoka kwa mawakala, wamiliki wa taasisi mbalimbali, viwanda na makampuni pamoja na wazalishaji wengine wa taka kwa viwango vilivyoainishwa katika **Jedwali “C”** la Sheria Ndogo hizi.

***Adhabu***

43 (1) . Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi Shilingi za Kitanzania Elfu Hamsini au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja yaani faini na kifungo.

(2) Mtu yeyote atakayemzuia mtu mwingine kutekeleza sheria ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na atatozwa faini isiyozidi (300,000/=) laki atu au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja

**JEDWALI “A”**

**GHARAMA ZA UKUSANYAJI TAKA KATIKA MAJENGO YAMAKAZI NA BIASHARA**

(Chini ya Kifungu cha 10)

Na.	Aina ya biashara	Viwango kwa Mwezi
1. 1	Makazi (Kaya)	
2.	(a) Kundi lenye kipato cha juu	5000/=
	(b) Kundi lenye kipato cha kati	3000/=
	(c) Kundi lenye kipato cha chini	2000/=
3.	Mgahawa mdogo	1000/=
4.	Mgahawa mkubwa	2000/=
5.	Nyumba ya kulala wageni	10,000/=
6.	Zahanati (taka zisizo hatari)	5,000/=
7.	Kituo cha afya (taka zisizo hatari)	10,000/=

8.	Hospitali	15,000/=
9.	Hospitali ya rufaa	25,000/=
10.	Kiwanda cha kuuza na kupasua mbao	20,000/=
11.	Fundi seremala wakubwa	15,000/=
	Fundi seremala wa kati	10,000/=
	Fundi seremala wadogo	5,000/=
12.	Fundi chuma/Duka la kutengneza vifaa vya aluminiam	10,000/=
13.	Karakana	10,000/=
14.	Kiwanda kidogo	25,000/=
	Kiwanda kikubwa	50,000/=
15.	Duka la jumla	10,000/=
	Duka la rejereja/huduma	7,000/=
16.	Shule ya Msingi ya Bweni (binafsi)	10,000/=
	Shule ya msingi ya kutwa (binafsi)	5,000/=
17.	Shule ya Sekondari ya kutwa (binafsi)	5,000/=
	Shule ya Sekondari ya Bweni (binafsi)	10,000/=
18.	Kituo cha kulelea watoto	0
19.	Kituo cha kutunzia watu wenye mahitaji maalum	0
20.	Duka dogo la mazao chakula	5,000/=
21.	Duka kubwa la mazao ya chakula	30,000/=
22.	Baa	10,000/=
23.	Klabu ya usiku	10,000/=
24.	Kumbi za Sherehe	10,000/=
25.	Duka la kuuza nyama na samaki	5,000/=
26.	Duka la dawa za Mifugo, binadam na mimea	10,000/=
27.	Dobi mdogo	1,000/=
28.	Dobi mkubwa	5,000/=
29.	Fundi wa vifaa vya umeme m.f jiko, jokofu, Luninga, pasi, redio n.k	5,000/=
30.	Fundi kushona kwa kila cherehani	1,000/=
31.	Saluni	2,000/=
32.	Kituo cha kuuza mafuta	20,000/=

33.	Ghala	10,000/=
34.	Hoteli:	10,000/=
35.	Taasisi	5,000/=
36.	klabu ya pombe ya asili	2,000/=
37.	Kituo cha michezo/Mazoezi	5,000/=
38.	Washona viatu	1,000/=
39.	Stoo za mkaa	2,000/=
40.	Mama lishe/Baba lishe	1,000/=
41.	Duka la kuuza Magari	20,000/=
42.	Vituo vya kuoshea magari	3,000/=
43.	Aina nyingine ya biashara/huduma ambayo haikutajwa hapo juu.	Ada itapangwa na kamati ya kudumu husika na chanzo hicho kila itakapo hitajika.

#### **JEDWALI “B”**

#### **GHARAMA ZA UBOMOAJI NA UONDOAJI WA MABAKI YA VIFAA VYA UJENZI**

[Chini ya Kifungu cha 34(2)]

<b>NA.</b>	<b>ENEO KWA MITA YA UJAZO</b>	<b>KIWANGO KWA MWEZI</b>
1	Mita moja ya mraba	5,000/=

#### **JEDWALI “C”**

#### **GHARAMA ZA UTUPAJI TAKA KWENYE JAA LA TAKA**

(Chini ya Kifungu cha 42)

<b>NA.</b>	<b>KIASI CHA TAKA</b>	<b>KIWANGO</b>
1	Tani moja kwa safari	50,000/=
	Chini ya Tani moja kwa safari	40,000/=

#### **JEDWALI HATI YA KUKIRI KOSA**

Tarehe.....

Hati Na..... ya mwaka 20.....

Mimi.....  
.... nakiri Chini ya kifungu cha 8 cha Sheria Ndogo hizi za (Usafi na Hifadhi ya Mazingira)  
za Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua za Mwaka ,2014 kutenda makosa yafuatayo:-

- 1.....
- 2.....
- 3.....
- 4.....
- 5.....

Kwa hiari yangu ninakubali kuadhibiwa kwa kulipa faini ya Shilingi.....(kwa maneno:.....)  
badala ya kushitakiwa mahakamani kwa makosa haya.

Saini ya Mkosaji..... Tarehe.....

ADHABU/FAINI HII IMETOLEWA NA:-

Jina.....  
Cheo.....

Saini..... Tarehe.....

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua ilibandikwa katika Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe.....mwezi.....mwaka 2014 na nembo hiyo ilibandikwa mbele ya;-

.....  
**ABDALLAH S.NGODU**  
Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.

.....  
**JOHN KADUTU**  
Mwenyekiti,  
Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.

NIMEKUBALI.

.....  
**MHE.MIZENGO P.PINDA(MB)**  
WAZIRI MKUU.

Dodoma  
Tarehe.....2014.

TANGAZO LA SERIKALI Na. .... La tarehe .....

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(Sura ya 290)

**SHERIA NDOGO**

*Zimetugwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16 (1)*

**SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MAZAO) ZA HALMASHAURI  
YA WILAYA YA KALIUA ZA MWAKA 2014**

- |                            |   |
|----------------------------|---|
| Jina na mwanzo wa kutumika | 1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ushuru wa Mazao) za Halmashauri ya wilaya ya Kaliua za mwaka 2014 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.   |
| Eneo la matumizi           | 2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililopo chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.  |
| Tafsiri                    | 3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo<br>“Afisa Mwidhinishwa” maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekerezaji wa Sheria Ndogo hizi;<br><br>“Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua;<br><br>“Mazao” maana yake ni mazao yote yatokanayo na zao la kilimo;<br><br>“Mkurugenzi” maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua pamoja na Afisa yeyote wa umma aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.<br><br>“Mmiliki” maana yake ni mtu yeyote mwenye chombo cha usafiri ikiwa ni pamoja na dereva wa gari lililobeba mazao ya kilimo;<br><br>“Mnunuzi” maanayake ni mtu taasisi kikundi cha watu, kampuni au kiwanda au shirika linalonunua mazao ya biashara katika eneo la Halmashauri. |



“*Muuzaji*” maana yake ni mtu, taasisi, kikundi cha watu, kampuni au kiwanda kilichoko au shirika linalonunua mazao ya biashara katika eneo la Halmashauri;

“*Ushuru*” maana yake ni malipo anayotoa mtu yeyote muuzaji mfanyabiashara kwa muujibu wa Sheria Ndogo hizi;

Ushuru	4. - (1) Kutakuwepo na Ushuru wa Mazao ambao utatozwa na kukusanywa na Halmashauri kwa mazao yatakayosafilishwa na Kuingizwa ndani ya Halmashauri ya Wilaya Kaliua kama ilivyoonyeshwa katika jedwali A na B (2) Ushuru huo utalipwa na mnunuzi wa mazao kutoka kwenye eneo ambalo zao au mazao hayo yanazalishwa ndani ya Halmahauri.
Kibali	5. – (1) Ushuru wa mazao utalipwa kwa Halmashauri au kwenye mamlaka ya soko lililotengwa na Halmashauri au kijiji kwa ajili ya kuuza na kununua mazao.  (2) Kikundi, Chama au kampuni iliyosajiliwa vinaweza kununua mazao kwa taratibu zinazowekwa na Halmashauri na vitalipia ushuru ulivyowekwa na Sheria Ndogo hizi.
Wajibu wa Mnunuzi	6. Kila mnunuzi atatakiwa kuhakikisha kwamba mazao anayosafirisha yamelipiwa ushuru kwa muujibu wa Sheria Ndogo hizi
Muda wa kusafirija mazao	7. Mazao yote yatasafirishwa kuanzia saa 1:00 asubuhi hadi 12:00 jioni
Mamlaka ya Afisa Muidhiniwa	8. – (1) Afisa muidhinishwa anaweza :-  (1) Kuingia katika jengo au sehemu yoyote inayohifadhia mazao kusimamia utekerezaji wa Sheria Ndogo hizi;  (2) Kusimamia chombo chochote cha usafiri ikiwa ana sababu za kuamini kuwa mazao yanayo safirishwa hayajalipiwa ushuru.  (3) Kumtaka mnunuzi yeyote kuonyesha risiti aliyo lipia ushuru ;
Makosa	9. Mtu yeyote ambaye :-  (a) atanunua na kusafirisha mazao bila kulipia ushuru

- (b) atakataa au kukwepa kulipa ushuru
- (c) atamshawishi mtu au kundi la watu wasilipe ushuru
- (d) atalipa ushuru pungufu au kidogo usiolingana na thamani ya mazao aliyonunua.
- (e) atasafirisha mazao usiku.
- (f) atamzuia au kumsababishia Afisa Muidhiniwa kutekeleza majukumu yake
- (g) atakwepa kizuizi(geti) na kupita pembembeni mwa barabara.
- (h) Atagonga geti lilowekwa na wakala au Halmashauri

atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili jela au adhabu zote mbili kwa pamoj yaani faini na kifungo

#### **JEDWALI A**

##### **Ushuru wa kuingiza Mazao ndani ya Wilaya**

- i. Mahindi gunia kg 100 tsh 1500/=
- ii. Maharage gunia kg 100 tsh 1500/=
- iii. Mchele kg 100 tsh 2000/=
- iv. Mpunga gunia kg 100 tsh 1500/=
- v. Karanga zilizomenywa tsh 1500/=
- vi. Karanga ambazo hazijamenywa tsh 1000/=
- vii. Mihigo kg 100 tsh 1000
- viii. Choroko,Mbaazi,Kunde,Nyonyo,ufuta,ndegu,na Fiwi kg 100 tsh 1500/=
- ix. Viazi Mviringo kg 100 tsh 1000/=
- x. Viazi vitamu kg 100 tsh 1000/=
- xi. Mawese,Alizert Kg 100 tsh 1000/=
- xii. Daga gunia kg 100 tsh 1500/=
- xiii. Ndizi mkungu kg 100 tsh 500/=
- xiv. Tikiti maji tenga kg 100 tsh 500/=
- xv. Machungwa,embe,machenza,malimau na nanasi kg 100 tsh 500/=

#### **JEDWALI B**

##### **Ushuru wa kusafirisha Mazao nje ya Wilaya,**

- i. Mahindi gunia kg 100 tsh 1500/=
- ii. Maharage gunia kg 100 tsh 1500/=
- iii. Mchele kg 100 tsh 2000/=
- iv. Mpunga gunia tsh 1500/=
- v. Karanga zilizomenywa tsh 1500/=
- vi. Choroko,Mbaazi,Kunde,Nyonyo,ufuta,ndegu,na Fiwi

- kg 100 tsh 1500/=
- vii. Viasi Mviringo kg 100 tsh 1000/=
  - viii. Viasi vitamu kg 100 tsh 1000/=
  - ix. Mawese, Alizert Kg 100 tsh 1000/=
  - x. Daga gunia kg 100 tsh 1500/=
  - xi. Ndizi mkungu kg 100 tsh 500/=
  - xii. Tikiti maji tenga kg 100 tsh 500/=
  - xiii. Machungwa, embe, machenza, malimau na nanasi kg 100 tsh 500/=

## **HATI YA KUKILI KOSA**

### **(Chini ya kifungu cha 13)**

Mimi.....nakiri  
 mbele ya.....Mkurugenzi Mtendaji wa  
 Halmashauri ya Kaliua kwamba mnamo tarehe .....ya mwezi  
 .....mwaka.....nilitenda kosa la kukiuka masharti ya  
 kifungu cha .....cha Sheria Ndogo za (Ushuru wa Mazao)  
 za Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua ya mwaka 2013. Nipo tayari  
 kulipa kiasi cha ada/au ushuru ninaodaiwa pamoja na faini ikiwa  
 Mkurugenzi ataamua kutekeleza mmlaka aliyopewa chini ya Sheria  
 Ndogo zilizotajwa hapo juu.  
 Nathibitisha kwamba maelezo ya hapo juu ni kweli nimeyatoa kwa  
 hiari yangu kadri  
 ya ufahamu wangu.  
 Tarehe.....  
 Saini.....

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua libandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe .....Mwezi.....2014 na nembo ilibandikwa mbele ya:

.....  
**ABDALLAH S.NGODU**  
*Mkurugenzi Mtendaji*  
*Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua*

.....  
**JOHN KADUTU**  
*Mwenyekiti,*  
*Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.*

*NIMEKUBALI.*

.....  
**MHE. MIZENGO P.PINDA(MB)**  
**WAZIRI MKUU**

**Dodoma,**  
**Tarehe.....2014**

TANGAZO LA SERIKALI Na. .... La tarehe .....

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(Sura ya 290)

**SHERIA NDOGO**

*Zimetugwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16 (1)*

**SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA SAMAKI) ZA HALMASHAURI YA  
WILAYA YA KALIUA NA MWAKA 2014**

Jina la sheria	1.Sheria ndogo hizi zitajulikana Kama Sheria Ndogo za (Ushuru wa Samaki) za Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua za mwaka 2014 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali
Mwanzo wa kutumika	2.Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua
Tafsiri	3.Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo;- “Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua. “Ushuru” maana yake ni malipo yanayolipwa na mtu au watu kwa ajili ya ushuru wa samaki na daga; “Wakala” maana yake ni mtu yeyote, kampuni, taasisi au asasi iliyoteuliwa na Halmashauri kukusanya ushuru kwa niaba yake.
Ushuru	3. - (1) Kutakuwa na ushuru wa samaki ambao utalipwa kwa Halmashauri au kwa wakala wake kutoka kwa kila mnunuzi wa samaki wanaotoka au kuingizwa kwenye eneo la Halmashauri kwa viwango vilivyooneshwa kwenye jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.  - (2) Ushuru huo utalipwa kwenye maeneo yaliyobainishwa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi pamoja na mahali popote ambapo Halmashauri itatenga kama eneo malumu kwa ajili ya kulipa ushuru wa samaki.
Wajibu wa mkusanya ushuru	4. Itakuwa ni wajibu wa mkusanya ushuru kutoa stakabadhi yenye nembo ya Halmashauri kwa mtu yeyote aliyelipa ushuru.Mlipa

	ushuru atahakikisha kuwa anapata stakabadhi hiyo baada ya kulipa ushuru huo																		
Makosa	5. Mtu yeyote ambaye:- (a) atakataa au kushindwa kulipa ushuru (b) atamshawishi mtu au kundi la watu wasilipe ushuru.																		
Adhabu	atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atalipa faini ya shilingi elfu 50,000/=au kifungo kisichozidi miezi sita jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.																		
	<p><b>JEDWILI LA KWANZA</b></p> <table border="1"> <thead> <tr> <th>Bidhaa</th> <th>Kiasi</th> <th>Ushuru</th> </tr> </thead> <tbody> <tr> <td>1. Samaki au dagaa</td> <td>gunia</td> <td>2000/=</td> </tr> <tr> <td>2. Samaki au dagaa</td> <td>tenga kubwa</td> <td>2000/=</td> </tr> <tr> <td>3. samaki au dagaa</td> <td>tenga la kati</td> <td>1000/=</td> </tr> <tr> <td>4. Samaki au dagaa</td> <td>tenga dogo</td> <td>8.000/=</td> </tr> <tr> <td>5. Samaki au dagaa</td> <td>kiroba</td> <td>5.000/=</td> </tr> </tbody> </table> <p>6. Ada ya kibali tsh 9500 kwa mtu mmoja mwenye tenga la samaki kwa Mwezi.</p> <p style="text-align: center;"><b>HATI YA KUKILI KOSA</b></p> <p style="text-align: center;"><b>(Chini ya kifungu cha 13)</b></p> <p>Mimi.....nakiri mbele ya.....Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Kaliua kwamba mnamo tarehe .....ya mwezi .....mwaka.....nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha .....cha Sheria Ndogo za (ushuru wa Samaki) za Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua ya mwaka 2014. Nipo tayari kulipa kiasi cha ada/au ushuru ninaodaiwa pamoja na faini ikiwa Mkurugenzi ataamua kutekeleza mamlaka aliyopewa chini ya Sheria Ndogo zilizotajwa hapo juu. Nathibitisha kwamba maelezo ya hapo juu ni kweli nimeyatoa kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu.</p> <p>Tarehe..... Saini.....</p>	Bidhaa	Kiasi	Ushuru	1. Samaki au dagaa	gunia	2000/=	2. Samaki au dagaa	tenga kubwa	2000/=	3. samaki au dagaa	tenga la kati	1000/=	4. Samaki au dagaa	tenga dogo	8.000/=	5. Samaki au dagaa	kiroba	5.000/=
Bidhaa	Kiasi	Ushuru																	
1. Samaki au dagaa	gunia	2000/=																	
2. Samaki au dagaa	tenga kubwa	2000/=																	
3. samaki au dagaa	tenga la kati	1000/=																	
4. Samaki au dagaa	tenga dogo	8.000/=																	
5. Samaki au dagaa	kiroba	5.000/=																	

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua libandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia  
Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika  
tarehe .....Mwezi.....mwaka 2014 na nembo hiyo ilibandikwa mbele ya:

.....

**ABDALLAH S.NGODU,**  
*nMkurugenzi Mtendaji*  
*Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua*

.....

**JOHN KADUTU**  
*Mwenyekiti ,*  
*Halmashauri ya wilaya Kaliua.*

*NIMEKUBALI,*

.....  
**MIZENGO P.PINDA (MB)**  
**WAZIRI MKUU**

Dodoma  
Tarehe.....2014





